

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 28 Aprili, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MADINI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Manya. Nimwite sasa Waziri wa Katiba na Sheria. Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pinda.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria; kwa niaba yake Mheshimiwa Ng'wasi D. Kamani.

MHE. NG'WASI D. KAMANI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2021/2022. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge naamini makofi hayo ni kwa viongozi wa Kamati hii, wanalea vizuri vijana kwenye Kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Kigua.

MHE. OMARI M. KIGUA - K.n.y. MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2021/2022. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kigua.

Waheshimiwa tunaendelea. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 148

Hitaji la Vituo vya Afya – Kata za Jimbo la Segerea

MHE. BONNAH L. KAMOLI aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaongeza Vituo vya Afya katika Kata za Jimbo la Segerea Pamoja na kupandisha hadhi Zahanati za Kinyerezi, Segerea, Kipawa na Yombo Kiwalani ili kuondoa adha kwa wananchi wa Kata 13 wanaotegemea Kituo kimoja cha Afya?

(b) Je, ni lini Kata za Minazi Mirefu, Buguruni, Kimanga na Kisukuru zitapatiwa Zahanati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha huduma za afya katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali iliipatia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam; iliyokuwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Mwezi Februari 2021, Serikali imeipatia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu kwenye Hospitali ya Halmashauri na imetenga shilingi milioni 500 katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 na 2019/2020, Serikali iliipatia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Guluka Kwalala na upanuzi wa Kituo cha Afya Buguruni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia mapato yake ya ndani, imetenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili

ya ujenzi wa vituo vitatu vya afya na shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya kuongeza miundombinu katika zahati tano ili ziweze kupandishwa hadhi kuwa vituo vya afya zikiwemo Zahanati za Kinyerezi na Kiwalani katika Jimbo la Segerea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya kukamilisha maboma matano ya zahanati katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam zikiwemo Zahanati za Bonyokwa na Tabata zilizopo katika Jimbo la Segerea. Aidha, kuitia mapato ya ndani, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imetenga shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kulipa fidia kwenye maeneo ambayo yatachukuliwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya huduma za afya katika Jimbo la Segerea na nchini kote ili kuendelea kuboresha huduma za afya kwa wananchi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bonnah Kamoli, swali la nyongeza.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Ahsante. Pamoja na majibu mazuri ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili nyongeza. Swali la kwanza: Je, ni lini Serikali itaanza kupanga vituo vya afya kutoptana na wingi wa watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Sera ya Serikali ni kila Kata kuwa na Kituo cha Afya na Kila Mtaa uwe na Zahanati: Je, ni lini Serikali italeta vituo vya afya katika Kata ya Kimanga, Kisukuru, Buguruni pamoja na Minazi Mirefu ili hawa wananchi waweze kuondokana na matatizo hayo?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ni kweli kwamba

tunajenga Vituo vya Afya, Zahanati na Hospitali za Halmashauri katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia: kwanza, ukubwa wa kijigrafia wa maeneo hayo; na pili, idadi ya wananchi katika maeneo husika ili kuhakikisha vituo vile vinasogezza huduma za afya karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Bonnah kwamba Serikali imeendelea kujenga vituo vya afya kwa kuzingatia vigezo hivyo viwili; kigezo cha ukubwa wa jimbo au halmashauri na pia kigezo cha idadi ya wananchi. Kwa mfano, katika Jiji la Dar es Salaam, miaka miaka mitano iliyopita, zaidi ya vituo vya afya 12 vimeendelea kujengwa na Hospitali za Wilaya zimeendelea kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ujao wa 2021/2022 katika Manispaa ya llala kwa maana ya Jiji la Dar es Salaam peke yake, kuna vituo vya afya vipatavyo sita vitakwenda kujengwa, pamoja na Hospitali ya Halmashauri na katika Halmaashauri zote za Jiji la Dar es Salaam zitakwenda kujenga angalau vituo vya afya vitatu. Kwa hiyo, tunaona Serikali imeendelea kuhakikisha inaongeza idadi ya vituo vya afya katika Manispaa na Jiji la Dar es Salaam kwa kuzingatia idadi ya wananchi; na suala hili linafanyika kwa utaratibu huu nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Sera ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo ya Msingi ni kuhakikisha kila Kata inakuwa na Kituo cha Afya na Zahanati katika Vijiji. Sera hii imeendelea kutekelezwa kwa vitendo na Waheshimiwa Wabunge wamekuwa mashahidi kwamba Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa sana katika ujenzi wa zahani na vituo vya afya katika kata zetu. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi kwa vituo vya afya ambavyo tayari Serikali imeanza kujenga na katika kata hizo ambazo Mheshimiwa Kamoli amezitaja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Jitihada za kujitolea ambazo wananchi wa Jimbo la Segerea wamezionesha, zinafanana sana na jitihada ambazo wananchi wa Jimbo la Nkasi Kaskazini wamezionesha katika kata 17 tunavituo vya afya viwili lakini kuna vituo ambavyo tayari vimeanzishwa kwa nguvu za wananchi. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwenye Kata ya Kabwe ili kuheshimu na kuendelea kuhamasisha wananchi kujitolea? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini pamoja na wananchi wa Nkasi Kaskazini kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya kuhakikisha wanachangia nguvu zao katika ujenzi wa miradi ya maendeleo vikiwemo vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua na inathamini sana nguvu za wananchi na tutaendelea kuhakikisha tunatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ambayo wananchi wameanza kuyajenga kwa nguvu zao na mfano mzuri katika bajeti ya mwaka ujao maboma zaidi ya 108 kwa maana ya vituo vya afya vitakwenda kujengwa kwa mapato ya ndani ya halmashauri na vituo vya afya 18 vitakwenda kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna vile zahanati maboma 578 yatakwenda kujengwa.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba katika mpango huu ujao pia katika Jimbo hili la Nkasi Kaskazini tutakwenda kulipa kipaumbele kuhakikisha kwamba wananchi wanaona matunda ya Serikali yao katika kujali nguvu ambazo wameziweka katika maboma yale.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jerry Silaa, swali la nyongeza.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeendelea kutenga fedha na kupeleka fedha kwenye Hospitali ya Wilaya ya Kivule na tayari Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imepokea shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi na shilingi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Afya ya Kinywa na Meno.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutenga fedha na kupeleka kwenye Kituo cha Afya cha Mama na Mtoto, Chanika ili kiweze kujengewa wodi na kuweza kupanda hadhi kuwa hospitali kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya wananchi wa Kata za Chanika, Zingiziwa, Msongola, Majohi na Buyuni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Jerry Silaa kwa kusimamia kwa karibu sana miradi mbalimbali ya maendeleo katika Jimbo la Ukonga. Kwa kweli Serikali imeendelea kushirikiana sana kwa karibu na wananchi pamoja na Mbunge wa Ukonga kuhakikisha vituo vya afya hivyo alivyovitaja Kivule na pia kuhakikisha fedha zaidi ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali zimepelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Chanika kwa sasa kinatoa huduma kwa akina mama wajawazito, lakini Serikali inaona kuna kila sababu ya kutenga fedha ili kuongeza miundombinu ya huduma za afya katika Kituo cha Afya cha Chanika ili pamoja na huduma za Afya ya Mama na Mtoto kianze kutoa huduma nyingine kwa wagonjwa ili kusogeza huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba katika mipango ya Serikali, tutakipa kipaumbele Kituo cha Afya cha Chanika ili kiweze kupata fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo na kuhakikisha kwamba huduma zote za afya zinasogezwa kwa wananchi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Magomeni, sasa aulize swali lake.

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nifanye masahihisho. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Magomeni, Zanzibar. Halafu katika jibu langu ameandika Mwanahamisi, ni Mwanakhamis. Ni k, h.

NAIBU SPIKA: Kwangu inasomeka sawa sawa. Ngoja, ngoja, ngoja twende vizuri. Kwanza umebisha hii Magomeni. Ulitaka iandikweje? Wewe sio Mbunge wa Magomeni? Maana huku Bara hakuna Jimbo linaitwa Magomeni.

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mbunge wa jimbo, huku wameniandika Mbunge wa Viti Maalum.

NAIBU SPIKA: Aaah sawa. Basi huku kwangu inasomeka Magomeni, ndio maana nimekutaja Magomeni. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi, taarifa itakaa vizuri.

Na. 149

**Fidia kwa Wastaifu Ofisi ya Makamu wa
Rais Zanzibar**

MHE. MWANAHAMIS KASSIM SAID aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa waliokuwa Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano waliostaafishwa kwa maslahi ya Umma tarehe 30 Juni, 1996?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA (MHE. HAMAD HASSAN CHANDE)**
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu ya Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said wa Jimbo la Magomeni, Zanzibar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipokea malalamiko ya wastaa fu saba waliopunguzwa kazini kwa manufaa ya Umma mwaka 1996. Baada ya uchambuzi wa suala hili na kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango, ilibainika kwamba stahili zao zote zilishalipwa kipindi walipostaa fishwa. Hivyo, hawastahili kulipwa pensheni kutokana na masharti yao ya ajira, bali walilipwa kiinua mgongo cha mkupuo ambacho ni stahili ya watumishi walioajiriwa chini ya masharti ya *"Operational Services."* Hii ni kwa mujibu wa Kanuni Na. 6 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi Serikalini za Mwaka 1994 na Sheria Na. 36 ya Mwaka 1964 (*The National Provident Fund Act*).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, swalii la nyongeza.

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa wazee hawa walifanya kazi kwenye Serikali hii, walitumia vigezo gani kuwa walipwe kiinua mgongo na wasilipwe pensheni yao ya kila mwezi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili: Je, Waziri yuko tayari kwa ruhusa yako kuungana nami kwenda kuwaona wazee hawa kuwapa maneno mazima? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA (MHE. HAMAD HASSAN CHANDE):**
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana
Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said wa Jimbo la
Magomeni kwa juhudi yake ya kufuatilia wazee kupata stahiki
zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo ambavyo tumetumia
ni Kanuni, Taratibu na Sheria ambazo zimewekwa na kama
hatukutumia vigezo hivyo, basi ingekuwa ni kinyume na
taratibu. Hivyo basi, Serikali bado iko na usikivu. Serikali yetu
ni sikivu, Mheshimiwa Mbunge anao uwezo wa kupeleka
malalamiko tena na tutayazingia kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Swalii la pili, niko tayari
kabisa mimi na Waziri wangu kufuatana naye kwenda
kushuhudia jambo hilo, *Inshaallah. (Makofii)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Maliasili na
Utalii, Mheshimiwa Cecilia Parezzo, Mbunge wa Viti Maalum,
sasa aulize swalii lake.

Na. 150

**Wanyama Wanaovamia Mashamba ya
Wananchi Ngorongoro**

MHE. CECILIA D. PARESSO aliuliza:-

Wananchi wanaoishi jirani na Mamlaka ya Hifadhi ya
Ngorongoro Wilayani Karatu kwa muda mrefu wamekuwa
wakipata adha kubwa ya wanyama kuingia na kuvamia
mashamba yao na wakati mwininge kujeruhi wananchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na
Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Cecilia Daniel Parezzo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na shughuli za kibinadamu zikiwemo kilimo na ufugaji kwenye shoroba za wanyama, maeneo ya mtawanyiko wa wanyamapori na maeneo ya kinga ya Hifadhi ya Ngorongoro, kumekuwepo na changamoto ya wanyamapori kuingia kwenye mashamba yaliyopo pembezoni mwa hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hii, Wizara inatoa rai kwa wananchi kutumia mbinu mbadala za kuepuka wanyamapori wakali na waharibifu kuingia kwenye maeneo yao. Mbinu hizo ni pamoja na kwanza, ni kuanzisha miradi ya ufugaji nyuki kwenye mipaka ya Hifadhi zilizo karibu na maeneo ya vijiji ili kuhakikisha kuwa wanyamapori hawavuki kwenda kwenye mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbinu nyingine ni wananchi wanahamasishwa kulima zao la pilipili kandokando ya mashamba yao, kwani zao hili limeonekana kuwa ni tishio kwa wanyama wakali na waharibifu kama tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbinu nyingine ni wananchi wanashauriwa kutopanda mazao yanayovutia tembo kusogea katika mashamba yao kama vile mazao yanayohusiana na katani, miwa, ndizi na matikiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wananchi kuendelea kutumia *oil chafu* iliyochanganywa na pilipili na majivu ili kuzuia wanyama kama tembo kusogea kwenye maeneo ya mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni wananchi wanashauriwa sasa kutoa taarifa haraka pindi wanyama hao wanapoonekana kukaribia kwenye maeneo ya mashamba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za kuongezeka kwa matukio mbalimbali ya wanyama wakali wakiwemo tembo, Wizara imeongeza idadi ya vituo vya muda na vya kudumu vya askari katika maeneo yaliyohifadhiwa likiwemo eneo la Ngorongoro (Wilaya ya Karatu) na kuendelea na doria za usiku kuhakikisha wanyamapori waharibifu wanarudishwa hifadhini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa katika majibu ya Serikali wanaonesha kabisa kwamba mbadala wa wanyama hawa kutokuingia kwenye maeneo ya wananchi ni kutumia mbinu zilizoainishwa hapa, lakini mbinu hizi zinahitaji wananchi waelimishwe na wawezeshwe kwa sababu unapomwambia afuge nyuki na kadhalika, mwananchi huyu hana huo uwezo. Sasa je, Serikali inafanya nini kuwawezesha wananchi hawa kama kweli wana uhakika hili ndiyo litakuwa suluhisho ya kuondoa kero hii ya muda mrefu ya wanyama kuingia kwenye maeneo ya wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wananchi wanapoingia kwenye maeneo wakaribu mazao, fidia inayolipwa hailingani na uharibifu uliotokea, lakini hata fidia hiyo inayolipwa inachukua miaka na miaka mwananchi kupata fidia hiyo. Je, ni lini sasa Serikali italeta sheria hapa Bungeni tufanyie marekebisho ili wananchi waweze kupata haki yao kwa jinsi ambavyo wanastahili? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya

nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imekiri kwamba kumekuwa na changamoto ya hawa wanyama wakali wakiwemo tembo kuendelea kuvamia mashamba ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii tumeendelea kuiongelea hata katika Bunge lako hili Tukufu kwamba kwa kuwa wananchi wameendelea kusogea kwenye maeneo ya hifadhi na asilimia kubwa ya maeneo ambayo shughuli za kilimo zinafanyika ni ushoroba wa wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni changamoto kwa sababu wanyama hao sasa badala ya kupita yale maeneo wakaenda kwenye shughuli zao zingine zikiwemo pamoja na kutafuta madini pamoja na dawa asili wanazotumia ambazo sisi wanadamu hatuwezi kuzitambua, lakini wao kama nilivyokuwa nikiendelea kusema, wana Serikali yao, basi yale maeneo sasa wanapokutana na mazao wanafanya vurugu ambayo sio ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kuhamasisha wananchi kama wataweza waachane na mazao yanayohamasisha tembo kupita katika maeneo ya mashamba yao. Kama itashindikana sana basi kwenye jibu langu lile la msingi nimeelezea mbinu mbadala ya kuweza kusaidia ili angalau kuepuka hili tatizo linaloendelea kujitokeza kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kutoa elimu kwenye maeneo husika na kupitia vyombo vy ya habari na hata hapa naendelea kutoa rai kwa wananchi kwenye maeneo ambayo mashamba yao yanavamiwa na tembo, wafuate haya tunayoelekeza ili wasaidie. Wapande pilipili, waweke hiyo mizinga ya nyuki, lakini pia waendelee kutoa taarifa kwa Serikali kwa sababu Serikali iko kwa ajili yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu fidia. Lengo la Serikali si ku-*compensate* mpaka mwananchi afurahi. Tukisema kila mwananchi apate kile ambacho anakusudia, basi hii Wizara haina haja ya kuwepo kazini kwa sababu uhifadhi ni gharama kubwa sana, lakini pia hata tunapotekeleza tunahakikisha kwamba tunahifadhi ili kuendelea kuiongezea Serikali mapato kupitia utalii, lakini kwa wakati huo huo tunaendelea ku-*compensate* wananchi wanaoathirika na hao wanyama. Kwa hiyo niombe rai kwa wananchi...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge, ameelewa.

Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali kwa kifupi.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa fursa hii. Niseme kwamba kutohana na jitihada za wananchi wetu kule Vunjo kupanda miti na kuitunza kwenye mashamba yao ya kahawa na ndizi, ngedere na tumbili wameongezeka sana mpaka wamekuwa tishio kwa maisha ya watoto wachanga wanaoachwa nyumbani na ni vigumu sana kupambana na ngedere na tumbili kwa vile wana akili kama binadamu. Sasa nataka nijue, je Serikali ina suluhisho gani kuhusiana na ongezeko hili kuwaondoa hawa ngedere na tumbili? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kimei kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli changamoto hii ipo katika Mkoa wa Kilimanjaro na wiki iliyopita tu tulienda kuangalia changamoto hii katika Wilaya ya Rombo na kukawa kuna changamoto ya nyani pamoja na hao ngedere. Wizara ya Maliasili na Utalii ilitoa tamko kwamba tutaenda kuwahamisha hao nyani pamoja na ngedere,

tuwapeleke kwenye maeneo ya hifadhi ambako kutafaa zaidi. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Thecla Ungele, swali la nyongeza.

MHE. TECLA M. UNGELE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kadha inayowapata wananchi wa Karatu ndiyo hiyo inayowapata wananchi wa Mkoa wa Lindi Wilaya ya Kilwa, Liwale, Lindi Vijiji, Nachingwea. Hata hivi juzi tu Wilaya ya Liwale, Kata ya Mbaya kuna mwananchi kule ameuawa na tembo. Pia wanaharibu mashamba ya vyakula na mazao kiasi kwamba wananchi wanaendelea...

NAIBU SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. TECLA M. UNGELE: Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo hili la wanyama kule Nachingwea, Liwale na Kilwa ili wananchi wa huko nao wawe na maisha mazuri? Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum Lindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimekwishakuelezea kwenye jibu langu la msingi nimetoa rai kwa wananchi kupanda mazao ambayo yanaweza yakaepusha hawa wanyama. Hata hivyo, tukumbuke kwamba tunaishi kwenye maeneo ambayo yalikuwa ni njia za wanyama na tukumbuke kwamba hawa wanyama walikuwepo kabla hata ya sisi kuwepo.

Kwa hiyo, wanyama siku zote wanaenda kwenye maeneo yao ya siku zote ambayo sisi ndiyo tumefanya mashamba. Niwaombe wananchi tena kwamba waendelee kupanda mazao haya ambayo tunahamasisha, lakini

ikishindikana basi wasilime kwenye maeneo ambayo yako kandokando ya hifadhi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jafar Sanya Jussa, Mbunge wa Paje, sasa aulize swalii lake.

Na. 151

Hitaji la Samani Vituo vya Polisi Paje na Jambiani

MHE. JAFAR SANYA JUSSA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itavipatia Vituo vya Polisi vya Paje na Jambiani samani za Ofisi pamoja na magari kwa ajili ya doria?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jaffar Sanya Jussa, Mbunge wa Paje, kutoka Mkoa wa Kusini Unguja, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya ukosefu wa samani katika Vituo mbalimbali vya Polisi nchini, ikiwa ni pamoja na Vituo vya Paje na Jambiani kutoka Mkoa wa Kusini Unguja na hii ni kutohakana na ufinyu wa bajeti. Aidha, Serikali imekuwa ikishirikiana na wadau werevu wa ulinzi na usalama ili kuhakikisha Vituo vya Polisi vinapata samani za kisasa ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kituo cha Paje wadau werevu wamechangia meza sita, viti kumi na nne na makabati manne. Pia katika Kituo cha Jambiani Mkoa wa Kusini Unguja wamechangia meza tatu, viti sita na mabenchi mawili na wameahidi kuchangia ama kuendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inatambua pia umuhimu wa vyombo vyaya usafiri katika kutekeleza majukumu ya Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi linatarajia kupata magari kwa ajili ya kutendea kazi na pindi yatakapofika yatatengwa kwenye maeneo yenye uhitaji wa magari na Vituo vyaya Paje na Jambiani vitazingatiwa zaidi. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jafar Sanya Jussa, swali la nyongeza.

MHE. JAFAR SANYA JUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri atafanya ziara kuvitembelea vituo hivyo vyaya Jambiani na Paje na nyumba za askari wa Jeshi la Polisi Makunduchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, ni lini Serikali italipatia Jeshi la Polisi, Wilaya ya Kusini gari kwa ajili ya doria?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sanya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Sanya. Hakika amekuwa anafanya kazi kubwa sana ya kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Paje hasa wa maeneo ya Jambiani, Paje, Bwejuu, Makunduchi, Kizimkazi, Mtende na maeneo mengine ya jirani ili kuhakikisha kwamba wanapata kwa utulivu na uhakika huduma za usalama na ulinzi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie tu ndani ya Bunge hili tumeshapanga na Mheshimiwa Sanya twende tukakabidhi mabati kwa ajili ya kuezeka Kituo cha Paje na fedha hizi zitatoka ndani ya mfuko wake. Kwa hiyo nimpongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sanya. Kwanza anauliza je, niko tayari kwenda kuangalia maeneo hayo? Nimejibu tu kwamba niko tayari na nimuahidi tu kwamba ndani ya Bunge hili la Bajeti tutapanga siku tuchupe mara moja twende tukakague, tukayaone hayo maeneo. Tukazione hizo hali na changamoto, halafu tujue namna ya kuzitafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini je, tuko tayari kutoa gari? Nimwambie tu kwamba awe na Subira, katika bajeti ijayo tutajitahidi Vituo vya Paje na Jambiani, Wilaya wa Kusini Unguja tuvizingatie zaidi katika kuhakikisha kwamba wanapata gari kwa ajili ya kufanya doria za ulinzi na usalama katika Jimbo lake. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zackaria Issay, swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya miundombinu inayoikabili Jeshi la Polisi nchini inaikabili sana Wilaya ya Mbulu. Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Mbulu kilijengwa mara baada ya uhuru, kwa sasa kina uchakavu mkubwa. Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hili la uchakavu wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Mbulu na makazi ya askari katika Wilaya yetu ya Mbulu? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu letu kama Serikali na Wizara ni kuhakikisha kwamba ulinzi na usalama wa nchi unaenea kila mahali. Hilo la kujenga vituo vya polisi na kuvipatia magari, yote ni sehemu ya jukumu na wajibu wetu. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge, awe na subira kidogo kwa sababu kasungura bado kadogo lakini kakija

kakichononoka kidogo, basi hilo ni jambo ambalo linawezekana na tukipata fedha ya kutosha, basi tutampelekea kituo cha polisi na huduma nydingine za polisi katika Jimbo lake. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 152

Utaratibu wa Kuvuna Viungo vya Binadamu

MHE. ROSE C. TWEVE aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha utaratibu maalum wa kuvuna viungo vya binadamu kama vile figo na moyo kwa ajili ya Watanzania wenye uhitaji wa viungo hivyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Benjamin Mkapa zimeanza kutoa huduma ya uvunaji na upandikizwaji wa figo nchini tangu mwezi Novemba, 2017 kutoka kwa wachangiaji walioridhia. Hadi sasa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imepandikiza figo 62 na Hospitali ya Benjamin Mkapa imepandikiza figo 18. Aidha, kwa upande wa upandikizaji wa moyo, Serikali inaendelea kujenga uwezo wa ndani wa kutoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya upandikizaji wa viungo nchini kama ambavyo Mbunge ameainisha, Serikali imeandaa Muswada wa Kutunga Sheria itakayoongoza taratibu za uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa viungo ambayo ipo kwenye hatua ya ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau. Hata hivyo, kwa kuwa huduma zimeanza kutolewa, kwa sasa nchi inatumia miongozo ya kimataifa inayosimamia uvunaji na upandikizaji wa viungo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, swalilala nyongeza.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kama alivyoainisha Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa upande wa figo, kama Taifa tumepiga hatua kubwasana pia kwa kutumia wataalam wetu wa ndani.

Hata hivyo, utakubaliana nami kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa sana la magonjwa yasiyoambukizwa ikiwemo kisukari, moyo na figo. Sasa swalilangu la kwanza, kwa Serikali, ni lini mchakato huu wa kuandaa huu Muswada utakamilika kama alivyoonesha sasa hivi tunatumia utaratibu wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini sasa Muswada huu utaletwa hapa Bungeni ili kutupa nafasi sisi ambao tuko tayari kuchangia viungo vyetu kama vile figo tuweze kufanya hivyo? Sheria hii itaruhusu sasa wale wenzetu ambao wanafikia mwisho wa maisha yao wataweza kuchangia viungo vyao kama vile figo na moyo ili kuwasaidia Watanzania wenzetu wenye uhitaji wa viungo hivyo waweze kuboresha afya zao na kuendelea kujenga Taifa letu. Nashukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo

amekuwa akifuatilia sana huduma za watu wake wa Iringa. Amekuwa akiwasiliana na sisi sana, hasa wagonjwa wake wanapokuwa Bugando, Muhimbili, KCMC na kwingine amekuwa akifuatilia kwa karibu sana. nadhani ndiko alikojifunzia kwamba, haya matatizo yanatakiwa yashughulikiwe haraka sana kwasababu, yanasumbua wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı lake ni kwamba, ni lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwasababu kama nilivyosema kwamba, tuko sasa kwenye hatua ya kukusanya maoni ya wadau. Kwa hiyo, kwenye Bunge la mwezi wa tisa tutaleta muswada kwa ajili ya kufanya hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niliombe Bunge lako Tukufu kwamba, suala sio kwamba tu sisi kuja na sheria ya kuweza kuruhusu upandikizaji na kuvuna viungo. Suala ni kwamba, ni kwa nini imeongezeka tatizo la watu kuharibika figo na matatizo ya moyo, hilo ndio swalı kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Wabunge wenzangu kwa sababu sauti zao zinafika mbali na zinaheshimiwa na wananchi zile za taratibu za kuzuia matatizo ya figo, za kuzuia kupata magonjwa ya moyo. Tutakapokuja Wizara na mkakati na mtaona wakati wa *corona* tulikuwa na mkakati mzuri ambao mmetusaidia endeleeni kutuunga mkono ili kuzuia watu wasipate haya matatizo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ng'azi Ulenge*, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake.

Na. 153

Huduma ya Afya kwa Mama na Mtoto – Tanga

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE aliuliza:-

Mwaka 2018 *KFW Germany* walisitisha udhamini kwa huduma za Afya kwa Mama na Mtoto Mkoani Tanga.

(a) Je, ni juhudhi gani zimefanyika kuhakikisha Mdhaminini huyo anaendelea na udhamini wake Mkoani Tanga?

(b) Je, Serikali ina mpango gani kupata Mdhaminini mwingine?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge*, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kuititia Benki ya *KFW* ilianzisha mpango wa Bima ya Afya kwa akinamama wajawazito na watoto. Mpango huo ulitekelezwa kwa makubaliano ya kipindi maalum toka 2012 hadi 2018. Mpango huo umechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza uelewa wa dhana na umuhimu wa kuwa na Bima ya Afya katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inakamilisha Rasimu ya Muswada wa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambao utawasilishwa Bungeni mwezi Juni 2021, swali la Mheshimiwa Mbunge lenye kipengele (a) na (b) litaenda kupata suluhisho. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuwahamasisha wadau mbalimbali katika kuchangia miradi ya Sekta ya Afya, ikiwemo Bima ya Afya kwa Wote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ng'anzi Ulenge*, swali la nyongeza.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *KFW Germany* wamekuwa wakitoa huduma hiyo tangu mwaka 2013 mpaka 2018 mwishoni Mkoani Tanga, lakini 2019 mwanzoni ndipo walisitisha huduma zile na kuweza kupeleka mikoa mingine. Naomba kujua sababu gani imesababisha *KFW Germany* kuacha kutoa huduma ile ya mama na mtoto Mkoani Tanga na kuhamishia sehemu nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Mwaka 2017 Serikali kwa mara ya kwanza ilianzisha upasuaji kwa watoto wenyewe upungufu wa usikivu nchini Tanzania, yaani wanafanyiwa upasuaji na wanapata mashine ambayo ni *cochlear implant surgery machine*, lakini *accessories* ama *spare parts* za mashine hizo zimekuwa ni ghali sana kwa wananchi wa kawaida kuweza kuzi-afford. Betri moja la mashine ile ambayo ni *rechargeable* ni zaidi ya laki tano, lakini ukienda kwenye...

NAIBU SPIKA: Swali Mheshimiwa.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, Serikali sasa ione haja ya kuvigiza vifaa hivyo nchini na wananchi waweze kununua kuititia Serikali, ili kuweza kushusha bei ya ununuzi kwasababu India ni rahisi sana. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, umeshauliza swali. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ni kwamba, kwa nini, sababu iliyofanya ule mkataba ukavunjika

wa elfu mbili maana mkataba ule ulikuwa ni wa kipindi maalum 2012 ambao umeanza kama anavyosema 2013 na mpaka 2018, lakini nafikiri anauliza sababu iliyofanya:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kwanza ambayo sisi tunajua ilikuwa ni mkataba wa wakati maalum, lakini nimuombe Mheshimiwa Mbunge tutafuatilia vizuri zaidi kwasababu inawezekana kulikuwa na uwezekano wa kuongeza mkataba na ukawea kusitishwa. Tutaenda kufuatilia pamoja na yeche ili tuje na nitampa taarifa kwamba, ni nini kama kuna uwezekano wa kufanya lolote tuweze kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kufuatia hilo najua amekuwa akipata shida sana na umekuwa ukija wizarani kwa ajili ya akinamama wa Mkoa wa Tanga kuchajiwa hela. Mimi na wewe tutatafuta muda tuende tukaangalle tatizo ilko wapi tulishughulikie haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swalilake la pili lilikuwa ni suala la upandikizaji wa viungo, watu wenye shida ya usikivu, upandikizaji ili waweze kusikia:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikwambie kwamba, Serikali yetu ukweli watu walikuwa wanapelekwa nchi za nje kwenda kuweza kupandikizwa hivyo viungo na walikuwa wanatumia zaidi ya milioni 100 kwa mtu mmoja. Lakini sasa Tanzania vimeshanunuliwa vifaa na upandikizaji huo umeanza kwenye hospitali yetu ya Muhimbili na ndicho anachozungumzia Mheshimiwa ambayo bado ni changamoto kwasababu, kununua tu vifaa vyenyewe ni zaidi ya milioni 40 ili kuweza kumpandikiza mtu huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaenda vilevile kuja na Muswada wa kupanga gherama za vifaa tiba na dawa hatuna muongozo wa kudhibiti bei za vifaa hivyo, mtu anajiamulia tu kuuza bei anayoitaka. Lakini kwasababu Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan alitoa bilioni 80 juzi kwa ajili ya kununua vifaa tiba tutaenda kuzingatia

kwenye eneo hilo tuhakikishe Muhimbili wana vifaa hivyo kupitia *MSD*.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 154

Ujenzi wa Barabara ya Tingi – Kipatimu

MHE. FRANCIS K. NDULANE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Tingi – Kipatimu yenye urefu wa kilometra 50 kwa kiwango cha lami hasa ikizingatiwa kuwa barabara hiyo inapita katika maeneo yenye kumbukumbu za Vita vya Majimaji na vivutio muhimu vya Utalii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *Eng. Msongwe*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) aliujibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa barabara ya Tingi – Kipatimu yenye urefu wa kilometra 50 kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, mkakati wa Serikali kwa sasa ni kuunganisha makao makuu ya mikoa kwa barabara za lami zilizoainishwa kwenye shoroba za maendeleo (*development corridor*). Serikali itakapokamilisha mpango huu barabara nyengine za mikoa zitafuata ikiwemo barabara ya Tingi – Kipatimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na matengenezo ya kawaida na matengenezo ya muda maalum ili kuifanya barabara hii kupitika majira yote ya mwaka ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi milioni 496.569 zimetengwa kwa ajili ya kuifanya matengenezo barabara hii. Aidha, Serikali imepanga kuimarisha baadhi ya sehemu korofi kwa kuziwekea lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Kwa sasa Barabara ya Tingi – Kipatimu ina maeneo mengi ambayo hayapitiki na mengine yanapitika kwa shida sambamba na Barabara ya Nangurukuru – Liwale.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuweza kurekebisha barabara hizo mbili ili ziweze kutengenezwa na hatimaye wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, barabara hizi mbili za Nangurukuru – Liwale kilometra 258 na hiyo ya Tingi – Kipatimu katika miaka ya karibuni zilipanuliwa upana wake, lile eneo la hifadhi ya barabara kutoka mita 30 hadi kufikia mita 45. Na hii Hali ilisababisha wananchi kuweza kuvunjiwa nyumba zao na kuondolewa mazao yao. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa wananchi ambao hawajalipwa hadi sasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa *Engineer Msongwe*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Tingi – Kipatimu ina vilima, na katika swali lake la msingi

nimejibu kwamba, tayari *TANROADS* Mkoa wa Lindi umeainisha maeneo yote korofi ambayo yana vilima na yatawekewa lami. Na hivi tunavyoongea mwaka huu itawekwa walao mita 500 na mwaka wa fedha kama bajeti itapita pia, maeneo yameainishwa ambayo tunategemea kuongeza kiwango cha lami maeneo ambayo barabara inakuwa ina milima na inateleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Barabara ya Nangurukuru – Liwale, yako maeneo ambayo inapita kwenye bonde na maji huwa yanajaa. Na tunategemea kwenye bajeti ya mwaka huu tunayoiendea kama itapitishwa litajengwa tuta kubwa ambapo maji sasa yatakuwa hayana uwezo wa kufurika na kuziba njia hiyo ya Barabara ya Nangurukuru – Liwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia, ni kweli kwamba, baada ya sheria kupitishwa barabara zetu zimetanuliwa kutoka mita 30 hadi 45, lakini 45 hadi 60. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mita hizi ambazo zimeongezeka saba na nusu, sab ana nusu kwa upande, pale ambapo ujenzi utanza basi wananchi hawa ambao watakuwa ni wathirika watapata fidia wakati mradi huu utakapoanza kutekelezwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Awack swalil la nyongeza.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali iliahidi kwa muda mrefu sana Barabara ya Karatu – Mbulu – Singida na mpaka sasa hamna dalili yoyote ya kujenga kwa kiwango cha lami. Je, ni lini Serikali itatenga hela kwa ajili ya Barabara ya Karatu – Mbulu – Singida?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Karatu – Mbulu – Singida ni kati ya barabara ambazo zimeainishwa kwenye ilani na ambazo zinategemea kujengwa kwa kiwango cha lami katika kipindi hiki cha miaka mitano. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Karatu na wananchi wa Karatu na wote watakaonufaika na barabara hizi kwamba, kadiri Serikali itakavyopata hela na katika kipindi hiki cha miaka mitano barabara hizi zitajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inaendelea kukamilisha ahadi za viongozi waliotangulia. Mheshimiwa wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Jakaya Kikwete alitembelea Wilaya ya Nyan'ghwale na kuahidi ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kahama – Nyan'ghwale kwenda Sengerema, lakin mwaka 2015 Hayati Dkt. John Pombe Magufuli naye aliahidi hivyo hivyo kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Swali, ni lini Serikali itatenga fedha za upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo la lami?

NAIBU SPIKA: mheshimkiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer Msongwe*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye majibu mengine, Barabara ya Kahama – Nyn'ghwale – Sengerema pale Busisi ni barabara ambazo zimeahidiwa na viongozi wetu na ni barabara muhimu sana kwa kuunganisha maeneo haya. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Nyan'ghwale kwamba, barabara hii itafanyiwa upembuzi yakinifu mara bajeti tunayoiendea itakapokuwa imepitishwa. Kwa hiyo, baada ya kufanya hivyo taratibu nyingine kwa maana ya

usanifu wa kina utafanyika, ikiwa ni hatua za awali kuelekea ujenzi wa lami wenyewe. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 155

Daraja la Kuunganisha Kata ya Ilagala na Kata ya Sunuka – Uvinza

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja kwenye Mto Malagarasi ili kuunganisha Kata ya Ilagala na Kata ya Sunuka katika Wilaya ya Uvinza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine, Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Malagarasi (*Lower Malagarasi Bridge*) linaunganisha Kata ya Ilagala na Kata ya Sunuka katika Wilaya ya Uvinza kupitia Barabara ya Simbo – Ilagala hadi Kalya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa daraja hili katika bajeti ya mwaka huu wa 2020/2021, Wizara yangu imetenga shilingi milioni 345 kwa ajili ya kufanya kazi ya Upembizi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Daraja hili la Malagarasi. Aidha, katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2021/2022 daraja hili limetengewa

shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuendelea na kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina. Kwa sasa taratibu za ununuzi wa Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hiyo zinaendelea. Baada ya kazi hiyo kukamilika, ujenzi wa daraja hili utaanza kadiri ya upatikanaji wa fedha utakavyokuwa. Asante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa usanifu ulikamilika na kuwa usanifu unaofanyika ni uhuishaji wa usanifu wa awali. Je, Serikali haioni haja kutenga fedha mwaka ujao wa fedha ili kujenga daraja hilo 2021/2022 ili kunusuru maisha ya wanawake na watoto wanaopoteza maisha kwasababu ya kutokuwa na kivuko hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa, kivuko kinaanca kazi saa 01:00 asubuhi na kuishia saa 01:00 jioni. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza saa ili kivuko hicho kifiki saa 06:00 usiku kuweza kuwanusuru wananchi wanaopoteza maisha kutokana na saa hizo kuwa fupi?

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jibu langu la msingi nimeeleza kwamba, tumetenga, kama bajeti itapitishwa kama ilivyoombwa, tumetenga milioni 400 kukamilisha usanifu wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimueleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, daraja hili ni katika madaraja makubwa yatakayojengwa Tanzania, Mto Malagarasi ni katika ya mito mikubwa katika Tanzania hivyo, tutakapokamilisha usanifu wa kina ndio ujenzi utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kivuko kinafanya kazi kuanzia saa 01.00 hadi saa 01.00 jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungananae, na kwasababu ya changamoto ya Mto Malagarasi ambaa ni mto mkubwa una zaidi ya kilometa 300 na unapita kwenye misitu mikubwa ambayo inabeba magogo na miti, lakini pia kuna wakati unafurika na mpaka zile sehemu zake za ku-park vile viuvuko huwa hazipo ndio maana Serikali imeona isifanye kazi usiku kwasababu, inaweza ikapeleka kivuko ziwani na hata kukipindua hicho kivuko kwa sababu ya hayo magogo na miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa anafahamu kwamba tumeweka utaratibu pale ambapo kuna dharura, watu hao wapo na wamekuwa wanafanya kazi. Hata hivyo, illi kuondokana na changamoto hiyo kabisa ndiyo maana Serikali sasa imekuja na mpango wa kujenga daraja, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona kwa ajili ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kivuko hiki cha Mto Malagarasi ni muhimu kama ilivyo barabara ya kutoka Kilosa – Magomeni – Masanze -Zombo – Ulaya - Muhenda – Mikumi. Pia barabara hii ilikuwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2015-2020 na ipo kwenye llani 2020-2025 na ipo kwenye bajeti...

NAIBU SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, je ni lini ujenzi wa barabara hii unaenda kuanza? Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja imeainishwa kwenye llani lakini pia ipo kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dennis Londo kwamba kuanzia bajeti hii tutakayoianza barabara hii itaanza kufanyiwa kazi kwenye mipango yetu kwani viongozi wengi wameahidi barabara hiyo ijengwe. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi yeye na wananchi wa Mikumi kwamba barabara hii ipo kwenye mpango na itatekelezwa katika kipindi hiki cha miaka mitano.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumalizie na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, sasa aulize swali lake.

Na. 156

Kufufua Zao la Kahawa Nchini

MHE. JAPHET N. HASUNGA aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua zao la Kahawa nchini ambalo ni moja ya mazao ya kimkakati?

(b) Je, ni lini Makampuni binafsi yataruhusiwa kununua Kahawa kwa Wakulima moja kwa moja bila kupitia Vyama vya Ushirika?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inaendelea kutekeleza Mkakati wa Miaka Kumi wa Maendeleo ya Zao la Kahawa wenyе lengo la kuongeza tija na ubora wa kahawa nchini. Utekelezaji wa mkakati huo umewezesha kuongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 43,872 za kahawa za msimu wa mwaka 2017/2018 hadi tani 67,000 msimu wa 2020/2021. Aidha, wastani wa bei kwa wakulima wa kahawa kavu aina ya Arabika umeongezeka kutoka shilingi 3,500 kwa mwaka 2019/2020 hadi shilingi 4,000 kwa mwaka 2020/2021 na bei ya kahawa ya maganda ya Robusta imeongezeka kutoka wastani wa shilingi 1,100 kwa mwaka 2019 hadi shilingi 1,200 mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mkakati wa Wizara ni kuhakikisha kwamba tunaongeza tija; uwekezaji mkubwa katika Taasisi yetu ya Utafiti ya *TaCRI*; mfumo wa masoko; kuboresha mfumo wa ushirika, uzalishaji na ugawaji wa miche. Mpaka sasa Wizara imeshaanza mradi wa uzalishaji wa miche milioni 5.5 kwa ajili ya kuendelea kugawa bure kwa wakulima wa kahawa nchini. Vilevile Serikali imeipatia Taasisi ya *TaCRI* jumla ya shilingi milioni 300 katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuhusu mfumo wa wanunuzi wa kahawa kupitia Vyama vya Ushirika umelenga kuongeza ushindani katika soko la awali kulingana na ubora wa kahawa na pia kuwawezesha wakulima kuwa na nguvu ya pamoja ya kushauriana ili kupata bei nzuri na kunufaika na kilimo, hivyo kuondokana na walanguzi ambao wamekuwa wakiwalaghai baadhi ya wakulima. Hivyo, kampuni binafsi na wenyе viwanda vya kahawa wanaruhusiwa kununua kahawa kutoka kwa wakulima kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi na Vyama Vikuu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, swalı la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, natoa shukrani kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika, ushirika ni kwa wana ushirika wenyewe lakini sasa hivi hali ilivyo ushirika umekuwa ukiwalazimisha watu ambao sio wanachama kwenda kuuza mazao yao kupitia kwenye Vyama vyta Ushirika. Serikali ina mpango gani wa kuwaruhusu kampuni binafsi na wafanyabiashara kwenda kununua moja kwa moja kwa wakulima siyo kupitia kwenye ushirika? Hilo ni swali la kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa sasa hivi hili ni moja ya mazao ya kimkakati na limekuwa likishuka uzalishaji; kwa mfano takwimu za Mkoa wa Songwe limeshuka, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba wanawakopesha wakulima fedha ili waweze kununua pembejeo kama mbolea na dawa na *CPU* ili kusudi waweze kuongeza uzalishaji na ubora wa kahawa hapa nchini? (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hasunga, mwalimu wangu kama ifuatavyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini haturuhusu wafanyabiashara kwenda kwa mkulima mmoja mmoja na Mheshimiwa Mbunge na ye ye anafahamu, utafiti na *experience* imeonyesha kwamba mfumo wa kuwaruhusu wafanyabiashara kwenda kwa mkulima mmoja mmoja hasa wa zao la kahawa umepelekea wakulima wengi hasa kwa upande wa Kagera kupata bei ndogo kwani walikuwa wanauza kahawa yao katika mfumo ambao sio halali kwa shilingi 500 au shilingi 700, mpaka wengine kukopeshwa na mashamba yao kunyang'anywa. Kwa hiyo, mfumo wa ushirika umesaidia kumfanya mkulima wa kahawa kuwa na *bargaining power*.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto katika ushirika ambazo hata Mheshimiwa Mbunge anazifahamu na

ambazo zinapelekea mapendekezo ya kufanya mabadiliko ya sheria ambapo tunachukua hatua. Mpaka sasa tunaamini kwamba mfumo wa ushirika ndio njia sahihi ambayo itamsaidia mkulima mdogo mdogo kuwa na *collective bargaining power* ambayo itamsaidia kuweza kupata haki yake. Kwa nini wasikopeshwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawagawia miche bure, lakini ili wakopeshwe lazima wawe na *vehicles*. Wakulima wa pamba ni mashahidi mfumo wa ushirika ndio njia pekee itakayowafanya wakulima waweze kukopeshwa. Tumefanya majaribio, tumeona kwenye zao la pamba mwaka huu wakulima wa pamba wamekopeshwa kuitia ushirika zaidi ya shilingi bilioni 37, wamepatiwa *input* bila *collateral*/yoyote. Kwa hiyo, kama zipo changamoto *specific* kwa eneo moja tujadiliane tuweze kuzitatua lakini *ku-abandon* mfumo ambao umetusaidia kuwapatia wakulima bei nzuri. Tunaamini kwamba wafanyabiashara wanaweza kununua kahawa katika Vyama vya Msingi kwa makubaliano yanayoonesha bei na *volume* bila kuwaruhusu kwenda kwa mnunuzi mmoja mmoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swalii la mwisho, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 157

Uzalishaji wa Zao la Vanila Nchini

MHE. MARYAM AZAN MWINYI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha uzalishaji wa zao la Vanila nchini.?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la vanila hulimwa kwa wingi katika Mikoa ya Kagera, Morogoro, Tanga, Mbeya, Arusha na Kilimanjaro ambapo uzalishaji umekuwa ukiongezeka kutoka tani 229 mwaka 2015 hadi kufikia tani 1,949 mwaka 2020. Katika kuhamasisha uzalishaji wa zao la hilo, Wizara ya kilimo imefanya tathmini ya kutambua wadau na masoko ya vanila ndani na nje ya nchi na kuzifahamu changamoto zinazokabili zao hilo ikiwemo upatikanaji wa mbegu bora. Wadau wakubwa wa vanila ni pamoja na Shirika la Msalaba Mwekundu Umoja wa Wazalishaji wa Viungo (*Tanzania Spice Producer Association*), Chama cha Wakulima wa Viungo vya Amani, Chama cha Maendeleo ya Wakulima (MAYAWA), Taassis ya Kilimo Endelevu SAT, Ushirika wa Wazalishaji Viungo wa Mtamba lakini Kiwanda cha *Natural Extract Limited* kilichopo Mkoani Kilimanjaro na Chama cha Wazalishaji wa Vanila Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali itaongeza upatikanaji wa miche bora ya vanila nchini kwa kuhamasisha wazalishaji wa ndani na kuandaa utaratibu wa kuingiza miche bora kutoka nje ya nchi. Pia Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuhamasisha uendelezaji wa zao la vanila na mazao mengine ya viungo kwa kutoa mbinu bora za kilimo cha vanila ili kujadili maendeleo ya tasnia ya viungo. Hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya wakulima 1,387 wa zao la vanila wamepatiwa mafunzo ya kanuni na mbinu bora za uzalishaji. Aidha, katika kuimarisha huduma za ugani kwa zao hilo, Maafisa Ugani 20 wamepatiwa mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Utafiti cha TARI – Tengeru kinafanya utafiti wa mazao ya bustani likiwemo zao la vanila na viungo. Kituo hicho kimeanza ukusanyaji wa vinasaba vya mazao likiwemo zao la vanila kwa ajili ya kufanya utafiti wa aina bora za vanila ili kuboresha uzalishaji. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha *International Trade Centre* imeandaa mfumo maalum wa

kutambulisha mazao ya viungo yanayozalishwa Tanzania katika masoko ya nje. Vilevile, Serikali itaendelea kusimamia mikakati yote inayolenga kuongeza uzalishaji tija na kuboresha mazigira ya biashara ya zao la vanila na mazao ya viungo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa vile wanawake ndiyo wanaoshughulika sana katika kilimo hiki cha vanila lakini mitaji, elimu na ujuzi wao pia ni mdogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuviwezesha vikundi hivi vya akina mama?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, Serikali imefanya tathmini gani ya bei hapa nchini kwetu na nchi za nje? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali ina mkakati gani kuwapatia uwezo wa kifedha vikundi vya akina mama ama wajasiriamali waliopo kwenye zao la vanila na mazao mengine ya kilimo. Kwanza, nitumie nafasi hii kuhamasisha Halmashauri zote za Wilaya ambazo zao la vanila na mazao mengine ya kilimo yanapatikana, ni vizuri asilimia 10 ya kukopesha akina mama na vijana ikaelekezwa kwenye maeneo ya uzalishaji ili kuweza kusaidia mitaji yenye gharama nafuu kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tutaendelea kuwasiliana na Serikali za Mitaa ili waweze kutusaidia katika hilo na tumepeleka mapendekezo Wizara ya Fedha namna ya kutumia cess inayopatikana kwenye mazao iweze kurudi

kwenye uzalishaji badala ya kufikiria kukopesha bodaboda na vitu vya namna hiyo. Hatua ya pili kuhusu *financing*, Waziri wa Kilimo hivi karibuni ameunda *committee* ya kuangalia namna gani tunaweza tukapata mitaji katika sekta ya kilimo ambayo inaendana na sekta ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kipengele cha pili, Taasisi yetu ya Tengeru inaendelea kufanya utafiti ambao utatoa majibu halisi ya bei. Naomba nitumie Bunge hili kusema kwamba maeneo kama ya Mbeya ambapo kuna watu wanapita kuwapotosha wakulima kuwaambia kwamba kilo moja ya vanila ni zaidi ya Sh. 150,000 – Sh. 200,000 sasa hivi katika soko, sio kweli, bei iliyopo sasa hivi haizidi Sh. 20,000 – Sh. 25,000. Kwa hiyo, wasiwapotoshe wakulima kwa kuwapa matumaini ambayo siyo sahihi. Wizara ya Killimo sasa hivi tunafanya tathmini na tutatoa taarifa kwa umma kuwaonesha masoko na bei halali za mazao hayo katika masoko ya nje na masoko ya ndani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kabula Shitobelo, swali la nyongeza.

MHE. KABULA E. SHITOBELO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali langu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na hali ya hewa au tabia nchi kwa mwaka huu Kenya haikuzalisha vizuri zao la parachichi, hivyo, wafanyakishara wengi walikuja Tanzania kwa ajili ya kununua zao hili. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha wakulima kuongeza kilimo hiki? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuwahamasisha wakulima wa parachichi sio dhambi

kumuuzia Mkenya kwa sababu ni *export* ambayo tunakwenda kuuza ingawa lengo letu ni kwenda kwenye *final markets*. Kwa hiyo, tunaendelea kuwahamasisha wauze.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili tunachukua hatua gani kuongeza uzalishaji? Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maagizo kwa Halmashauri zote ambazo mazao ya parachichi yanalinwa kutenga maeneo angalau ya ekari 10 kwa ajili ya kuzalisha miche na kuigawa kwa wakulima. Wizara ya Kilimo imeshaanza kazi hiyo kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, hii ni hatua ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili ni kuwatambua wakulima na kuwa *register* ili mazao yao wanayozalisha yaweze ku-*meet international standard* na hii *project* tunafanya pamoja na wenzetu wa *FAO* ili ku-*identify pest*. Hatua ya tatu tunafungua masoko. Sasa hivi tunamalizia kufungua soko la South Africa lakini tumeanza *negotiation* na wenzetu wa China ili tuweze kufungua soko la China na ita-*pull* yenyewe uzalishaji na wakulima watakwenda sokoni wakiwa na soko la uhakika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka Serikalini. Nilita matangazo tuliyonayo asubuhi hii, tutaanza na tangazo la wageni waliopo Bungeni.

Tunao wageni wangu sita ambao ni wasanii wa muziki wa asili wanaitwa Wamwiduka Band, hawa wanatoka Jijini Mbeya lakini wanaishi Dar es Salaam. Ahsanteni sana na karibuni sana vijana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, vijana hawa wanaimba vizuri sana, mkienda *YouTube* mtapata habari zao maana kuna watu wanachuma shilingi 1,000 wanahonga Sh. 700 wanakula shilingi 300. Hawa watoto ndiyo walioimba huo wimbo jamani, kwa hiyo wapo vizuri, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa

Katiba na Sheria ambaao ni Wakuu wa Taasisi pamoja na viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Profesa Sifuni Ernest Mchome. Karibuni sana na mimi nimefurahi kuwaona hapo, wengine walimu wangu na wengine wanafunzi wangu basi mambo yanakwenda vizuri. (*Makofi*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Kabudi ni Madiwani wa Kata na Madiwani wa Viti Maalum kutoka Wilaya ya Kilosa wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Tindiga Mheshimiwa Yahaya Mbaruku Mbanchi. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii na hawa ni jamaa zake kutoka Songea. Karibuni sana, hapa wamesema jamaa zake naamini na kura mlimpigia kwa hiyo wanaitwa wapiga kura pia. (*Makofi*)

Wapo pia wageni 28 wa Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wa Madini ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Jimbo la Bukombe. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambaao ni wafanyabiashara katika Sekta ya Madini kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Rehema Mtatifikolo. Naona hawakupata fursa ya kuingia humu ndani.

Wapo pia wageni 28 wa Mheshimiwa *Engineer* Andrea Mathew Kundo, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambaao ni wanafunzi wa vyuo vikuu vilivyoko jijini Dodoma wanaotokea Jimbo la Bariadi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia wapo wageni 11 wa Mheshimiwa Charles Mwijage pamoja na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo ambaao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi na Serikali kutoka Jimbo la Muleba wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muleba

Ndugu Athuman Kahara. Nafikiri na wao hawajapata fursa ya kuingia Bungeni asubuhi hii.

Wapo wageni 27 wa Mheshimiwa Dennis Londo ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Kilosa wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ambaye ni Ndugu Ameir Mbarak Ahmed, karibuni sana. (*Makof*)

Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Abdul-Hafar Juma ambaye ni mke wake, Ndugu Fatma Karume Said na huyo ameongozana na ndugu yake ambaye ni Hamida Mohamed kutoka Zanzibar. Naona na wao hawajapata fursa ya kuingia hii asubuhi. (*Makof*)

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Nusrat Hanje ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dodoma na huyu ni Ndugu Fatuma Chomoka, karibu sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 28 wa Mheshimiwa Bashungwa ambaye yeye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni wachezaji na viongozi wa *Nyaishozi Sports Club* ya Wilaya ya Karagwe wakiongozwa na Ndugu Paul Mbiliqi na Majaliwa Said, karibuni sana vijana wa *Nyaishozi Sports Club*. Naambiwa hawa mmefuzu kuingia ligi daraja la pili baada ya kushika nafasi ya tatu kwa washindi wa mikoa. Karibuni sana. (*Makof*)

Wapo pia wageni sita wa Mheshimiwa Kenneth Nollo ambao ni jamaa zake kutoka Bahi wakiongozwa na Ndugu Jonathan Chibalungu, karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Jerry Silaa ambao ni wafanyakazi wa *Sanlam Assurance* kutoka Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Nura Masoud, Ndugu Cosmas Muhamuzi na Ndugu Felix Manyungu, karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, hawa niliowatangaza mwisho ambao ni wafanyakazi wa *Sanlam Assurance*, wanalo banda lao sehemu ya ukumbi wa Msekwa. Ni muhimu

kwenda kuwatemebelea ili tuelewe kuhusu bima na hasa ukizingatia sisi wenyewe tunataka kuweka bima kwa ajili ya mambo yetu mengi. Kwa hiyo, ni vizuri kwenda pale ili tuelewe wanafanya shughuli gani na kama sisi tunaweza kuwa sehemu ya watu ambao tunataka kujiunga nao.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo pia tangazo la Mwenyekiti wa Jumuiya ya *Saint Thomas More* hapa Bungeni, Mheshimiwa Shally Josepher Raymond anawatangalzia Waheshimiwa Wabunge wote, wageni na watumishi wa Bunge pia kwamba kutakuwa na Ibada ya Misa Takatifu itakayoanza saa 7.00 mchana katika Kanisa la Bunge, yaani Bunge *Chape/mara* tu baada ya kusitisha shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo tuliyonayo siku ya leo, tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

NAIBU SPIKA: Nimuite Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi awasilishe hoja yake. (*Makofii*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yote ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria iingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa wingi wa rehema zake na kuniruzuku uhai na afya njema iliyoniwezesha kusimama hapa leo katika Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita kwa kuniamini na kunateua kuitumikia Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika nafasi ya Waziri wa Katiba na Sheria. Naahidi kuitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na unyenyekevu kwa maslahi mapana ya Taifa. Namwomba Mwenyezi Mungu anijalie hekima, ujasiri na busara ili niweze kutimiza wajibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba mnamo tarehe 17 Machi, 2021 Taifa letu lilipatwa na msiba mkubwa sana kwa kuondokewa na kiongozi, jemedari na shujaa wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na tulimpumzisha tarehe 26 Machi, 2021. Taifa limepatwa na masikitiko na majonzi makubwa kwa kumpoteza shujaa huyu wa mfano kwa Afrika na dunia nzima. Mwenyezi Mungu aipokee roho yake na kumpa pumziko la amani mpendwa wetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha, 2020/2021, Taifa pia lilipatwa na vifo vya Viongozi Waandamizi waliokuwa wakilitumikia Taifa katika nyadhifa mbalimbali. Viongozi hao ni pamoja na Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyeokuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar; Mheshimiwa Balozi Mhandisi John William Kijazi, aliyeokuwa Katibu Mkuu Kiongozi; Mheshimiwa Jaji (Mstaafu) Harold Reginald Nsekela aliyeokuwa Kamishna wa Maadili katika Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Mheshimiwa Bethuel Mmila aliyeokuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani; Mheshimiwa Salvatory Bongole aliyeokuwa Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Mheshimiwa Martha Umbula aliyeokuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoaa

wa Manyara; Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Muhambo; pamoja na viongozi wengine waliotumikia Taifa hili kwa nyadhifa mbalimbali. Hivyo, nitumie fursa hii kutuma salamu zangu za pole kwa Taifa kwa ujumla na ndugu waliopoteza wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuapishwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke kuliongoza Taifa letu katika Serikali ya Awamu ya Sita. Tunaendelea kumwombea kwa Mungu ampe maisha yenye siha na afya njema ili aweze kutekeleza vyema majukumu ya kuiongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge hili kwa asilimia mia moja kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Othman Masoud Othman Sharif kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Wabunge wote walioshinda uchaguzi kwenye majimbo yao na walioteuliwa. Hali kadhalika, nawapongeza Balozi Hussein Athman Kattanga kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhandisi Zena Ahmed Said kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa Zanzibar na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imeweka msingi wa

mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba nimpongeze Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza kwa uongozi wake mahiri wa kuiwezesha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi wakati akiwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Sillo Daniel Baran Mbunge wa Babati Vijijini, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa kuiongoza kamati hiyo ambayo ilipitisha Mpango na Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Vilevile, natoa shukrani za dhati kwa Kamati hizo kazi kubwa ya kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua na inathamini sana mchango wa Kamati hizo katika kuhakikisha Sekta ya Sheria inaendelea kuimarika na kutoa mchango stahiki katika kufanikisha mipango ya Taifa letu kwa maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Wizara inayo imani kubwa kwa Kamati hizo za Kudumu za Bunge na itaendelea kuzipatia ushirikiano unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri walioteuliwa tarehe 31 Machi, 2021 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kuziongoza Wizara mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakia kila la kheri wote walioteuliwa kushika

nafasi mbalimbali katika Utumishi wa Umma kwa utekelezaji wa majukumu yao mapya ya kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa hotuba yake aliyoitoa kwenye Bunge hili mnamo tarehe 22 Aprili, 2021. Kwa ujumla hotuba hiyo imeonyesha maono, mikakati na mwelekeo wa Taifa hili kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hiyo imeonesha ari mpya ya maendeleo ya nchi yetu na imebainisha maeneo ya kipaumbele kwa kila sekta katika kutekeleza sera, mipango na miongozo mbalimbali ya Taifa letu. Hivyo tunaahidi kuyazingatia maelekezo yote yaliyotolewa kuhusu sekta ya sheria na utoaji haki, tutayatekeleza kwa ufanisi mkubwa kama ilivyoelekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na dira ambayo ni katiba na sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa, pamoja na miongozo mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa. Dira hii inatoa mwelekeo wa kisera na kisheria katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa, hususan katika kudumisha hali ya amani, utulivu na utangamano wa Kitaifa ambazo ni nguzo muhimu za kujenga Taifa linalozingatia utawala wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, dhima ya Wizara ni kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa. Kwa ujumla, dira na dhima hizi zinaakisi Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, kwa kubainisha jinsi sekta ya sheria itakavyotoa mchango wake kufanikisha dira hiyo ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuelekea mwaka 2025, Wizara ya Katiba na Sheria imepanga na itaendelea kuweka mipango na mikakati inayojielekeza

katika kuendelea kuyafikia maono yaliyopo katika Ibara ya 1.2.3, shabaha zilizopo katika Ibara ya 3.2, msukumo uliopo katika Ibara ya 4.3 na maelekezo ya utekelezaji yaliyopo katika Ibara ya 5 ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Masuala haya yanagusa utawala wa sheria kama sehemu muhimu ya utawala bora itakayofanikisha maendeleo ya Taifa letu yanayotarajiwa ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mhimili wa Mahakama ya Tanzania; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Tume ya Utumishi wa Mahakama; Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini; Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania; Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto; Baraza la Elimu ya Sheria, Bodi ya Taifa ya Msaada wa Kisheria na Masijala za Masuala ya Utajiri na Maliasili za Nchi Pamoja na Upatanishi, Majadiliano, Maridhiano na Usuluhihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake ambayo ni pamoja na kutunga sera za masuala ya kikatiba na kisheria na kuhakikisha utekelezaji wake; masuala ya kikatiba; haki na mfumo wa utoaji haki; uandishi wa sheria; uendeshaji wa mashtaka ya jinai; uendeshaji wa mashauri ya madai yanayohusu Serikali; uhakiki wa mikataba mbalimbali inayohusu Serikali; masuala ya Sheria za Kimataifa; masuala ya haki za binadamu, ikiwemo haki za watu; huduma ya msaada wa kisheria; urekebu wa sheria; masuala ya usafirishaji wa wahalifu kuletwa nchini au kwenda nje ya nchi; masuala ya ushirikiano wa kisheria na Mataifa mengine katika masuala mbalimbali ya jinai; usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka, ufilisi, udhamini na kuasili watoto; uangalizi na ufuatiliaji wa utajiri na maliasilia za nchi; utendaji na uendelezaji wa rasilimaliwatu katika Wizara; na Shughuli za Taasisi, mipango na miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara na Taasisi zake ilibainisha masuala mahsusii

ya kipaumbele kuwa msingi wa kutekeleza majukumu yake. Masuala hayo yameainishwa katika ukurasa wa sita wa kitabu cha hotuba yangu. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali kuititia Wizara ya Katiba na Sheria imekamilisha maandalizi ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1/2021, ambayo pamoja na mambo mengine, imeruhusu rasmilugha aushi ya Kiswahili kuwa lugha ya uandishi wa sheria, uendeshaji wa shughuli za Mahakama, Mabaraza na vyombo vingine vyenye jukumu la kutoa haki hapa nchini. Lengo la kutafsiri sheria hizo ni kutekeleza matakwa ya Kimataifa yanayozitaka nchi kutumia lugha inayoleweka kwa wananchi ili kuweza kuwafikia na kuwawezesha kupata haki zao kwa urahisi na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 ya mwaka 2021 kuitishwa na Bunge, Wizara ilianza kuratibu zoezi la kutafsiri sheria zote za nchi kutoka lugha Kiingereza kuwa lugha ya Kiswahili ili kutekeleza matakwa ya sheria hiyo. Wizara ilichukua hatua mbalimbali ambazo ni pamoja na kutoa mwongozo na utaratibu wa zoezi la kutafsiri sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, iliagiza kuwa kila Wizara, mamlaka na Taasisi za Umma zitafsiri sheria inayozisimamia na kuandaa Rasimu ya Kwanza ya tafsiri ya sheria zake. Katika kusimamia maagizo hayo, Wizara iliandaa Mpango Kazi wa kutafsiri sheria hizo na kuwasilisha kwenye kila Wizara, Mhimili wa Bunge na katika Mhimili wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeshatoa Mwongozo kwa Wizara zote kuanza na kukamilisha tafsiri za Sheria Kuu zipatazo 449 pamoja na sheria ndogo ndogo zipatazo 39,000 zinazosimamiwa na Wizara husika au Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Hadi Machi, 2021 jumla ya Sheria Kuu zilizotafsiriwa ni 157 na Sheria Ndogo zaidi ya 15,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mwongozo huo unaelekeza kuandaliwa kwa Kamusi ya Istilahi za Kisheria. Inatarajjiwa kwamba zoezi la kutafsiri Sheria Kuu na Kamusi litakamilika Desemba, 2021 na kuendelea na maandalizi ya kutafsiri Kanuni za Sheria mbalimbali zoezi linalotarajjiwa kukamilika Juni, 2022. Wizara inawataka wadau wanaohusika na zoezi la kutafsiri sheria kuzingatia mwongozo huo ili kuweza kukamilisha jukumu hilo katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kila Wizara au taasisi wanaohusika katika zoezi la kutafsiri Sheria kuwashirikisha ipasavyo wataalamu wa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) na Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili (TATAKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenye zoezi hilo kwa kuwa ndiyo Taasisi zenyenye utaalamu wa Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu Kiswahili cha sheria ni tofauti kidogo na Kiswahili cha kawaida, kama ilivyo kwa lugha ya Kiingereza. Ushirikiano na taasisi hizi na nyingine zenyenye ulewa wa masuala haya, ikiwa ni pamoja na kutoka upande wa pili wa Muungano, yaani Tanzania Zanzibar, utatusaidia kujenga ulewa wetu zaidi katika tasnia ya sheria katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 baadhi ya Wizara na taasisi pamoja na Mihimili ya Bunge na Mahakama zimeanza kazi ya kutafsiri sheria na kanuni zake kwa kuishirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Tasisisi zake ilibainisha sheria 50 ambazo inazisimamia ili kuzitafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza zoezi hilo, Wizara na taasisi zake iligawa sheria hizo ili zitafsiriwe kisekta kwa kuzingatia taasisi na sheria inayoitekeleza. Katika mgawanyo huo, Wizara (Makao Makuu) iliunda timu ya kutafsiri sheria 17 ilizopangiwa na kukamilisha zoezi hilo tarehe 22 Machi, 2021 na hatimaye kupata rasimu ya kwanza ya sheria zilizotafsiriwa. Timu hiyo iliundwa na wataalam wa Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa

Serikali, Tume ya Kurekebisha Sheria, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania na Chama cha Wanasheria Tanganyika. Taasisi nyingine ndani ya Wizara ziko katika hatua ya mwisho kukamilisha tafsiri ya sheria kuu nyingine 33 zilizosalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara nyingine zote pamoja na taasisi zinaendelea na zoezi la kutafsiri sheria zinazosimamiwa na Wizara na taasisi hizo kwa kuzingatia Mpango Kazi ulioandaliwa ili ifikapo Desemba, 2021 sheria zote ziwe zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Hadi kufikia Machi, 2021 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeweza kutafsiri jumla ya Sheria Kuu sita pamoja na kanuni tisa za sheria hizo. Sheria hizi zimewasilishwa Wizarani ili hatimaye ziwasilishwe kwenye Kikosi Kazi cha Taifa cha kuhariri Rasimu ya Kwanza ya Sheria zilizotafsiriwa na sekta zinazosimamia na kutumia sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mhimili wa Mahakama, uko katika hatua za mwisho kukamilisha zoezi hilo la kutafsiri kanuni zaidi ya 50 zilizotayarishwa na Jaji Mkuu. Aidha, Mhimili wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tayari umetafsiri sheria unazosimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza wote ambao wameifanya kazi hii kwa ufasaha na kupata mafanikio niliyoyaeleza. Asanteni sana kwa kazi nzuri na inayotia moyo. Kwa wale ambao bado kuanza au kukamilisha hatua za kuanza kutafsiri, nichukue pia fursa hii kuwakumbusha kuanza kazi hiyo mara moja ili sote tuendane na mpango kazi wetu na hatimaye kuimaliza kazi hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haki na mfumo wa utoaji haki; katika kuimarisha mifumo ya haki jinai nchini, Wizara kuititia mradi wa Programu Endelevu ya Kuzuia Rushwa Nchini, ilikamilisha andiko la mapendekezo ya Programu ya Maboresho ya Haki Jinai na Mpango kazi wa utekelezaji. Maboresho hayo yanalenga kuimarisha taratibu zinazofikiwa katika mnyororo wa muundo wa haki jinai ambazo ni uzuiaji wa uhalifu; kubaini uhalifu unapotokea;

ukamataji wahalifu; upelelezi wa makosa ya jinai; uendeshwaji na usikilizwaji wa mashauri Mahakamani; utoaji wa adhabu; urekebishaji wahalifu na ufuatilajji wa mienendo ya wanaokamilisha adhabu zao na wanaoachiwa kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu taratibu za kisheria, haki pamoja na wajibu wa kutoa taarifa za uhalifu kwa kushirikiana na vyombo vya dola katika kudhibiti vitendo vibaya katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usikilizwaji wa mashauri Mahakama ya Tanzania imeendelea kutekeleza mkakati wa kupunguza mlundikano wa mashauri ili kuhakikisha wananchi wanapata haki kwa wakati. Kwa upande wa usikilizwaji mashauri, Julai, 2020 Mahakama ilianza ikiwa na jumla ya mashauri 68,581 na kusajili mashauri mapya 175,311 ambapo hadi kufikia Machi, 2021 mashauri 177,344 yalisikilizwa, sawa na asilimia 73 na kubaki na mashauri 66,548, sawa na asilimia 27, ambayo yako kwenye hatua mbalimbali za kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Rufani ilianza na mashauri 3,966 na kusajili mashauri 1,583 ambapo hadi Machi, 2021 mashauri 831, sawa na asilimia 15, yalisikilizwa na kubaki mashauri 4,718 sawa na asilimia 85. Aidha, kwa upande wa Mahakama Kuu na Kanda zake ilianza Julai, 2020 na mashauri 13,410 na mashauri mapya yaliyosajiliwa ni 9,791 ambapo hadi Machi, 2021 mashauri 10,156, sawa na asilimia 44, yalisikilizwa na kubaki mashauri 13,045, sawa na asilimia 56.

Mheshimiwa Naibu Spika, Divisheni za Mahakama Kuu zilianza na mashauri 4,837 na kusajili mashauri 3,567 ambapo hadi kufikia Machi, 2021 mashauri 3,485, sawa na asilimia 41 yalisikilizwa na kubaki na mashauri 4,919, sawa na asilimia 59, ambayo yapo katika hatua mbalimbali za kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi juu ya mwenendo wa usikilizaji wa mashauri katika ngazi zote za Mahakama ya Tanzania yanapatikana katika ukurasa wa 12 na 13 kwenye kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendeshaji wa Mashtaka ya Jinai; katika mwaka wa fedha, 2020/2021, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kutekeleza jukumu la uratibu na usimamizi wa shughuli za upelelezi, ilishughulikia majalada 22,926 kutoka vyombo vya upelelezi. Kati ya hayo, majalada 14,006 sawa na asilimia 61 yaliandaliwa hati za mashtaka; majalada 2,020 sawa na asilimia tisa yalifungwa na majalada 4,638 sawa na asilimia 20 yalirejeshwa kwa upelelezi zaidi, hivyo kufanya majalada yaliyofanyiwa kazi kuwa 20,664 sawa na asilimia 90. Aidha, majalada 2,262 sawa na asilimia tisa yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kutekeleza jukumu la uratibu na usimamizi wa shughuli za upelelezi, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Jumla ya kesi za jinai 29,436 zilifanyiwa kazi katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ambapo kesi 14,527 sawa na asilimia 49 zilihitimishwa. Kati ya hizo, kesi 7,571 zilihitimishwa kwa washtakiwa kutiwa hatiani, ambayo ni sawa na asilimia 52.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi iliendesha kesi za jinai 5,282 katika Mahakama Kuu ya Tanzania ambapo kati ya hizo, kesi 2,203 ni za vikao vya Mahakama Kuu na kati ya hizo, kesi 698 sawa na asilimia 32 zilihitimishwa na kesi 1,505 sawa na asilimia 68 zinaendelea katika hatua mbalimbali. Aidha, kesi 3,079 zilihusu rufaa za Mahakama Kuu ambapo kesi 1,656 sawa na asilimia 54 zilihitimishwa na kesi 1,423 sawa na asilimia 46 zinaendelea katika hatua mbalimbali.

Vilevile, rufaa 786 za jinai zilifanyiwa kazi katika Mahakama ya Rufani ambapo kati ya hizo, rufaa 230 sawa na asilimia 29 zilihitimishwa na rufaa 556 zinaendelea katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu uratibu na usimamizi wa shughuli za upelelezi uendeshaji wa kesi za jinai pamoja na mafanikio yake yanapatikana kwenye ukurasa wa 13 hadi 15 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi; Wizara kuititia, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kujenga uwezo wa kitaasisi katika kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa kuhakikisha kuwa maslahi ya Taifa yanazingatiwa wakati wa uendeshaji wa mashauri hayo ambayo yanajumuisha mashauri ndani ya nchi au ya Kitaifa na ya nje ya nchi au ya kimataifa.

Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Ofisi ilianza na mashauri ya madai 3,111 ya kitaifa na kusajili mashauri mapya 545 na kuwa na jumla ya mashauri 3,656. Katika kipindi hicho mashauri 418 yamemalizika na 3,238 yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mashauri yanayoihusu Serikali kushtakiwa na taasisi au makampuni nje ya nchi, Wizara kuititia Wizara kuititia, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliwa na mashauri ya madai ya kimataifa 20. Kati ya hayo, mashauri manne (4) yamemalizika na 16 yanaendelea kufanyiwa kazi. Maelezo ya kina kuhusu uendeshwaji wa mashauri, usuluhishi pamoja na mafanikio yake yanapatikana kwenye ukurasa wa 15 hadi 17 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utoaji wa Ushauri wa Kisheria; kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara imeendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakala na Taasisi nyingine za Serikali na Mashirika ya Umma. Katika mwaka wa fedha, 2020/2021, maombi ya ushauri wa kisheria 768 yalipokelewa na kufanyiwa kazi. Kati ya maombi hayo, maombi 165 yalihusu masuala ya utawala; 98 yalihusu masuala ya uchumi; na 502 yalihusu masuala ya utoaji haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Mifumo ya Sheria mbalimbali; katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara kuititia Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea kuhakikisha sheria za nchi zinafanyiwa mapitio na maboresho ili ziendane na wakati kwa kuzingatia mabadiliko katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Katika kipindi husika, mifumo ifuatayo iliyofanyiwa mapitio:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mfumo wa Sheria Unaosimamia Uwakilishi wa Kisheria Mahakamani; Mfumo wa Sheria Unaosimamia Wazee wa Mahakama; na Mfumo wa Sheria unaosimamia Utatuzi wa Migogoro ya Kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yaliyomo katika taarifa hizi yamekusudia kuongeza kiwango cha wananchi kupata haki kwa wakati, uhakika na gharama nafuu. Aldha, Tume imeanza kufanya utafiti kuhusu Mfumo wa Sheria zinazosimamia Masoko ya Mazao ya Kilimo nchini. Utafiti huo unafanyika katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam, Mtwara, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Iringa na Njombe. Lengo la utafiti huo ni kubaini changamoto za mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mapitio ya mfumo wa sheria nilizotaja, imefanyika tathmini ya sheria zinazohusu mfumo wa kutoa adhabu mbadala na uboreshaji wa sekta ya utalii ambapo jumla ya sheria 12 katika mifumo hii zimefanyiwa tathmini kama bado zinakidhi mahitaji ya jamii kwa sasa na siku za usoni. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa jukumu hilo yanapatikana kwenye ukurasa wa 18 hadi 19 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki wa Mikataba mbalimbali inayoihusu Serikali; kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara imeendelea kufanya majadiliano na upekuzi wa Mikataba mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Katika mwaka wa fedha, 2020/2021, Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa 713 na Hati za Makubaliano 46 zilifanyiwa upekuzi. Kati ya Mikataba hiyo, 168 ilihusu masuala ya uwekezaji, ujenzi na ukarabati wa majengo; 191 masuala ya

ununuzi; 127 masuala ya utoaji wa huduma za jamii; 79 masuala ya uchumi na fedha; 75 masuala ya rasilimali na maliasili; na 73 masuala ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mikataba iliyofanyiwa upekuzi, 365 ilithaminishwa katika sarafu mbalimbali ambapo 273 ilikuwa na thamani ya Shilingi Trilioni 4.5, mikataba 73 ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani 1,328,494,478.29 sawa na Shilingi Trilioni 3.09 na mikataba 19 ilikuwa na thamani ya fedha ya Umoja wa Ulaya (*Euro*) 410,574,162.33 sawa na Shilingi Trilioni 1.08.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala ya Haki za Binadamu na Haki za Watu; katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2020/2021, Wizara iliendelea kuimarisha mifumo ya kisera ya utekelezaji wa haki za binadamu na haki za watu nchini. Aldha, Wizara illifanya majadiliano na wadau wa Serikali juu ya kuboresha mfumo wa uandaaji na uwasilishajhi wa Taarifa za Nchi za Utekelezaji wa Mikataba zinazohusu haki za wanawake na haki za mtoto ambayo Serikali imeridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni pamoja na Wizara kushiriki katika vikao vya kikanda na kimataifa vya haki za binadamu na haki za watu, kwa lengo la kutoa taarifa za nchi kuhusu hali ya utekelezaji wa haki za binadamu, zaidi ya hayo imeendelea kuelimisha watumishi wa Serikali kuhusu masuala ya za haki za binadamu ili kuhakikisha haki hizo siyo tu zinazingatiwa bali pia zinahifadhiwa na kulindwa na watumishi hao wakati wanapotekeleza majukumu ya Kiserikali katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora nchini. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Tume ilianza na malalamiko 2,361 na kupokea malalamiko mapya 354 na hivyo kufanya jumla ya malalamiko kuwa 2,715.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Machi, 2021, malalamiko 281 yamefanyiwa uchunguzi na kuhitimishwa na kubaki na malalamiko 2,434 ambayo yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi. Aidha, Tume ilifanya ziara za kimkakati katika mikoa 19 ya Tanzania Bara na mitano ya Zanzibar kwa lengo la kushughulikia malalamiko 574 ya muda mrefu ambapo kati ya hayo malalamiko 230 yalipatiwa ufumbuzi. Vilevile, Tume ilishughulikia malalamiko 96 ya watumishi kutoka Taasisi nane za umma Jijini Dodoma ambapo malalamiko 48 yalipatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume inaendelea kuboresha mfumo wa TEHAMA kwa kushughulikia malalamiko pamoja na kuhuisha mfumo wa utunzaji kumbukumbu. Maelezo kuhusu utekelezaji wa masuala za haki za binadamu na haki za watu yanapatikana kwenye ukurasa wa 20 hadi 23 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Msaada wa Kisheria; Wizara iliendelea kuratibu jukumu la utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, iliendesha zoezi la ukaguzi kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria ili kujiridhisha na huduma wanazotoa. Aidha, Wizara iliratibu maandalizi na kushiriki maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria yaliyofanyika kitaifa katika Mkoa wa Tanga ambapo wananchi 314,000 walipatiwa huduma ya msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikoa mingine idadi ya wananchi waliopatiwa huduma hiyo ni 1,455,566. Kati ya hao, 529,079 walikuwa wanawake, 514,051 walikuwa wanaume na 412,436 walikuwa watoto. Vilevile, huduma ya msaada wa kisheria ilitolewa kwa wafungwa na mahabusi 8,442 katika magereza 11 na vituo vya polisi 26 katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Wizara pia ilishughulikia malalamiko 101 ya wananchi yaliyowasilishwa Wizarani katika kipindi husika. Wizara imekubaliana na Mhimili wa Mahakama kuanzisha Madawati ya Msaada wa Kisheria katika Mahakama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuendesha Mafunzo ya Watoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria; katika mwaka wa fedha, 2020/2021, Wizara iliendelea kuratibu jukumu la kutoa mafunzo ya msaada wa kisheria ili kuhakikisha kwamba huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi, hususan kwa wasio na uwezo wa kugharamia huduma za kisheria wanapata huduma hiyo bure na kwa wakati. Kwa sehemu kubwa, mafunzo hayo yalitolewa wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria yaliyofanyika Novemba, 2020 katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo hayo yalihusu utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi na taasisi zilizosajiliwa kutoa huduma pamoja na viongozi mbalimbali wanaohusika na utatuzi wa migogoro katika jamii wakiwemo Wabunge, Kamati za Usalama, Watendaji wa Kata na Wajumbe wa Mabaraza ya Kata na Vijiji.

Aidha, wakati wa zoezi la kutoa mafunzo hayo Wizara iliweka msisitizo zaidi kwa mafunzo ya wasajili wasaidizi na watoa huduma ya msaada wa kisheria pamoja na wasaidizi wa kisheria ili kuhakikisha huduma ya msaada wa kisheria inapatikana kwa makundi maalum hususan haki ya mtoto. Maelezo ya kina kuhusu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria inapatikana ukurasa wa 24 hadi 26 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala ya Kusaidia katika Masuala ya Jinai Kimataifa; Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipokea jumla ya maombi manne ya kusaidiana katika masuala ya jinai. Maombi hayo yalihusu upatikanaji wa nyaraka za ushahidi na kuwahoji mashahidi walioko nchini kwa kesi za jinai zinazoendelea katika mataifa mengine. Kati ya maombi hayo, ombi moja limekamilika na maombi matatu yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliwasilisha maombi matatu ya upatikanaji wa nyaraka za ushahidi na kuwahoji mashahidi waliopo nje ya nchi. Maombi hayo yanaendelea kufanyiwa kazi katika nchi

hizo. Masuala ya ushirikiano wa kisheria na mataifa mengine katika masuala mbalimbali ya jinai yameelezwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uangalizi na Ufutiliaji wa Utajiri wa Asili na Maliasili Nchini; Wizara ya Katiba na Sheria imepewa jukumu la kuratibu masuala ya uangalizi wa utajiri asili na maliasili za nchi kupitia Sheria za Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Utajiri Asili na Maliasili za Nchi, Sura ya 449 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri Asili na Maliasili za Nchi, Sura 450. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta iliendelea kutekeleza shughuli za kuweka mifumo na kutoa miongozo mbalimbali ili shughuli za uchimbaji, utafutaji, uvunaji na utumiaji wa utajiri asili na maliasili asilia za nchi kuzingatia sheria kiongozi na kufanya ufuutiliaji wa utekelezaji wa Sheria, Sura 449 na Sura 450 ili kupima manufaa wanayoyapata wananchi kwa maeneo yaliyopo karibu na miradi ya pamoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeleo ya kina kuhusu utekelezaji wa jukumu la uangalizi na ufuutiliaji wa utajiri asili na maliasilia ya nchi yanapatikana kwenye ukurasa wa 28 hadi 30 wa kitabu cha hotuba yangu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri ungeenda kwenye mwaka wa fedha 2021/2022, kwa sababu naambiwa hapa muda wako uliobaki ni kidogo.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kisera katika sekta ya sheria ikiwa ni pamoja na kuratibu masuala yanayotekeliza na taasisi za Wizara kwa lengo la kutekeleza Dhima ya Wizara ili kuifikia Dira ya Wizara iliyowekwa. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara na Taasisi zimeainisha vipaumbele katika ukurasa wa 46 hadi 51.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vyta majukumu ya Wizara na Taasisi, Wizara

inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 78,464,886,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti kwa mafungu saba ya Wizara na Taasisi zake ni kama ifuatavyo: Fungu 12, 16, 19, 35, 41, 55 na 59.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, naliomba Bunge lako liidhinishe kiasi cha Sh. 153,228,859,000 kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama inayofafanuliwa kwenye ukurasa wa 55 na 59 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa kwenye vitabu vya Kasma za Mafungu husika ambavyo vimegawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge kuititia Mfumo wa kielektroniki wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako likubali kujadili na kuitisha makadirio ya mpango na matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA JOHN
AIDAN MWALUKO KABUDI (MB), WAZIRI WA KATIBA NA
SHERIA, AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO
YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Shukrani na Pole

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa wingi wa rehema zake na kuniruzuku uhai na afya njema iliyoniwezesha kusimama hapa leo katika Bunge lako kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita, kwa kuniamini na kunteua kuitumikia Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika nafasi ya Waziri wa Katiba na Sheria. Naahidi kuitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na unyenyekevu kwa maslahi mapana ya Taifa. Namwomba Mwenyezi Mungu anijalie hekima, ujasiri na busara ili niweze kutimiza wajibu huu.

3. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mnamo tarehe 17 Machi, 2021 taifa letu lilitpatwa na msiba mkubwa kwa kuondokewa na kiongozi, jemedari na shujaa wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na tulimpumzisha kwenye nyumba yake ya milele tarehe 26 Machi, 2021. Taifa limepatwa na masikitiko na majonzi makubwa kwa kumpoteza shujaa huyu wa mfano kwa Afrika na dunia nzima. Mwenyezi Mungu aipokee roho yake na kumpa pumziko la amani mpPENDWA wetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Amina.

4. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha, 2020/2021, Taifa lilipatwa pia na vifo vya Viongozi Waandamizi waliokuwa wakilitumikia Taifa katika nyadhifa mbalimbali. Viongozi hao ni pamoja na Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar; Mheshimiwa Balozi Mhandisi John William Kijazi aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi; Mheshimiwa Jaji (Mstaafu) Harold Reginald Nsekela aliyekuwa Kamishna wa Maadili katika Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Mheshimiwa Bethuel Mmila aliyekuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani; Mheshimiwa Salvatory Bongole aliyekuwa Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Mheshimiwa

Martha Umbula aliyejekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara; Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Nditiye aliyejekuwa Mbunge wa Muhammadi; pamoja na viongozi wengine waliotumikia Taifa hili katika nyadhifa mbalimbali. Hivyo, nitumie fursa hii kutuma salamu zangu za pole kwa Taifa kwa ujumla na ndugu waliopoteza wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahala pema peponi. Amina.

Salamu za Pongezi

5. Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuapishwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke kuliongoza Taifa letu katika Serikali ya Awamu ya Sita. Tunaendelea kumwombea kwa Mungu ampe maisha yenye siha na afya njema ili aweze kutekeleza vyema majukumu ya kuiongoza nchi yetu. Aidha, kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge hili kwa asilimia mia moja kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Othman Masoud Othman Sharif kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Nawapongeza wabunge wote walioshinda uchaguzi kwenye majimbo yao na walioteuliwa. Hali kadhalika, nawapongeza Balozi Hussein Athman Kattanga kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhandisi Zena Ahmed Said kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa Zanzibar na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

6. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imeweka msingi wa mwelekeo wa kisera katika

utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia shughuli za Serikali.

7. Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba nimpongeze Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, nitumie nafasi hii kumpongeza kwa uongozi wake mahiri wa kuiwezesha kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi wakati akiwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Sillo Daniel Baran Mbunge wa Babati Vijijini, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa kuiongoza kamati hiyo ambayo ilipitisha Mpango na Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Vilevile, natoa shukrani za dhati kwa Kamati hizo kwa kazi kubwa ya kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Wizara inatambua na inathamini sana mchango wa Kamati hizo katika kuhakikisha Sekta ya Sheria inaendelea kuimarika na kutoa mchango stahiki katika kufanikisha mipango ya Taifa letu kwa maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Wizara inayo imani kubwa kwa Kamati hizo za Kudumu za Bunge na itaendelea kuzipatia ushirikiano unaostahili.

8. Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza mawaziri wenzangu na naibu mawaziri walioteuliwa tarehe 31 Machi, 2021 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, kuziongoza wizara mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakia kila la kheri wote walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali katika utumishi wa umma kwa utekelezaji wa majukumu yao mapya ya kuwatumikia wananchi.

B. DIRA NA DHIMA

9. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na Dira ambayo ni **Katiba na Sheria Wezeshi kwa Maendeleo ya Taifa**. Pamoja na miongozo mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, Dira hii inatoa mwelekeo wa kisera na kisheria katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa, hususan katika kudumisha hali ya amani, utulivu na utangamano wa kitaifa ambazo ni nguzo muhimu za kujenga taifa linalozingatia utawala wa sheria. Aidha, Dhima ya Wizara ni **kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na Sheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa**. Kwa ujumla, Dira na Dhima hizi zinaakisi Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, kwa kubainisha jinsi sekta ya sheria itakavyotoa mchango wake kufanikisha Dira hiyo ifikapo mwaka 2025.

Katika kipindi cha kuelekea mwaka 2025, Wizara ya Katiba na Sheria imepanga na itaendelea kuweka mipango na mikakati inayojielekeza katika kuendelea kuyafikia maono yaliyopo katika Ibara ya 1.2.3, shabaha zilizopo katika Ibara ya 3.2, msukumo uliopo katika Ibara ya 4.3, na maelekezo ya utekelezaji yaliyopo katika Ibara ya 5 ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Masuala ha yanagusa utawala wa sheria kama sehemu muhimu ya utawala bora itakayofanikisha maendeleo ya Taifa letu yanayotarajiwaa ifikapo mwaka 2025.

C. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

10. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mhimili wa Mahakama ya Tanzania; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Tume ya Utumishi wa Mahakama; Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini; Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania; Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto; Baraza la Elimu ya Sheria, Bodi ya Taifa ya Msaada wa Kisheria na Masijala za masuala

ya utajiri na maliasilia za nchi pamoja na upatanishi, majadiliano, maridhiano na usuluhishi.

11. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake ambayo ni pamoja na kutunga Sera za masuala ya kikatiba na kisheria na kuhakikisha utekelezaji wake; masuala ya kikatiba; haki na mfumo wa utoaji haki; uandishi wa sheria; uendeshaji wa mashtaka ya jinai; uratibu, usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai yanayohusu serikali; uhakiki wa mikataba mbalimbali inayohusu serikali; masuala ya sheria za kimataifa; masuala ya haki za binadamu (ikiwemo haki za watu); huduma ya msaada wa kisheria; urekebu wa sheria; masuala ya usafirishaji wa wahalifu kuletwa nchini au kwenda nje ya nchi; masuala ya ushirikiano wa kisheria na mataifa mengine katika masuala mbalimbali ya jinai; usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka, ufilisi, udhamini na kuasili watoto; uangalizi na ufuatilaji wa utajiri na maliasilia za nchi; utendaji na uendelezaji wa rasilimaliwa katika Wizara; na Shughuli za Taasisi, mipango na miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara.

D. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

12. Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara na Taasisi zake ilibainisha masuala mahsus ya kipaumbele kuwa msingi wa kutekeleza majukumu yake. Masuala hayo yameainishwa katika **KIAMBATISHO A** cha hotuba hii. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

I. SERA ZA MASUALA YA KIKATIBA NA KISHERIA NA KUHAKIKISHA UTEKELEZAJI WAKE

a) Kukamilisha Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria

13. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha, 2020/2021, Wizara iliendelea na Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali ndani ya Serikali katika

kupata maoni kuhusu malengo yake. Hatua inayofuata ni kuwashirikisha wadau zaidi ili kupata maoni kuhusu mahitaji ya Sera ya Taifa kwenye Sekta ya Sheria. Aidha, Wizara pia ilishiriki katika mkutano wa siku moja wa wadau wa Sera nchini, ulioratibiwa na Ofisi ya Rais - IKULU kwa kushirikiana na Taasisi ya Uongozi. Pamoja na masuala mengine washiriki wa mkutano huo walipatiwa uelewa kuhusu uandaaji wa Sera za Kitaifa. Ni matumaini ya Wizara kuwa mkutano huo umekuwa na mchango katika maandalizi ya Sera zinazohusu sekta ya sheria.

b) Marekebisho ya Sheria na Kutafsiri Sheria Kutoka Lugha ya Kiingereza Kwenda Lugha ya Kiswahili

14. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imekamilisha maandalizi ya sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1/2021, ambayo pamoja na mambo mengine, imeruhusu rasmi lugha aushi ya Kiswahili kuwa lugha ya uandishi wa Sheria, uendeshaji wa shughuli za Mahakama, Mabaraza na vyombo vingine vyenye jukumu la kutoa haki hapa nchini. Lengo la kutafsiri sheria hizo ni kutekeleza matakwa ya Kimataifa yanayozitaka nchi kutumia lugha inayoleweka kwa wananchi ili kuweza kuwafikia na kuwawezesha kupata haki zao kwa urahisi na kwa wakati.

15. Mheshimiwa Spika, mara baada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 ya Mwaka 2021 kupitishwa na Bunge, Wizara ilianza kuratibu zoezi la kutafsiri Sheria zote za Nchi kutoka lugha Kiingereza kuwa lugha ya Kiswahili ili kutekeleza matakwa ya sheria hiyo. Wizara ilichukua hatua mbalimbali ambazo ni pamoja na kutoa mwongozo na utaratibu wa zoezi la kutafsiri sheria. Aidha, iliajiza kuwa kila Wizara, mamlaka na taasisi za umma zitafsiri sheria inayozisimamia na kuandaa Rasimu ya Kwanza ya tafsiri ya sheria zake. Katika kusimamia maagizo hayo, Wizara iliandaa Mpango Kazi wa kutafsiri sheria hizo na kuuwasilisha kwenye kila Wizara, Mhimili wa Bunge na katika Mhimili wa Mahakama.

16. Mheshimiwa Spika, Wizara imeshatoa Mwongozo kwa Wizara zote kuanza na kukamilisha tafsiri za Sheria Kuu zipatazo **449** pamoja na sheria ndogo zipatazo **39,000** zinazosimamiwa na Wizara husika au Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Hadi Machi, 2021 jumla ya sheria kuu zilizotafsiriwa ni **157** na Sheria ndogo zaidi ya **15,000**. Aidha; Mwongozo huo unaelekeza kuandaliwa kwa Kamusi ya Istilahi za Kisheria. Inatarajiwa kwamba zoezi la kutafsiri Sheria Kuu na Kamusi litakamilika Desemba, 2021 na kuendelea na maandalizi ya kutafsiri Kanuni za Sheria mbalimbali zoezi linalotarajiwa kukamilika Juni, 2022. Wizara inawataka wadau wanaohusika na zoezi la kutafsiri sheria kuzingatia mwongozo huo ili kuweza kukamilisha jukumu hilo katika muda uliopangwa. Vilevile, kila Wizara au taasisi wanaohusika katika zoezi la kutafsiri Sheria kuwashirikisha ipasavyo wataalamu wa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) na Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili (TATAKI) kwenye zoezi hilo kwa kuwa ndio Taasisi zenyenye utaalamu wa Lughya ya Kiswahili. Ninfahamu Kiswahili cha sheria ni tofauti kidogo na Kiswahili cha kawaida, kama ilivyo kwa lugha ya Kiingereza. Ushirikiano na taasisi hizi na nyininge zenyenye uelewa wa masuala haya, ikiwa ni pamoja na kutoka upande wa pili Muungano, yaani Tanzania Zanzibar, utatusaidia kujenga uelewa wetu zaidi katika tasnia ya sheria katika suala hili.

17. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 baadhi ya Wizara na taasisi pamoja na Mihimili ya Bunge na Mahakama zimeanza kazi ya kutafsiri Sheria na Kanuni zake kwa kuishirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Tasisi zake ilibainisha sheria **50** ambazo inazisimamia ili kuzitafsiri. Katika kutekeleza zoezi hilo, Wizara na taasisi zake iligawana sheria hizo ili zitafsiriwe kisekta kwa kuzingatia taasisi na sheria inayoitkeleza. Katika mgawanyo huo, Wizara (Makao Makuu) iliunda timu ya kutafsiri sheria 17 ilizopangiwa na kukamilisha zoezi hilo tarehe 22 Machi, 2021 na hatimaye kupata Rasimu ya Kwanza ya sheria zilizotafsiriwa. Timu hiyo iliundwa na wataalam wa Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Kurekebisha Sheria, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania na Chama cha Wanasheria Tanganyika. Taasisi nyininge ndani ya Wizara

ziko katikaa hatua ya mwisho kukamilisha tafsiri ya sheria kuu nyiningine **33** zilizosalia.

Wizara nyiningine zote pamoja na taasisi zinaendelea na zoezi la kutafsiri sheria zinazosimamiwa na Wizara na taasisi hizo kwa kuzingatia Mpango Kazi ulioandalialiwa ili ifikapo Desemba, 2021 Sheria zote ziwe zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Hadi kufikia Machi, 2021 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeweza kutafsiri jumla ya Sheria Kuu **6** pamoja na Kanuni 9 za sheria hizo. Sheria hizi zimewasilishwa Wizarani ili hatimaye ziwasilishwe kwenye Kikosi Kazi cha Taifa cha kuhariri Rasimu ya Kwanza ya Sheria zilizotafsiriwa na sekta zinazosimamia na kutumia sheria hizo.

18. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mhimili wa Mahakama, uko katika hatua za mwisho kukamilisha zoezi la kutafsiri kanuni zaidi ya **50** zilizotayarishwa na Jaji Mkuu. Aidha, Mhimili wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tayari umetafsiri sheria unazosimamia. Nichuke fursa hii kuwapongeza wote ambao wameifanya kazi hii kwa ufasaha na kupata mafanikio niliyoyaeleza. Asanteni sana kwa kazi nzuri na inayotia moyo. Kwa wale ambao bado kuanza au kukamilisha hatua za kuanza kutafsiri, nichukue pia fursa hii kuwakumbusha kuanza kazi hiyo mara moja ili sote tuendane na mpango kazi wetu na hatimaye kuimaliza kazi hii kwa wakati.

19. Mheshimiwa Spika, katika kipindi husika, Wizara pia ilisimamia utekelezaji wa Sheria ya Usuluhishi Sura ya 15 na kuandaa Kanuni za kutekeleza Sheria hiyo. Kanuni hizo zilizochapishwa kwenye Gazeti la Serikali kwa Matangazo Na. 146, 147, 148, na 149 ya terehe 29 Januari, 2021 zinahusu; Ithibati ya wanaojihusisha na utatuvi wa migogoro nje ya mfumo wa mahakama; Kanuni za Kituo cha Usulushi; Kanuni za Utawala za Kituo cha Usuluhishi na Kanuni za Maadili ya wanaojihusisha na utatuvi wa migogoro nje ya mfumo wa mahakama. Aidha, Wizara inaratibu uanzishwaji wa kituo cha usuluhishi cha Tanzania ambacho Makao Makuu yake yatakuwa Jijini, Arusha. Vilevile, imeanzishwa ofisi ya Msajili wa Ithibati ya Watoa Huduma za Maridhiano, Majadiliano,

Upatanishi na Usuluhihi. Katika kusimamia ithibati hiyo umeanzishwa mfumo wa usajili wa watoa huduma za Maridhiano, Majadiliano, Upatanishi na Usuluhihi. Inatarajiwa kuwa Kituo hicho cha usuluhihi Tanzania kitaanza kazi rasmi Julai, 2021.

c) Kukamilisha Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha, 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Uongozi, ilifanya utafiti kuhusu visababishi vyta changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya Sheria kwa kufanya mapitio na uchambuzi wa taarifa mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi katika sekta hiyo. Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kuhakiki sababu zilizobainishwa na wadau kuwa ni chanzo cha changamoto hizo na kupendekeza hatua za kisera na mikakati ya kuzitatua. Wizara, inaandaa andiko la *Mapendekezo ya Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria*, itakayokuwa na malengo ya kutatua changamoto zilizopo na kuiwezesha sekta ya Sheria kutoa mchango stahiki katika kufanikisha malengo ya kitaifa ya kuleta maendeleo nchini.

II. MASUALA YA KIKATIBA

20. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya sheria imeendelea kuhakikisha kwamba Katiba ya Nchi inatekelezwa kuendana na mahitaji yaliyopo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni ili kuimarisha utendaji wa sekta mbalimbali hapa nchini. Suala kubwa la Kikatiba lililotekelawa katika Mwaka wa Fedha 2020/21 ni Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ambaao ulifanyika Oktoba, 2020 kwa amani, utulivu, haki na kwa kuzingatia Katiba ya nchi. Hata hivyo, katika kipindi hicho, nchi ilimpoteza Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Josef Magufuli tarehe 17 Machi, 2021 na kupumzishwa kwenye nyumba yake ya milele tarehe 26 Machi, 2021. Kutokana na kifo hicho, Katiba ya nchi ilifuatwa na kuwezesha upatikanaji wa Rais wa Awamu ya Sita wa nchi yetu

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa amani na utulivu mkubwa. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu maendeleo ya Katiba ikiwa na pamoja na uzingatiwaji wa sheria, kanuni na miongozo ya kisheria iliyopo.

III. HAKI NA MFUMO WA UTOAJI HAKI

a)Maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai

21. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mifumo ya haki jinai nchini, Wizara kupitia mradi wa Programu Endelevu ya Kuzuia Rushwa Nchini, ilikamilisha andiko la mapendekezo ya Programu ya Maboresho ya Haki Jinai na Mpango kazi wa utekelezaji. Maboresho hayo yanalenga kuimarisha taratibu zinazofikiwa katika mnyororo wa mfumo wa haki jinai ambazo niuzuiaji wa uhalifu; kubaini uhalifu unapotokea; ukamataji wahalifu; upelelezi wa makosa ya jinai; uendeshwaji na usikilizwaji wa mashauri mahakamani; utoaji wa adhabu; urekebishaji wahalifu na ufuutiliaji wa mienendo ya wanaokamilisha adhabu zao au wanaoachiwa kwa sababu mbalimbali. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu taratibu za kisheria, haki pamoja na wajibu wa kutoa taarifa za uhalifu kwa kushirikiana na vyombo vya dola katika kudhibiti vitendo vibaya katika jamii.

b)Usikilizwaji wa mashauri

22. Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania imeendelea kutekeleza mkakati wa kupunguza mlundikano wa mashauri ili kuhakikisha wananchi wanapata haki kwa wakati. Kwa upande wa usikilizwaji mashauri, Julai 2020 Mahakama ilianza ikiwa na jumla ya mashauri **68,581** na kusajili mashauri mapya **175,311** ambapo hadi kufikia Machi, 2021 mashauri **177,344**yalisikilizwa, **sawa na asilimia 73** na kubaki na mashauri **66,548**, sawa na **asilimia 27**, ambayo yako kwenye hatua mbalimbali za kufanyiwa kazi. Mahakama ya Rufani ilianza na mashauri **3,966** na kusajili mashauri **1,583** ambapo hadi Machi, 2021 mashauri **831**, sawa na **asilimia 15**, yalisikilizwa na kubaki mashauri **4,718** sawa na **asilimia 85**. Aidha, kwa upande wa Mahakama Kuu na Kanda zake ilianza Julai, 2020

na mashauri **13,410** na mashauri mapya yaliyosajiliwa ni **9,791** ambapo hadi Machi, 2021 mashauri **10,156**, **sawa na asilimia 44**, yalisikilizwa na kubaki mashauri **13,045**, **sawa na asilimia 56**. Divisheni za Mahakama Kuu zilianza na mashauri **4,837** na kusajili mashauri **3,567** ambapo hadi kufikia Machi, 2021 mashauri **3,485**, sawa na **asilimia 41** yalisikilizwa na kubaki na mashauri **4,919**, sawa na **asilimia 59**, ambayo yapo katika hatua mbalimbali za kufanyiwa kazi.

23. Mheshimiwa Spika, Mahakama za Hakimu Mkazi, zilianza Julai, 2020 na mashauri **9,838**na kusajili mashauri mapya **8,686** ambapo hadi Machi, 2021 mashauri **9,820**, sawa na **asilimia 53** yalisikilizwa na kubaki na mashauri **8,704**, sawa na **asilimia 47**. Aidha, Mahakama za Wilaya zilianza Mwaka na Mashauri **17,308** na kipindi husika, na kusajili mashauri mapya **30,573** ambapo mashauri **30,244**, sawa na asilimia 63, yalisikilizwa na kubaki na mashauri **17,637**, sawa na **asilimia 37**. Vilevile, kwa upande wa Mahakama za Mwanzo zilianza mwezi Julai, 2020 na mashauri **19,222** na kusajili mashauri mapya **121,111** ambapo hadi Machi, 2021, mashauri **122,808**, sawa na **asilimia 88** yalisikilizwa na kubaki na mashauri **17,525**, sawa na **asilimia 12** ambayo yapo kwenye hatua mbalimbali za kusikilizwa.

24. Mheshimiwa Spika, Mahakama iliendelea na uendeshaji wa *Mahakama Zinazotembea (Mobile Courts)* katika mikoa ya Mwanza na Dar es Salaam. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Mahakama hizi zilianza na Mashauri **83** na kusajili mashauri mapya **518**, ambapo hadi Machi, 2021, mashauri **531**, sawa na **asilimia 88** yalisikilizwa na kubaki na mashauri **70**, **sawa na asilimia 12** ambayo yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Mahakama hizi pia zinatoa huduma za elimu kwa umma kuhusiana na masuala mbalimbali ya upatikanaji haki ambapo jumla ya wananchi **6,378** wamenufaika na huduma hiyo.

IV. UENDESHAJI WA MASHTAKA YA JINAI

25. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha, 2020/2021, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kutekeleza

rukumu la uratibu na usimamizi wa shughuli za upetelezi, ilishughulikia majalada **22,926** kutoka vyombo veya upetelezi. Kati ya hayo, majalada **14,006** sawa na **asilimia 61** yaliandaliwa hati za mashtaka; majalada **2,020** sawa na asilimia Tisa **(9)** yalifungwa na majalada **4,638** sawa na **asilimia 20** yalirejeshwa kwa upetelezi zaidi, hivyo kufanya majalada yaliyofanyiwa kazi kuwa **20,664** sawa na **asilimia 90**. Aidha, majalada **2,262** sawa na **asilimia Tisa (9)** yanaendelea kufanyiwa kazi.

26. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kuititia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Jumla ya kesi za jinai **29,436** zilifanyiwa kazi katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ambapo, kesi **14,527** sawa na **asilimia 49** zilihitimishwa. Kati ya hizo, kesi **7,571** zilihitimishwa kwa washtakiwa kutiwa hatiani, ambayo ni sawa na **asilimia 52**. Ofisi iliendesha kesi za jinai **5,282** katika Mahakama Kuu ya Tanzania ambapo kati ya hizo, kesi **2,203** ni za vikao veya Mahakama Kuu na kati ya hizo, kesi **698** sawa na **asilimia 32** zilihitimishwa na kesi **1,505** sawa na **asilimia 68** zinaendelea katika hatua mbalimbali. Aidha, jumla ya kesi **3,079** zilihusu rufaa za Mahakama Kuu ambapo kesi **1,656** sawa na **asilimia 54** zilihitimishwa na kesi **1,423** sawa na asilimia **46** zinaendelea katika hatua mbalimbali. Vilevile, rufaa **786** za jinai zilifanyiwa kazi katika Mahakama ya Rufani ambapo kati ya hizo, rufaa **230** sawa na asilimia **29** zilihitimishwa, na rufaa **556** zinaendelea katika hatua mbalimbali.

27. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, washtakiwa walioitiwa hatiani kutokana na kesi za jinai walipewa adhabu mbalimbali zikiwemo za vifungo, faini na mali kutaifishwa. Kiasi cha **Shilingi 1,230,258,839.00** kililipwa mahakamani kama faini katika kesi **4,738**. Katika kipindi hicho, mali mbalimbali zilitaifishwa kuwa mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mali hizo ni pamoja na fedha taslimu kiasi cha **Shilingi 5,554,321,919.41**, magari **14**, nyumba Tatu **(3)**, pikipiki Sita **(6)**, magogo **105**, Mbao **3,205**, seti moja **(1)** ya kompyuta, Kompyuta mpakato mbili **(2)**, runinga mbili

(2), Kamera moja (1), meno ya Tembo mawili (2), Meno ya Kiboko matatu (3) na madini ya **Almas Karats 71,654** yenye thamani ya Dola za Marekani **29,509,821.84**.

28. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza zoezi la makubaliano ya kumaliza kesi za jinai chini ya utaratibu wa washitakiwa kukiri makosa yao (plea bargaining) kwa mujibu wa sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali Na. 11 ya Mwaka 2019. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya kesi **192** zilihitimisha kwa njia hiyo na jumla ya washitakiwa **243** walikiri makosa na kulipa Serikalini kiasi cha **Shillingi 35,073,204,715.97** kama fidia kwa serikali pamoja na faini kutokana na makosa ya uhujumu uchumi. Zoezi hili ni endelevu na fedha hizi zimewekwa katika akaunti maalum iliyoko Benki Kuu ya Tanzania

29. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza Programu ya Kutenganisha Shughuli za Upenelezi na Uendeshaji Mashtaka kwa kusogeza huduma za mashtaka kwa wananchi katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilifungua Ofisi katika Mkoa wa Songwe na kufanya jumla ya Ofisi za Mikoa kuwa **26**. Aidha, Ofisi za Wilaya tano (**5**) zimefunguliwa katika wilaya za Kahama (Shinyanga), Serengeti (Mara), Mufindi (Iringa), Karagwe (Kagera), na Kilombero (Morogoro) na kufanya jumla ya Ofisi za Wilaya zilizofunguliwa kufikia **16**. Ofisi nyingine zilizokwisha kufunguliwa ni Monduli (Arusha), Kondoa (Dodoma), Ilala, Kigamboni, Temeke na Kinondoni (Dar es Salaam), Illemela (Mwanza), Korogwe (Tanga), Nzega (Tabora), Tarime (Mara) na Chato (Geita). Aidha, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ina mpango wa kufungua Ofisi katika Wilaya ya Kalambo (Rukwa). Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kufungua Ofisi katika Wilaya zilizobaki kadri fedha zitakavyopatikana.

30. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kukagua magereza na vituo vya polisi vinavyohifadhi mahabusi. Lengo la ukaguzi huu ni kuainisha changamoto za kiutendaji na

kiupelelezi na kutoa maelekezo ya kutatua changamoto hizo. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, ilifanya ukaguzi katika magereza **46** na vituo vya polisi **166** katika mikoa **26** ya Tanzania Bara. Kupitia ukaguzi huo mahabusi **1,852** waliachiwakutokana na sababu mbalimbali. Idadi ya vituo vya polisi na magereza yaliyokaguliwa katika kipindi hiki ni kama inavyoonekana katika **KIAMBATISHO B.**

V. UENDESHAJI WA MASHAURI YA MADAI NA USULUHISHI

31. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kujenga uwezo wa kitaasisi katika kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa kuhakikisha kuwa maslahi ya Taifa yanazingatiwa wakati wa uendeshaji wa mashauri hayo. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Ofisi illanza na mashauri yamadai **3,111** ya kitaifa na kusajili mashauri mapya **545** na kuwa na jumla ya mashauri **3,656**. Katika kipindi hichomashauri **418** yamemalizika na **3,238** yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji.

32. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikuwa na mashauri ya madai ya kimataifa **20**, kati ya hayo, mashauri manne (**4**) yamemalizika na **16** yanaendelea kufanyiwa kazi. Katika kuendesha mashauri hayo ya madai ya kitaifa na kimataifa, Serikali imeokoa kiasi cha **Shilingi132,245,636,607.81** ambacho kingelipwa kwa wadai endapo Serikali ingeshindwa kesi hizo.

33. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeiwakilisha Serikali katika Mashauri **15** ya uchaguzi. Kati ya hayo, mashauri ya ubunge yalikuwa manne (**4**) na **11** ya udiwani. Mashauri matatu (**3**) yali funguliwa Mahakama Kuu Zanzibar na Shauri moja (**1**) lili funguliwa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, na mashauri **11** ya udiwani yali funguliwa Mahakama za Hakimu Mkazi katika mikoa ya Dodoma, Ruvuma, Mara, Tabora na Kigoma. Mashauri yaliyokamilika ni **13** ambapomashauri matatu (**3**) ni ya ubunge na mashauri **10** ni ya udiwani. Aidha, shauri moja (**1**) la ubunge na shauri

moja **(1)** la udiwani yapo katika hatua za mbalimbali za usikilizwaji.

34. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kuititia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikuwa na Mashauri **60** ya usuluhishi ambayo ni ya zamani na ilipokea mapya **38**, hivyo kufanya jumla ya mashauri ya usuluhishi kufikia **98**. Kati ya hayo, mashauri **76** ni ya kitaifa na **22** ni ya kimataifa. Hadi kufikia Machi, 2021 mashauri ya kitaifa **27** yamemalizika na kubaki na mashauri **49** ambayo yapo katika hatua mbali mbali za usikilizwaji. Vilevile, katika mashauri ya kimataifa ya usuluhishi mawili **(2)** yalimalizika na kubaki mashauri **20** ambayo yapo katika hatua mbalimbali. Katika Mashauri yaliyomalizika, ofisi imeokoa kiasi cha **Shilingi 511,477,787,314** ambacho kingelipwa kwa wadai endapo Serikali ingeshindwa kesi hizo. Sambamba na hilo, Mashauri **14** ya usuluhishi yalfanyiwa vikao vya maridhiano ambapo taarifa husika ziliwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mwongozo wa maridhiano kabla na baada ya usuluhishi.

VI. UANDISHI, UREKEBU NA UFASIRI WA SHERIA

35. Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuhakikisha kwamba sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali. Katika Mwaka wa Fedha, 2020/2021, Miswada mitatu **(3)** iliwasilishwa bungeni ambayo ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Mbalimbali Sheria Na. 1 wa Mwaka 2021; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2021 na Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Usimamizi wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021. Aidha, jumla ya sheria ndogo **893** zimeandaliwa na kuchapishwa katika matoleo mbalimbali ya Gazeti la Serikali.

36. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitafsiri Sheria Kuu **24** na Sheria Ndogo **17** kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili ili kuongeza uelewa zaidi kwa

wananchina kuwezesha kupata haki zao kwa urahisi. Vilevile, Sheria Kuu **24** zilifanyiwa urekebu ili ziendane na mahitaji ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Sheria zilizofanyiwa urekebu na kutafsiriwa katika kipindi cha Julai,2020 hadi Machi,2021 zimeoneshwa katika **KIAMBATISHO C.** Aidha, kuanzia sasa Serikali itatayarisha na kuwasilisha katika Bunge lako miswada yote ya Sheria kwa lugha ya Kiswahili.

VII. UTOAJI WA USHAURI WA KISHERIA

37. Mheshimiwa Spika, kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara imeendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakala na taasisi nyingine za Serikali na mashirika ya umma. Katika Mwaka wa Fedha, 2020/2021, maombi ya ushauri wa kisheria **768** yalipokelewa na kufanyiwa kazi. Kati ya maombi hayo, maombi **165** yalihusu masuala ya utawala, **98** yalihusu masuala ya uchumi na **502** yalihusu masuala ya utoaji haki.

VIII. MAPITIO YA MIFUMO YA SHERIA MBALIMBALI

38. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea kuhakikisha kwamba sheria za nchi zinafanyiwa mapitio na maboresho ili ziendane na wakati kwa kuzingatia mabadiliko katika nyanja za kijami, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Katika kipindi husika, mifumo ifuatayo iliyofanyiwa mapitio; Mfumo wa Sheria Unaosimamia Uwakilishi wa Kisheria Mahakamani, Mfumo wa Sheria Unaosimamia Wazee wa Mahakama na Mfumo wa Sheria unaosimamia Utatuvi wa Migogoro ya Kazi. Mapendeleko yaliyomo katika taarifa hizi yamekusudia kuongeza kiwango cha wananchi kupata haki kwa wakati, uhakika na gharama nafuu. Aidha, Tume imeanza kufanya utafiti kuhusu Mfumo wa Sheria zinazosimamia Masoko ya Mazao ya Kilimo nchini. Utafiti huo unafanyika katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam, Mtwara, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Iringa na Njombe. Lengo la utafiti huo ni kubaini changamoto za Mfumo wa Masoko ya mazao ya kilimo Tanzania.

39. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria inaandaa taarifa mbili za tathmini ya utekelezaji wa sheria zinazohusu mifumo ya kutoa adhabu mbadala; na uboreshaji wa Sekta ya Utalii. Katika mfumo wa sheria za adhabu mbadala, sheria zinazofanyiwa tathmini ni pamoja na Sheria ya Magereza, Sura ya 58; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200; Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291; Sheria ya Bodi ya Msamaha, Sura ya 400 na Sheria ya Kikomo cha Adhabu, Sura ya 90. Madhumuni ya tathmini hii ni kubainisha kama sheria zilizopo zinaweza kutumika kupunguza msongamano magerezani na hivyo kupunguza gharama za kuendesha magereza.

40. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uboreshaji wa sekta ya utalii, sheria zilizofanyiwa tathmini ni pamoja na Sheria ya Utalii, Sura ya 65; Sheria ya Wanyamapori, Sura ya 283; Sheria ya Mbuga za Wanyama, Sura ya 282; Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Mamlaka ya Ngorongoro, Sura ya 284; na Sheria ya Malikale, Sura ya 333. Tathmini katika Sekta ya Utalii inalenga kubaini endapo Sheria zilizopo zinaweza kutumika kuongeza makusanyo ya mapato na utunzaji endelevu wa vivutio vya utalii. Vilevile, Tume imeendelea kutoa elimu ya sheria kwa umma kupitia vipindi vya radio, vipeperushi; maonesho ya wiki ya sheria, nane nane na mikutano mbalimbali kwa madhumuni ya kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala mbalimbali ya sheria.

IX. UHAKIKI WA MIKATABA MBALIMBALI INAYOIHUSU SERIKALI

41. Mheshimiwa Spika, kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara imeendelea kufanya majadiliano na upekuzi wa Mikataba mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Katika Mwaka wa Fedha, 2020/2021, Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa **713** na Hati za Makubaliano **46** zilifanyiwa upekuzi. Kati ya Mikataba hiyo, **168** ililhusu masuala ya uwekezaji, ujenzi na ukarabati wa majengo; **191** masuala ya ununuzi; **127** masuala ya utoaji wa huduma za jamii; **79** masuala ya uchumi na fedha; **75** masuala ya rasilimali na maliasili; na **73** masuala

ya Kimataifa. Kati ya mikataba iliyofanyiwa upekuzi, **365** ilithaminishwa katika sarafu mbalimbali ambapo **273** ilikuwa na thamani ya **Shilingi Trilioni 4.5**, mikataba **73** ilikuwa na thamani ya **Dola za Marekani 1,328,494,478.29** sawa na **Shilingi Trilioni 3.09** na mikataba **19** ilikuwa na thamani ya fedha ya Umoja wa Ulaya (Euro) **410,574,162.33**sawa na **Shilingi Trilioni 1.08**.

X. MASUALA YA HAKI ZA BINADAMU NA HAKI ZA WATU

42. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Wizara iliendelea kuimarisha mifumo ya kisera ya utekelezaji wa haki za binadamu na haki za watu nchini. Aidha, Wizara ilifanya majadiliano na wadau wa Serikali juu ya kuboresha mfumo wa uandaaji na uwasilishaji wa Taarifa za Nchi za Utekelezaji wa Mikataba zinazohusu haki za wanawake na haki za mtoto ambayo Serikali imeridhia. Vilevile, katika kipindi hicho, Wizara ilishiriki katika vikao vyta kikanda na kimataifa vyta haki za binadamu na haki za watu. Vikao hivyo, ni vyta 44 na 45 vyta Baraza la Haki za Binadamu viliyofanyika tarehe 30 Juni hadi 17 Julai, 2020, na tarehe 14 Septemba hadi 7 Oktoba, 2020. Wizara imeshiriki katika kikao cha 46 cha Baraza hilo kuanzia tarehe 22 Februari, 2021 na kumalizika tarehe 22 Machi, 2021. Katika mikutano hiyo, Wizara iliwasilisha taarifa ya Serikali kuhusu masuala ya kukuza, kulinda na kuheshimu haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

43. Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki kwenye Kikao cha 66 cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu, kilichofanyika tarehe 13 Julai hadi 07 Agosti, 2020; Kikao cha 67 kilichofanyika tarehe 13 Novemba hadi 03 Desemba, 2020 na Kikao cha 68 kilichoanza tarehe 14 Aprili,2021 na kinaendelea hadi tarehe 4 Mei, 2021. Katika vikao hivyo, Wizara iliwasilisha taarifa ya Serikali kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa haki za binadamu na haki za watu nchini. Kwa upande wa Kamisheni ya Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto, Wizara ilishiriki kwenye kikao cha 35 cha tarehe 31, Agosti hadi 8 Septemba, 2020 na kikao cha 36 cha tarehe 23 Novemba hadi 4 Desemba, 2020 ambapo taarifa za Serikali

kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Kulinda Haki na Ustawi wa Mtoto ziliwasilishwa.

44. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuelimisha watumishi wa Serikali kuhusu masuala ya haki za binadamu. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ilitoa elimu kwa watumishi wa Umma **111** wa Wizara na Taasis mbalimbali kwa lengo la kuongeza uelewa na kujenga uwezo kwa watumishi hao katika kutekeleza kazi zinazohusiana na kulinda na kukuza haki za binadamu. Mapendekezo hayo yaliyokubaliwa na Serikali chini ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mapitio katika Kipindi Maalum mwaka 2016 pamoja na mikataba ya haki za binadamu na haki za watu ambayo Serikali imeridhia. Aidha, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu yaliyofanya Desemba, 2020 ambapo watumishi wa sekta ya umma na sekta binafsi wapatao **209** walishiriki na kupewa elimu kuhusu haki za binadamu na haki za watu.

45. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Tume ilianza na malalamiko **2,361** na kupokea malalamiko mapya **354** na hivyo kufanya jumla ya malalamiko **2,715**. Hadi Machi, 2021, malalamiko **281** yamefanyiwa uchunguzi na kuhitimishwa na kubaki na malalamiko **2,434** ambayo yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi. Aidha, Tume ilifanya ziara za kimkakati katika mikoa **19** ya Tanzania Bara na mitano ya Zanzibar kwa lengo la kushughulikia malalamiko **574** ya muda mrefu ambapo kati ya hayo malalamiko **230** yalipatiwa ufumbuzi. Vilevile, Tume ilishughulikia malalamiko **96** yawatumishi kutoka Taasisi nane (8) za umma jijini Dodoma ambapo malalamiko **48** yalipatiwa ufumbuzi. Tume inaendelea kuboresha mfumo wa TEHAMA wa kushughulikia malalamiko pamoja na kuhuisha mfumo wa utunzaji kumbukumbu.

46. Mheshimiwa Spika, Tume imeendelea kuelimisha umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora na jinsi ya kutumia huduma zinazotolewa na Tume kupitia vyombo vya habari, mikutano, maadhimisho ya kitaifa na kimataifa, machapisho na warsha. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, nakala **1,900** za vipeperushi na machapisho yalisambazwa kwa wananchi na taasisi mbalimbali, vipindi **12** vya redio na **23** vya runinga vilirushwa kwa lengo la kuitangaza Tume na majukumu yake. Aidha, elimu zaidi imetolewa kupitia Vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa na Wilaya katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Morogoro, Dar es Salaam, Arusha, Tabora na Mwanza kwa Tanzania Bara na mikoa ya Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja na Kusini Unguja kwa upande wa Zanzibar. Vile vile, Tume imeendelea kutoa elimu kwa umma hususan kwa wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo vya ualimu ambapo jumla ya wanafunzi **1,750** na walimu **55** walijengewa uelewa wa masuala ya elimu ya haki za binadamu, utawala bora na wajibu wao kwa Taifa. Klabu **32** za haki za binadamu zilianzishwa na kufanya klabu zilizokwishaanzishwa hapa nchini hadi Machi, 2021 kufikia **254**.

47. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha demokrasia na haki za binadamu nchini, Tume imefanya uangalizi wa zoezi la Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, kuanzia hatua ya uboreshaji wa daftari la wapiga kura, mikutano ya kampeni, upigaji kura, kuhesabu na kujumlisha kura na utangazaji wa matokeo katika vituo **320** vya kupigia kura. Uangalizi huo ulihusisha mikoa saba (**7**) ya Tanzania Bara ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Lindi, Iringa, Arusha, Singida na Dodoma; na vituo **29** katika mikoa minne (**4**) ya Zanzibar ambayo ni Mjini Magharibi, Kusini Unguja, Kaskazini Unguja na Kusini Pemba. Kwa ujumla uchaguzi huo ulifanyika katika mazingira ya amani na utulivu.

48. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume imeendelea kuimarisha uzingatiwaji wa haki za binadamu na haki za watu katika maeneo ya vizuizi kwa mujibu wa Sheria za nchi na Mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Tume ilifanya ukaguzi katika magereza **18** na vituo vya Polisi **14** katika mikoa mitano (**5**) ya Tanzania

Bara. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Taarifa za ukaguzi na mapendekezo ya Tume zinafanyiwa kazi na Serikali kama Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sura 391 inavyoelekeza. Sambamba na hilo, Tume imekamilisha taarifa ya mwaka ya hali ya haki za binadamu ya 2019/20 na kuwasilishwa Serikalini. Aidha, Taarifa ya Tume kuhusu utendaji wa majukumu yake kulingana na Mkataba wa Afrika 2020 imekamilishwa na kuwasilishwa kwenye Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Taarifa hii inaeleza namna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kama Taasisi huru ya Serikali inavyotekeleza majukumu yake ya kutetea, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini.

XI. HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA)

a) Utoaji wa Huduma ya Msaada ya Kisheria

49. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuratibu jukumu la utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, iliendesha zoezi la ukaguzi kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria ili kujiridhisha na huduma wanazotoa. Aidha, Wizara iliratibu maandalizi na kushiriki maadhimisho ya wiki ya msaada wa kisheria yaliyofanyika kitaifa katika Mkoa wa Tanga ambapo wananchi **314,000** walipatiwa huduma ya msaada wa kisheria. Katika mikoa mingine idadi ya wananchi waliopatiwa huduma hiyo ni **1,455,566**. Kati ya hao, **529,079** walikuwa wanawake, **514,051** walikuwa wanaume na **412,436** walikuwa watoto. Vilevile, huduma ya msaada wa kisheria ilitolewa kwa wafungwa na mahabusi **8,442** katika magereza **11** na vituo vya polisi **26** katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Dodoma, Morogoro na Dar es salaam. Wizara pia ilishughulikia malalamiko **101** ya wananchi yaliyowasilishwa Wizarani katika kipindi husika.

50. Mheshimiwa Spika, Wizara imekubaliana na Mhimili wa Mahakama kuanzisha Madawati ya Msaada wa Kisheria katika Mahakama nchini. Lengo la kuanzishwa madawati

hayo ni kuwawezesha wananchi wenyе mashauri Mahakamani na wenyе kuhitaji msaada wa kisheria kupata huduma hiyo katika maeneo ya mahakama. Kufuatia makubaliano hayo, Wizara imeandaa andiko la namna ya kuanzisha Madawati hayo pamoja na Mwongozo wa kuyaendesha ambapo taratibu zinafanyika ili kuanza kwa utekelezaji.

b) Kuendesha Mafunzo ya Watoaji Huduma za Msaada wa Kisheria

51. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha, 2020/2021, Wizara iliendelea kuratibu jukumu la kutoa mafunzo ya msaada wa Kisheria ili kuhakikisha kwamba huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi, hususan wananchi wasio na uwezo wa kughamramia huduma za kisheria wanapata huduma hiyo bure na kwa wakati. Kwa sehemu kubwa, mafunzo hayo yanatolewa sambamba na maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa kisheria yaliyofanyika Novemba, 2020. Katika maadhimisho hayo yaliyofanyika katika mikoa yote Tanzania Bara, mafunzo yalitolewa kwa Wananchi na Taasisi zilizosajiliwa kutoa Huduma ya Msaada wa kisheria pamoja na viongozi mbalimbali wanaohusika na utatuzi wa migogoro katika jamii wakiwemo Wabunge, Kamati za Usalama, watendaji Kata na wajumbe wa Mabaraza ya Kata na vijiji. Sambamba na maadhimisho hayo Wizara iliendelea kuratibu vipindi vyaya elimu kwa umma kuhusu *Huduma za Msaada wa Kisheria* kuitia vyombo mbalimbali vyaya habari vikiwemo radio na televisheni. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliratibu mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria **89** katika Wilaya za Simanjiro, Kiteto na Karatu.

52. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma ya Msaada wa Kisheria inapatikana kwa makundi maalum hususan haki ya mtoto, Wizara katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, iliratibu mafunzo kwa Wasajili Wasaidizi wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria pamoja na Wasaidizi wa Kisheria kutoka katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa na Njombe. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuwajengea uwezo Wasajili Wasaidizi na Wasaidizi wa Kisheria katika kusimamia, kuratibu

na kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa watu wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za mawakili hususan watoto walio kwenye mgogoro na sheria na katika maeneo wanayoyasimamia kwenye Halmashauri zao. Jumla ya Wasajili Wasaidizi **27** na Wasaidizi wa Kisheria **20** walipewa mafunzo hayo. Kati ya Wasajili Wasaidizi **27** waliopata mafunzo hayo, Wanawake ni **22** na wanaume walikuwa watano **(5)**. Kwa upande wa Wasaidizi wa Kisheria 20 waliopata mafunzo, wanawake walikuwa wawili (2) na wanaume walikuwa **18**. Mafunzo haya ni utekelezaji wa kazi ambazo zipo kwenye Mkakati wa Pili wa Haki Mtoto wa miaka mitano ambaa dhumiuni la mkakati huo ni kuboresha mfumo wa haki mtoto nchini.

53. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha, 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania illkamilisha maandalizi ya Mtaala wa mafunzo ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria. Taasisi hiyo imepata kibali kutoka Baraza la Taifa ya Elimu ya Ufundı cha kutoa mafunzo husika kwa ngazi ya Astashahada. Mafunzo haya yanalenga kuimarisha huduma ya msaada wa kisheria kwa kuweka mizania ya ubora na kiwango sawa cha aina ya huduma za msaada wa kisheria, na hivyo kuongeza wigo wa usogezaji wa huduma za kisheria kwa wananchi na kuwawezesha kuifikia haki kwa wakati. Mafunzo hayo kwa ngazi ya Astashahada yanatarajiwa kuanza Septemba, 2021.

XII. MASUALA YA USAFIRISHAJI WA WAHALIFU KULETWA NCHINI AU KWENDA NJE ZA NCHI

54. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza jukumu lake la kimataifa kwa kushirikiana na mataifa mengine katika kupambana na kusimamia kurejeshwa kwa watuhumiwa wa uhalifu katika nchi walikofanya makosa. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ilipokea na kushughulikia maombi manane **(8)** ya kurejesha watuhumiwa wa makosa mbalimbali ya jinai walokimbilia nchini baada ya kutenda makosa kwenye nchi hizo. Kati ya maombi haya, maombi saba **(7)** yalishughulikiwa na moja **(1)** linaendelea kufanyiwa

kazi.Aidha, Wizara iliwasilisha katika mataifa mengine maombi matatu **(3)** ambapo moja **(1)** kati ya hayo limekamilika na mtuhumiwa kurejeshwa nchini kukabiliana na kosa lake na mawili **(2)** yanaendelea kufanyiwa kazi.

XIII. MASUALA YA KUSAIDIANA KATIKA MASUALA YA JINAI KIMATAIFA

55. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipokea jumla ya maombi manne **(4)** ya kusaidiana katika masuala ya jinai. Maombi hayo yalihusu upatikanaji wa nyaraka za ushahidi na kuwahoji mashahidi walioko nchini kwa kesi za jinai zinazoendelea katika mataifa mengine. Kati ya maombi hayo, ombi moja **(1)** limekamilika na maombi matatu **(3)** yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliwasilisha maombi matatu **(3)** ya upatikanaji wa nyaraka za ushahidi na kuwahoji mashahidi walipo nje ya nchi. Maombi hayo yanaendelea kufanyiwa kazi katika nchi hizo. Masuala ya ushirikiano wa kisheria na mataifa mengine katika masuala mbalimbali ya jinai.

XIV. USAJILI WA MATUKIO MUHIMU YA BINADAMU NA TAKWIMU PAMOJA NA MASUALA YA UDHAMINI

56. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini imeendelea kuimarisha shughuli za usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili ikiwa ni haki ya msingi ya utambuzi na upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi,2021 Wakala ulisajili vizazi **1,095,072**; vifo **24,945**; ndoa **36,411**; talaka **403** na hati za watoto wa kuasili²⁵. Aidha, Wakala uliandika na kuhifadhi wosia **87** na kusajili bodi za wadhamini **57**. Wakala uliendelea na utekelezaji wa mpango wa usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano katika Mikoa ya Tanga na Kilimanjaro ambapo jumla ya watoto **457,780** walisajiliwa na kupatiwa vyeti ambayo ni sawa na asilimia **78** ya lengo la usajili wa Watoto **584,658** katika mikoa hiyo. Usajili huu umeongeza kiwango cha usajili kitaifa kutoka asilimia **49.4** mwaka 2019 hadi kufikia asilimia **55** mwaka 2020. Katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma

za usajili, Mfumo wa Usajili kwa kutumia mtandao (e-huduma) umeendelea ambapo umewawezesha wananchi kupata huduma mbalimbali zikiwemo; maombi mapya ya vyeti nya vizazi na vifo, uhakiki wa vyeti nya vizazi na vifo na kubadili vyeti nya kuzaliwa na vifo. Katika husika, jumla ya maombi **118,245** yalipokelewa. Kati ya hayo, maombi **112,809** yalikuwa ni ya wanafunzi wanaoomba mikopo katika Bodi ya Elimu ya Juu na maombi **5,436** yalikuwa ni wadau wengine ambayo yalihakikiwa kuititia mfumo huu kwa lengo la kutambua uhalali wake.

57. Mheshimiwa Spika, katika kujenga uelewa kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini, elimu kwa umma kuititia vyombo mbalimbali nya habari imeendelea kutolewa ambapo makala **105** zilichapishwa kwenye magazeti na vipindi **272** nya mahojiano na matangazo vilifanyika katika redio na runinga mbalimbali. Aidha, habari **96** zilitolewa katika mitandao ya kijamii na vipeperushi **16,000** vinavyohusiana na huduma zinazotolewa na Wakala vilichapishwa na kusambazwa kwa wananchi kwa lengo la kutoa elimu, hamasa, gharama na maelekezo ya jinsi ya kupata huduma.

XV. UANGALIZI NA UFUAMILIAJI WA UTAJIRI ASILI NA MALIASILIA ZA NCHI

58. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria imepewa jukumu la kuratibu masuala ya uangalizi wa utajiri asili na maliasilia za Nchi kuititia Sheria za Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Utajiri asili na Maliasilia za Nchi, Sura ya 449 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri asili na Maliasilia za Nchi, Sura 450. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta iliendelea kutekeleza shughuli za kuweka mifumo na kutoa miongozo mbalimbali ili shughuli za uchimbaji, utafutaji, uvunaji na utumiaji wa utajiri asili na maliasilia za nchi zitekelezwe kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Miongozo na Mifumo hiyo ni pamoja na:-

- i. Mwongozo wa kuratibu Utekelezaji wa Sheria za Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Utajiri asili na Maliasilia za Nchi, na Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri asili na Maliasilia za Nchi, 2021;
- ii. Mwongozo wa usajili wa mikataba ya Utajiri asili na Maliasilia za Nchi, 2021; kwa lengo la kubaini idadi ya mikataba ilioingiwa kati ya Serikali na wawekezaji pamoja na kutambua maudhui ya mikataba husika;
- iii. Rasimu ya Kanuni za Utekelezaji wa sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Utajiri asili na Maliasilia za Nchi, Sura 449;
- iv. Mfumo wa ki-elektroniki wa uangalizi wa utajiri asili na maliasilia za Nchi

59. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria Sura ya 449 na Sura ya 450, ili kupima manufaa wanayoyapata wananchi wa maeneo yaliyo karibu na miradi inayohusika na shughuli za utajiri asili na maliasilia za nchi pamoja na Taifa kwa ujumla. Matokeo ya ufuatiliaji huo yalibainisha kuwa Watanzania wanashiriki katika nafasi ambazo hapo awali zilishikwa na wageni. Mfano katika mradi wa uchakataji wa gesi asilia uliopo katika kata ya Madimba Mkoani Mtwara kati ya wafanyakazi **62** walioajiriwa katika mradi huo wataalam kutoka nje ni wawilli (2) tu ambao wapo kwenye ratiba ya kukabidhi majukumu yao kwa Watanzania. Aidha, kupitia Mpango wa usambazaji wa gesi asilia majumbani nyumba 127 na taasisi 4 za mafunzo zimeshaunganishwa katika huduma ya mfumo wa usambazaji katika Mkoa wa Mtwara.

60. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kupitia Mikataba ili kubaini vifungu vyenye masharti hasi. Katika kipindi husika Wizara kwa kushirikiana na wadau ilipitia mikataba **18** ya watoa huduma katika Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa Ngorongoro ikiwemo mikataba ya ujenzi na ukarabati wa hoteli za Kitalii. Aidha, Wizara imeshiriki katika majadiliano ya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Mji wa Hoima (Uganda)

hadi Tanga ili kuhakikisha kwamba masuala ya utajiri asili na maliasilia za nchi yanazingatiwa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii imefanya mapitio ya vifungu vya Sheria ya Misitu Na.14 ya mwaka 2002 na kupendekeza marekebisho yanayohusu uwiano wa makosa na adhabu. Wizara kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mazingira migodini ilifanya ufuutiliaji katika Mikoa ya Shinyanga na Mara ili kubaini uzingatiwaji wa matakwa ya Sheria Sura ya 449, Sura ya 450 na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

61. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha na kuelimisha umma pamoja na viongozi mbalimbali wa Wizara na Taasisi kuhusu Sheria tajwa. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 mafunzo yalitolewa kwa Makatibu wakuu **11**, wakuu wa Taasisi **11**, Maafisa waandamizi **40** kutoka kwenye Wizara na Idara za Serikali pamoja na maafisa viungo **20** kutoka sekta zinazosimamia masuala ya utajiri asili na maliasilia za nchi. Mafunzo ya Sheria hizi yalitolewa pia kwa vyombo vya usalama katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Geita.

XVI. UENDELEZAJI WA RASILIMALI WATU

62. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia watumishi wake ili kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma. Wizara imendelea kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi waliokiuka maadili ya kazi kwa kutoa onyo, kushushwa vyeo na wengine kuachishwa kazi. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, watumishi wapya ni **594** katika Wizara na Taasisi; jumla ya watumishi **245** walithibitishwa kazini; watumishi **371** walipandishwa vyeo/kuteuliwa; Watumishi **874** walipata mafunzo; watumishi sita (**6**) walismamishwa kazi, **46** kuachishwa kazi, **18** walipewa onyo; watumishi **45** walihamia sehemu nyingine na watumishi **49** walihamia katika Wizara na Taasisi zake. **KIAMBATISHO D** kinaonesha mchanganuo wa maendeleo ya Watumishi katika Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

63. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuboresha utendaji wa kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilikagua utendaji wa Kamati za Maadili kwenye Mikoa sita **(6)** ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Mbeya na Iringa pamoja na Wilaya **11** za Kilwa Masoko, Lindi, Mtwara, Newala, Songea, Njombe, Wanging'ombe, Mbeya, Kyela, Iringa na Kilolo. Vilevile, Tume imeshiriki Maonesho ya Wiki ya Sheria kwa ajili ya kutoa elimu kwa Umma kuhusu Muundo na Majukumu ya Tume na Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama ambapo nakala **2,500** za vipeperushi zilisambazwa.

XVII. URATIBU WA MAFUNZO

a. Mafunzo ya Uongozi wa Mahakama

64. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, imeendelea kusimamia shughuli za taaluma ya Uongozi wa Mahakama. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Chuo kimedahili wanachuo **944** wa ngazi ya Astashahada na Stashahada ya Sheria ikilinganishwa na wanachuo **872** wa mwaka wa masomo 2019/20. Aidha, Chuo chini ya ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto - UNICEFkimeandaa Taarifa ya Tathmini ya Mafunzo ya Uendeshaji wa Mashauri ya mtoto. Tathmini hiyo imefanyika kwa wadau wa masuala ya mtoto waliopatiwa mafunzo kwenye Kanda zote za Mahakama Kuu Tanzania Bara. Lengo la Tathmini hiyo ni kuona mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizopo na namna ya kuzitatuwa.

65. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania kimeendesha mafunzo ya uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi. Mafunzo hayo yalihuisha Majaji **15** wa Mahakama ya Rufani, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Majaji **75** wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Wasajili na Naibu Wasajili **34**, Mahakimu Wakazi **141** wa Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya, Wasaidizi wa Sheria wa Majaji **84** pamoja na Warajisi watatu **(3)** kutoka Mahakama Kuu ya Zanzibar. Aidha, Chuo kwa kushirikiana na Mahakama ya

Tanzania kiliratibu na kuendesha mafunzo elekezi kwa mahakimu wapya **183** wa Mahakama za mwanzo. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wa uendeshaji wa mashauri katika Mahakama za Mwanzo, miiko, maadili na utendaji kazi katika utumishi wa umma. Vilevile, Chuo kiliendesha mafunzo ya namna bora ya uendeshaji wa mashauri ya madai na jinai kwa Majaji na Mahakimu **28** wa Mahakama ya Zanzibar.

66. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kwa ufadhilli wa Shirika la **Pact Tanzania** kimeendesha mafunzo kwa wadau **212** wanaohusika na mashauri ya mtoto. Wadau hao ni Mahakimu, Mawakili wa Serikali, Waendesha Mashtaka na Maafisa Ustawi wa Jamii. Mafunzo hayo yalitolewa pia kwa Majaji **63** wa Mahakama Kuu na Majaji wawili (**2**) wa Mahakama ya Rufani. Mafunzo hayo yalifanyika katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Ruvuma na wilaya ya Lushoto. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa kuendesha na kusikiliza mashauri yanayomhusu mtoto. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo kwa Madalali wa Mahakama **38** na Wasambaza Nyaraka za Mahakama **19** ili kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa amri za Mahakama na kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati. Vilevile, Chuo kwa kushirikiana na wadau wengine wa Sheria kilitoa elimu ya sheria kwa wanajamii **100** katika Wiki ya Msaada wa Kisheria iliyofanyika Novemba, 2020 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Wiki ya Sheria iliyofanyika Januari, 2021. Vilevile Chuo kiliendesha Mafunzo ya Usuluhihi na Mbinu za Usuluhihi kwa wajumbe sita (**6**) wa Menejimenti ya Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati ya Zanzibar. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wa namna bora ya kutatua migogoro kwa njia mbadala ya maridhiano.

67. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Chuo kwa ufadhilli wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani-FAO kimetoa ushauri wa kitaalamu wa kuandaa mwongozo wa kuendesha mafunzo na kutoa mafunzo kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa njia mbadala. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wanasheria wa halmashauri, wenyeviti wa wilaya, wenyeviti na makatibu wa mabaraza

ya ardhi, watendaji wa kata, watendaji wa vijiji na asasi za kijamii kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi. Mafunzo hayo yalifanyika katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi Mkoani Morogoro ambapo washiriki **92** walinufaika. Vilevile, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji **16** na Mabaraza ya Kata **12** yaliyopatiwa mafunzo yalifanyiwa tathmini. Matokeo ya tathmini yalionesha kuwa mafunzo hayo yalichangia kuboresha utendaji kazi katika utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa njia mbadala.

b. Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo

68. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa wanasheria. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021 Taasisi imedahili wanafunzi **1,324** sawa na **asilimia 88.3** ya malengo ya udahili wa wanafunzi **1,500**. Aidha, Taasisi imetoa wahitim **174** wanaostahili kusajiliwa kuwa mawakili na kufanya idadi ya wahitim waliopata mafunzo kupitia Taasisi hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2007 kufikia **6,990**.

69. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania kupitia ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa - UNDP, imeandaa mwongozo wa kutoa msaada wa kisheria kwa lengo la kuwaongoza watoa msaada wa kisheria kutoa huduma bora kwa kufuata sheria na taratibu zinazoongoza utoaji wa huduma hiyo. Mwongozo huo utawawezesha watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za kisheria kupata haki. Vilevile, Taasisi kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto - UNICEF, imeandaa mwongozo wa kutoa msaada wa kisheria kwa watoto ambaa umezingatia mahitaji ya msingi ya mtoto kabla na wakati wa kufungua na kusikilizwa kwa shauri linalomuhusu. Mwongozo huo umezingatia kwamba, mtoto ana mahitaji ya msingi ya kisheria ambayo ni tofauti na ya watu wazima, na yanatakiwa yazingatiwe wakati wote wa utoaji wa msaada wa kisheria.

E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

70. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara iliendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni;

a) Mradi wa Kuimarisha Ufikiwaji Haki na Haki za Binadamu (Strengthening Access to Justice and Human Rights Projection in Tanzania)

Mradi huu unalenga kusawanisha mifumo ya Utoaji wa Haki na masuala ya ulinzi wa Haki za binadamu nchini, hususan kwa Makundi Maalum, wakiwemo; wanawake, watoto, wazee, na watu wenye ulemavu. Katika mwaka wa fedha wa 2020/21, kiasi cha **Shilingi 2,835,212,000.00**, fedha za nje, zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi za Kuandaa Mpango Kazi wa Pili wa Taifa wa Haki za Binadamu na Kuimarisha mfumo wa Ufuatilajji na Tathmini ya Utekelezaji wa Masuala ya kuhifadhi, kulinda na maendeleo ya Haki za Binadamu.

Kupitia mradi huu Wizara imeendelea kukamilisha Mpango Kazi wa Pili wa Taifa wa Haki za Binadamu wa miaka mitano (2021/22 hadi 2025/2026). Lengo la Mpango Kazi huu ni kutatua changamoto zinazotukabili kama Taifa katika kushughulika na masuala ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ili kuboresha usimamizi na uratibu wa masuala hayo hapa nchini. Hatua iliyofikiwa ni kuwashirikisha wadau katika pande zote mbili za Muungano ili waweze kutoa maoni. Aidha, tarehe 16 Machi, 2021 Wizara ilipokea maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambayo yatazingatiwa ipasavyo kwenye Mpango Kazi huo utakaowasilishwa Serikalini kwa ajili ya kuidhinishwa.

b) Mradi wa Kujenga Mpango endelevu wa Kupambana na Rushwa (Building Sustainable Anti-Corruption Action in Tanzania-BSAAT).

Mradi huu unalenga kuondoa mianya ya rushwa katika Mifumo ya kitaasisi nayounda mfumo wa Haki-Jinai ambayo ni kikwazo kwa wananchi katika kupata haki na kupiga vita

dhidi ya Umasikini. Katika mwaka wa fedha wa 2020/21, Mradi huu ilitengewa **Shilingi 730,000,000.00** fedha za nje, ili kutekeleza kazi za; Kuandaa na kuanza kutekeleza programu ya Maboresho ya Mfumo wa haki Jinai Nchini, na; Kufanya mapitio ya sheria zinazosimamia mfumo wa haki jinai na kupendekeza marekebisho ili kuimarisha mfumo wa Haki Jinai ulipo kwa hapa nchini. Hadi Machi, 2021 kiasi cha **Shilingi 112,549,197.02** fedha za nje; kilitumika kutekeleza kazi zifuatazo; Kuandaa Andiko la Mapendekezo kuhusu Programu ya Maboresho ya Haki Jinai yanayobainisha maboresho kwenye mnyororo wa Haki Jinai katika hatua za: kubaini uhalifu unapotokea; kuzuia uhalifu; taratibu za ukamataji wa wahalifu; upelelezi wa makosa ya jinai; uendeshwaji na usikilizwaji wa mashauri mahakamani; utaratibu wa utoaji wa adhabu na urekebishaji wahalifu, ufuatiliaji wa mienendo ya wale wanaokamilisha adhabu zao au wanaaoachiwa kwa sababu mbalimbali; na Kuandaa Kanuni za kutekeleza Sheria ya kuwalinda Mashahidi na Watoa Taarifa ya Mwaka 2015.

b) Mradi wa e-Justice

Mradi huu unalenga kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika Sekta ya Sheria na kusawanisha mifumo ya taasisi ya utoaji huduma za kisheria kwa njia za kielektroniki ili kuongeza ufanisi kwa kupunguza ghamama na kutoa huduma hizo kwa wakati. Katika mwaka wa fedha wa 2020/21, Mradi huu ilitengewa **Shilingi 1,000,000,000.00** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi mbali za kuyafikia malengo hayo. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, jumla ya **Shilingi 518,521,573.00**, zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatavyo: Kusanifu na kujenga mfumo wa kielektroniki wa utendaji kazi zinazohusu utoaji Haki; Kununua vifaa vya kuwezesha mfumo wa mawasiliano ya kielektroniki ilikuwezesha huduma ya utoaji haki kwa njia ya mtandao; Kufunga mtandao kiwambo (LAN & Teleconference systems) ili kuwezesha mawasiliano ya kielektroniki na kurahisisha huduma za utoaji haki; Kufunga mfumo wa umeme wa dharura kwenye mtandao wa wizara; Kusanifu na kuanza ujenzi wa Dirisha Moja la Taarifa na

Takwimu kwenye Sekta ya Sheria (Justice Sector Dashboard); na Ununuzi wa samani za Ofisi.

c) Mradi wa kuboresha Uwajibikaji wa Kitaasisi katika kupambana na Rushwa na kuongeza Wigo wa Kuifikia Haki (Improving Accountability through fighting Corruption and Increased Access to Justice - IMPACT)

Mradi huu unalenga kuongeza wigo na kumarisha mazingira ya wananchi kuifikia haki hususan kwa makundi maalum ikiwemo wanawake, watoto, wenye walemavu na wazee pamoja na kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa. Kiasi cha **Shillingi 1,349,840,744.75** fedha za nje zilitengwa kwa mwaka wa fedha wa 2020/21, kwa ajili ya kazi za: Kuimarisha huduma ya Msaada wa kisheria nchini; na; kuandaa mitaala ya elimu na mbinu za utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria, na; kujenga na kutekeleza mfumo wa Ufuatillaji na Tathmini ya Utoaji huduma ya Msaada wa kisheria nchini. Hadi Machi, 2021 kazi zifuatazo zilitekelezwa; Kuratibu utoaji wa mafunzo kwa Watoa huduma ya msaada wa kisheria kuhusu huduma ya msaada na kutoa huduma za kisheria kwa wananchi wenye kuhitaji; Kuwezesha kufanyika kwa bodi ya kitaifa ya ushauri wa utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria; Kuwezesha ushiriki wa Wizara kwenye mkutano wa kikanda wa masuala ya msaada wa kisheria.

d) Mradi wa Unicef Support to Multisectoral

Mradi huu unalenga kufanikisha Mipango ya Serikali inayohusu ulinzi na maendeleo ya mtoto nchini. Shughuli zinazohusika na mradi huu ni pamoja na kuimarisha kazi za jukwaa la Haki Mtoto (Child Justice Forum) pamoja na kuimarisha shughuli za usajili wa matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu, hususan usajili wa vizazi kwa watoto. Kiasi cha **Shillingi 2,605,338,000.00** kilitengwa kwa mwaka wa fedha wa 2020/21, kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo; Kuandaa Mpango Mkakati wa Pili wa Miaka Mitano wa Haki Mtoto 2021/22- 2025/26, na; Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa usajili wa Vizazi vya Watoto wa Umri wa chini ya Miaka Mitano. Katika kipindi cha Julai,2020 hadi Machi,2021 jumla

ya **Shilingi 3,310,268,000.00**, zilipokelewa na Wizara na zilifanikisha kutekelezwa majukumu ya; kukamilisha na kuzindua Mpango Mkakati wa Pili wa Haki Mtoto (2020/2021 – 2024/2025) ambao, pamoja na masuala mengine, utazingatia kukabiliana na unyanyasaji dhidi ya watoto; na kusajili Vizazi **44,9726** katika Mikoa ya Tanga na Kilimanjaro.

e) Miradi ya Ujenzi ya Miundombinu ya Mahakama

Jumla ya fedha, kiasi cha **Shillingi 69,875,000,000.00** zilitengwa kwa mwaka wa fedha wa 2020/21, kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa miradi hii. Kati ya fedha hizi **Shilingi 39,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 30,875,000,000.00** ni fedha za nje. Fedha zilizopokelewa hadi Machi, 2021 ni **Shilingi 23,547,403,186.40** fedha za ndani na **Shilingi 21,079,719,869.75**. Serikali imeendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu ya utoaji haki na huduma zinazotolewa kwa kukamilisha miradi ya ukarabati wa Mahakama Kuu Sumbawanga; ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi mbili (**2**) katika mikoa ya Simiyu na Njombe; Kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama za Wilaya nne (**4**) za Kasulu, Makete, Longido na Wanging'ombe; Kukamilika kwa Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo (**6**); za Ngerengere (Morogoro), Mtae (Lushoto), Msanzi, Laela na Mtowisa (Sumbawanga) na Kibaigwa (Kongwa); na kukamilika kwa ujenzi wa Nyumba za Mahakimu Loliondo na ujenzi wa Jengo la Kuhifadhi Kumbukumbu, Tanga.

Mahakama pia imeendelea kutekeleza miradi ifuatayo: ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Mahakama sita (**6**) katika mikoa ya Dodoma, Arusha, Mwanza, Morogoro na Dar es salaam katika Wilaya za Temeke na Kinondoni; ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi tatu (**3**) katika mikoa ya Lindi, Katavi na Songwe; ujenzi wa Mahakama **13** za Wilaya za Sikunge, Kilindi, Rungwe, Ludewa, Bunda, Chemba, Bahi, Same, Mwanga, Ngara, Tandahimba, Namtumbo na Nanyumbu; kuendelea na ujenzi wa Mahakama nane (**8**) za mwanzo ambazo ni; Mlimba na Mang'ula (Morogoro), Kabanga (Ngara), Hydom (Mbulu), Kimbe (Kilindi), Chanika (Ilala), Nyakibimbili (Bukoba) na Matiri (Mbinga); na kuendelea na ujenzi wa Mahakama

nyingine mpya za Wilaya **25** katika maeneo ambayo hayana Mahakama za Wilaya. Vilevile, Mahakama imeendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama Jijini Dodoma ambalo lipo katika hatua za ujenzi wa boma (main structure). Miradi ya Ujenzi wa majengo ya Mahakama imeoneshwa kwenye **KIAMBATISHO E.**

f) Miradi ya Kuimarisha Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Utoaji wa Huduma za Kimahakama

71. Mheshimiwa Spika, Mahakama imeendelea kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa huduma. Kwa kutumia TEHAMA, Mahakama imeanzisha mifumo na kufanya maboresho mbalimbali ikiwemo Mfumo wa kielektroniki wa usimamizi na uendeshaji wa mashauri; mfumo wa kurekodi mwenendo wa mashauri; Mfumo wa maktaba mtandao; Mfumo wa kuratibu Mawakili na Mfumo wa usikilizwaji wa mashauri kwa njia ya mtandao (Video Conferencing). Matumizi ya TEHAMA yameongeza tija katika usikilizwaji wa mashauri mahakamani na utoaji wa haki nchini ambapo hadi Machi, 2021, jumla ya Mashauri **19,855** yamesikilizwa kwa njia ya mtandao. Zoezi la uboreshwaji wa Mifumo ni endelevu ili kuwezesha shughuli zote za Mahakama kutumia mifumo ya kielektroniki.

72. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara imeendelea kujenga mifumo ya TEHAMA ili kuboresha mifumo yake ya utoaji huduma za sheria. Wizara ipo katika hatua za mwisho za kujenga mifumo ifuatayo; Mfumo wa kushughulikia usajili wa malalamiko yanayowasilishwa wizarani kutoka kwa wadau mbalimbali; Mfumo wa kushughulikia usafirisahi wa watuhumiwa wa uhalifu kwenda nje na kuja ndani ya nchi; Mfumo wa kushughulikia vibali vya Waziri vya kuongeza muda wa kuwasilisha kesi mahakamani; mfumo wa kushughulikia menejimetu ya amri za kuwachia wahalifu wengine matatizo ya afya ya akili; mfumo wa kushughulikia masuala ya huduma ya msaada wa kisheria na mfumo wa dirisha moja la ubadilishanaji wa taarifa katika sekta ya sheria ambao ujenzi wake unakamilishwa kuititia Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika- Dar es Salaamu.

E. UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA MWAKA 2015 HADI 2020

73. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha kwamba inawajibika ipasavyo kwa wananchi kuititia utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ahadi na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa. Miongoni mwa ahadi hizo ni pamoja na kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma; kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na kuendeleza utawala wa sheria; na kuimarisha mfumo wa utoaji haki. Kulingana na Maelekezo hayo, Wizara inawajibika kutekeleza maeneo yafuatayo:

a) Kuendeleza Mapambano Dhidi ya Rushwa na Ubadhirifu wa Mali ya Umma

74. Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma yameendelea kuimarishwa, ambapo, mashauri sita **(6)** yalifunguliwa kwenye Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi na kufikisha mashauri **21** yaliyosajiliwa katika Mahakama hiyo. Hadi Machi, 2021 mashauri matano **(5)** yamehitimishwa na mengine **16** yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa.

b) Kukuza, Kulinda na Kuhifadhi Haki za Binadamu na Kuendeleza Utawala wa Sheria

75. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutekeleza shughuli za kulinda, kukuza na kuendeleza haki za binadamu na haki za watu nchini kwa mujibu wa matakwa ya Katiba, Sheria zilizopo na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa iliyordhiwa na nchi yetu. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kuelimisha watumishi wa Serikali kuhusu masuala ya haki za binadamu na watu, kutoa elimu kwa watumishi wa umma; kuandaa na kuwasilisha taarifa, pamoja na kushiriki kwenye vikao vya kikanda na kimataifa vya haki za binadamu. Aidha, katika kushirikiana na vyombo vya kimataifa vya haki za binadamu, Wizara inaendelea kuandaa taarifa ya tatu **(3)** ya nchi chini

ya mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mapitio katika Kipindi Maalum iliyopangwa kuwasilishwa kwenye Baraza la Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, Geneva Uswisi tarehe 9 Agosti, 2021.

c) Kuimarisha Mifumo ya Utoaji Haki

76. Mheshimiwa Spika, Wizara, kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutenganisha Mashtaka na Shughuli za Upelelezi kwa kusogeza huduma za mashtaka karibu na wananchi ili kurahisisha shughuli za utoaji Haki. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilifungua ofisi mpya moja (1) kwa ngazi ya mkoa na tano (5) kwa ngazi ya Wilaya.

77. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kutoa elimu kwa Serikali na Taasisi zake kuhusu namna ya kuzuia au kujiepusha kuzalisha kesi zisizokuwa na ulazima wa kufikishwa mahakamani; kuhakikisha misingi ya Demokrasia na Utawala Bora inazingatiwa katika uendeshaji mashauri; na kufanya tathmini ya kina ili kubaini vyanzo vya mashauri yanayoihu Serikali na namna bora ya kuyafanya kazi.

78. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeimarisha mfumo wa TEHAMA wa kupokea na kushughulikia malalamiko dhidi ya uvunjifu wa haki za binadamu. Maboresho hayo yamewezesha wananchi kuwasilisha na kupata mrejesho wa malalamiko yao kwa kubonyeza namba *152*00# kwenye simu ya kiganjani na kisha kufuata maelekezo. Aidha, ili kuimarisha utendaji kazi na kutoa huduma yenye mwitikio chanya kwa wananchi, Tume imekamilisha Mkakati wa Kushughulikia Malalamiko na inaendelea kuutumia katika kushughulikia malalamiko ya wananchi.

G. MWENENDO WA BAJETI NA FEDHA ZILIZOPOKELEWA NA WIZARA NA TAASISI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

79. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 12,634,533,000** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo ni pamoja na ada ya watoa huduma za msaada wa kisheria; na ada za kusajili mashauri, ada za usaliji wa matukio muhimu ya binadamu, ada za udhamini na uflisi, ada za wanafunzi, ada za mawakili; na faini zinazotokana na mashauri mbalimbali pamoja na pango la ofisi. Katika Kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Wizara na Taasisi ilikusanya jumla ya **Shilingi 5,641,594,065.50** sawa asilimia **44.7** ya lengo la makukusanyo yaliyopangwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo kwa kila fungu umefafanuliwa zaidi katika **KIAMBATISHO F** cha hotuba ya Wizara.

80. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi ilidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 73,684,796,059** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya maendeleo. Kati ya hizo **Shilingi 25,614,416,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi, **Shilingi 34,859,640,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 13,219,740,059** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo jumla ya **Shilingi 4,433,200,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 8,777,540,000** fedha za nje.

81. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 46,800,583,824.55** sawa na **asilimia 63.50** ya **Shilingi 73,684,796,059** zilizoidhinishiwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kati ya hizo **Shilingi 13,452,199,948** ni mishahara na **Shilingi 25,355,356,845** ni matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 1,320,677,335** ambazo zinajumuisha **Shilingi 518,521,573** fedha za ndani na **Shilingi 802,155,762** ni fedha za nje. Muhtasari wa mchanganuo wa Bajeti iliyoidhinishiwa na kiasi cha fedha zilizopokelewa na Wizara na Taasisi hadi Machi, 2021 umeoneshwa katika **KIAMBATISHO G.**

82. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mfuko wa Mahakama hadi Machi, 2021 jumla ya **Shilingi 131,864,142,384.63** zilipokelewa sawa na **asilimia 74.74** ya kiasi cha **Shilingi 176,437,977,000** zilizoidhinishwa kwa mwaka wa Fedha 2020/2021. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa **Shilingi 36,867,592,537.34** ni mishahara, **Shilingi 39,866,055,820.15** ni Matumizi Mengineyo, **Shilingi 29,241,889,475.54** ni fedha za Maendeleo za Ndani na **Shilingi 24,455,444,551.59** ni fedha za Maendeleo za Nje. Mchanganuo wa bajeti na fedha zilizopokelewa na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 umeonyeshwa kwenye **KIAMBATISHO H** cha Hotuba hii.

H. MAFANIKIO

83. Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 ni pamoja na: kuendelea kuwa na amani na utulivu katika nchi yetu kwa kuzingatia Katiba na Sheria zetu; matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mifumo yote ya uandishi wa nyaraka za kisheria na utoaji haki, kuboreshwa na kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za kimahakama kutokana na miradi inayoendelea kutekelezwa ya ujenzi wa mahakama katika ngazi zote hapa nchi; kuongezeka kwa kiwango cha usajili wa matukio muhimu ya binadamu kutokana na mifumo kuendelea kuimarika; kuimarika kwa mfumo wa ushughulikiaji wa mashauri ya madai na usuluhishi; kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki; kupunguza gharama za usikilizwaji wa mashauri, upatikanaji haki kwa wakati; kuimarika kwa utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria; na kuokolewa kwa fedha na mali ambazo Serikali au wananchi wangepoteza kutokana na kutekeleza mfumo wa haki jinai na madai.

I. CHANGAMOTO

84. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu, Wizara na Taasisi inazozisimamia imeendelea kukabiliana na changamoto ambazo ni pamoja na; Wanasheria walio wengi wanaomaliza

mafunko ya sheria kwa vitendo na kukubaliwa kuwa Mawakili, kukosa ajira ambapo awali walijiriwa kwenye Taasisi za umma na wengine kuwa Mawakili wa kujitegemea; kuchelewa kwa ufungaji wa mirathi kutokana na baadhi ya wasimamizi wa mirathi kutotekeleza wajibu wao pamoja na kuwepo kwa migogoro baina ya wanufaika wa mirathi, mwamko mdogo mionganoni mwa wananchi kuhusu kuandika na kuhifadhi wosia; Uelewa mdogo kwa wananchi katika kudai haki na kutekeleza wajibu wao; Ushirikiano mdogo wa wananchi katika kutoa taarifa za uhalifu wa makosa ya jinai na kutoa ushahidi mbele ya vyombo vyaa utoaji haki; na Baadhi ya Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama katika ngazi ya Mikoa na Wilaya kutotekeleza majukumu kwa kuzingatia misingi ya Sheria, Kanuni na Taratibu.

J. MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO

85. Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, Wizara iliendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana nazo na kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mfumo imara wa kikatiba na kisheria muda wote ili kufanikisha mipango ya maendeleo ya Taifa. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarissha matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma za kisheria na utoaji haki, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Usajili Ufilisi na udhamini kuendelea kujenga uelewa kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuandika wosia na kuweka mifumo ya kisera ambayo itaondoa changamoto za usimamizi wa mirathi; kuendelea kutoa elimu kwa wananchi na wadau mbalimbali kuhusu haki na wajibu wao kwa kuzingatia Sheria zilizopo; na Wizara kupitia Programu ya Maboresho ya Sekta Ndogo ya Haki Jinai, kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wananchi kushirikiana na Serikali na vyombo vyake katika kuzuia uhalifu kwa kutoa taarifa za uhalifu pale unapojitokeza na pia kutoa ushahidi mbele ya vyombo vyaa utoaji haki; na Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Mawakili Tanganyika, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, Vitivo vyaa Sheria kwenye Vyuo Vikuu hapa nchini na wadau wengine kuweka Programu ya kuwajengea uwezo Mawakili watarajiwa ili waweze kuelewa na kuzitumia fursa za ajira mbalimbali

zilizopo; na kuandaa na kusambaza miongozo ya uendeshaji wa Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama katika ngazi za Mikoa na Wilaya.

86. Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana ni juhudzi za pamoja kati ya Wizara, Idara, Taasisi na wadau wa Sekta ya Sheria wakiwemo washirika wa maendeleo. Hivyo, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano mzuri uliopo kati yetu na Washirika wa Maendeleo ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto, Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake, Umoja wa Ulaya, Pact Tanzania- Kizazi Kipyä, Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza, Shirika la Chakula na Kilimo Dunia pamoja na wadau wengine ikiwemo kampuni ya simu ya TIGO. Napenda niwahakikishie kuwa, Wizara inatambua na kuthamini uhusiano mzuri uliopo kati ya Serikali na wadau hawa, na tutahakikisha kuwa ushirikiano huo unaimarishwa kwa maendeleo ya sekta ya sheria na taifa kwa ujumla.

87. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya uwaziri. Hakika, ni kutokana na ushirikiano huo nimeweza kusimama leo hii mbele ya Bunge lako kueleza mafanikio, mipango na mikakati tuliyonayo katika kuwahudumia wananchi wetu. Hivyo, kipekee nimshukuru Mhe. Prof. Ibrahim Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania; Mhe. Prof. Adelardus Lubango Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb) Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Prof. Sifuni Ernest Mchome, Katibu Mkuu; Bw. Amon Anastas Mpanju, Naibu Katibu Mkuu; Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania; Bw. Mathias Bazirinkangu Kabunduguru Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Mhe. Wilbert Martin Chuma, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania; Bw. Biswalo Eutropius Kachele Mganga, Mkurugenzi wa Mashtaka; Bw. Gabriel Pascal Malata, Wakili Mkuu wa Serikali; Mhe. Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani January Henry Msoffe, Mwenyekiti wa

Tume ya Kurekebisha Sheria; Bw. Casmir Sumba Kyuki, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Mhe. Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania Mathew Mhina Mwaimu, Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Bw. Nabor Baltazar Assey, Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Bibi Emmy Kalomba Hudson, Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini; Mhe. Jaji Dkt. Benhajj Shaaban Masoud Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania; Mhe. Jaji Dkt. Paul Faustin Kihwelo, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Watendaji Wakuu, Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Aidha nawashukuru familia yangu ikiwa ni pamoja na mke wangu na watoto kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kunivumilia na kutia moyo wakati ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya kultumika Taifa.

K. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

88. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kisera katika sekta ya sheria ikiwa ni pamoja na kuratibu masuala yanayotekelawa na taasisi za Wizara kwa lengo la kutekeleza Dhima ya Wizara ili kuifikia Dira ya Wizara iliyowekwa. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara na Taasisi zimeainisha vipaumbele muhimu kama ifuatavyo: -

(i) Vipaumbele vya Wizara na Taasisi

Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria

- i. Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya kikatiba, Demokrasia na utawala wa sheria;
- ii. Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Huduma ya Msaada wa Kisheria;
- iii. Kuhuisha sheria mbalimbali;

- iv. Kutoa miongozo kuhusu matumizi ya Kiswahili katika shughuli za mfumo wa nyaraka za kisheria na utoaji haki;
- v. Kuboresha mfumo wa haki jinai nchini na kuhimiza utoaji huduma hiyo kwa njia ya TEHAMA;
- vi. Kujenga uwezo wa usimamizi wa utekelazaji wa adhabu mbadala kwa maafisa husika (ustawi wa jamii, Mahakama, Afya ya akili) na kutoa elimu ya umuhimu wa matumizi ya adhabu mbadala kwa maafisa wa Mahakama;
- vii. Kuandaa Mpango wa Kutenganisha shughuli za Upelelezi na Mashtaka;
- viii. Kuratibu na kusimamizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi;
- ix. Kuendelea kufanya vikao vya mara kwa mara na wadau vya kubainisha changamoto za utoaji haki na njia ya kukabiliana nazo;
- ix. Kuandaa Programu ya Miaka mitano ya sheria;
- x. Kuratibu maboresho ya mwongozo na utaratibu kuhusu Itifaki na Mikataba ya Kimataifa na Kikanda.

a. Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamsini

- i. Kuimarisha Usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu;
- ii. Kuboresha mazingira wezeshi ya biashara kwa kuratibu upatikanaji wa sheria mahususi ya ufilisi na kuleta usimamizi wa ufilisi wenye tija.
- iii. Kuimarisha usimamizi na utoaji wa elimu ya mirathi, udhamini pamoja kuhamasisha uandishi na uhifadhi wa wosia.
- iv. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utoaji wa huduma, ubadilishanaji taarifa na usimamizi wa ukusanyaji maduhuli.

b. Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo

- i. Kukamilisha taarifa ya utekelezaji wa Sheria iliyoanzisha Taasisi ya uanasheria kwa vitendo;
- ii. Kuboresha rasilimali watu;
- iii. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya taasisi; na
- iv. Kuboresha matumizi ya TEHAMA ili kurahisisha utoaji wa huduma.

Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama

- i. Kuwezesha vikao vya Kisheria vya Tume na Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama za Mikoa na Wilaya;
- ii. Kuimarishe Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama ya Mikoa na Wilaya;
- iii. Ujazaji wa nafasi za ajira na uteuzi katika Mahakama;
- iv. Kuboresha mazingira ya kazi na kuwajengaa uwezo watumishi wa Tume.

Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

- i. Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika mikoa ya Mbeya na Arusha;
- ii. Kufanya mapitio ya Sheria, Uandishi wa Sheria na ufasiri wa sheria;
- iii. Kufanya majadiliano na mapitio ya Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa;
- iv. Utoaji wa ushauri wa Kisheria kwa Serikali na taasisi zake; na
- v. Kuimarishe Mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa ushauri wa kisheria.

Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

- i. Kuratibu, kusimamia na kuendesha Mashauri ya Madai na Usuluhishi kwa niaba ya Serikali na Taasisi zake;
- ii. Kuanzisha ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Dodoma
- iii. Kuimarisha ofisi za mikoa;
- iv. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuboresha mfumo wa usimamizi wa Mashauri na udhibiti wa ubora; na
- v. Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi pamoja na maendeleo ya rasilmali watu.

Fungu 35: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

- i. Kuratibu upeletelezi unaofanywa na vyombo vyta upeletelezi na kuendesha mashtaka;
- ii. Utenganishaji wa shughuli za upeletelezi na mashtaka kwa kufungua Ofisi za Wilaya Tano (5);
- iii. Kuimarisha mfumo na shughuli za utaifishaji na urejeshaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu.
- iv. Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu Dodoma.

Fungu 40: Mfuko wa Mahakama

- i. Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (Backlog);
- ii. Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma;
- iii. Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;

- iv. Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali ikiwemo jengo la Makao Makuu Dodoma;
- v. Kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu, ikiwa ni pamoja na mafunzo, na nidhamu ya watumishi; na
- vi. Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki.

Chuo cha Uongozi wa Mahakama – Lushoto

- i. Kuboresha mitaala ya Stashahada na Astashahada ya Sheria;
- ii. Kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi ya Stashahada na Astashahada ya sheria kulingana na uwezo wa Chuo;
- iii. Kuanzisha Programu Mpya katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada;
- iv. Kuimarisha miundombinu na kukarabati majengo ya Chuo;
- v. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA iliyopo na kujenga mifumo mingine mipyaa; na
- vi. Kuimarisha huduma za Utafiti na utoaji ushauri wa kitaalamu.

Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

- i. Kuelimisha umma juu ya masuala ya haki za binadamu na utawala bora;
- ii. Kufanya uchunguzi wa malalamiko na kufuatilia mapendekezo ya Tume;
- iii. Kufanya utafiti kuhusu uvunjifu wa Haki za Binadamu na ukiukwaji wa Misingi ya Utawala Bora;

- iv. Kukagua sehemu wanamozuiliwa watu;
- v. Kuimarisha mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi kwenye eneo la Haki za binadamu na misingi ya Utawala Bora; na
- iv. Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria

- i. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mfumo wa sheria unaosimamia sekta ya Mifugo na Uvubi;
- ii. Kufanya Mapitio ya Mifumo ya Sheria; na
- iii. Kuwezesha Tume kutoa Elimu ya Sheria kwa Umma.

(ii)Makadirio ya Maduhuli ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/22

88. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 12,673,933,000.00** ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kama ifuatavyo;

Fungu 16	-	Sh.	3,332,000.00
Fungu 35	-	Sh.	54,400,000.00
Fungu 40	-	Sh.	12,571,199,000.00
Fungu 41	-	Sh.	45,000,000.00
Fungu 55	-	Sh.	2,000.00
JUMLA		Sh.	12,673,933,000

(iii) Makadirio ya Bajeti ya Wizara na Taasisi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

90. Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vyta majukumu ya Wizara na taasisi, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 78,464,886,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti kwa mafungu saba ya Wizara na taasisi zake ni kama ifuatavyo:

NA.	MAELEZO	MAKADIRIO YABAJETI (SH)
1.	Mishahara yawatumishi	24,334,553,000
2	Matumizi mengineyo	41,404,503,000
3	Maendeleo (Ndani)	5,000,000,000
4.	Maendeleo (Nje)	7,725,830,000
JUMA		78,464,886,000

91. Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha fedha kinaombwa kupitia mafungu ya bajeti yaliyo chini ya Wizara kama ifuatavyo: -

FUNGU 12: TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA

MAELEZO	MAKADIRIO YA BAJETI (SH)
Matumizi ya Mishahara	420,191,000
Matumizi Mengineyo	2,700,000,000
Fedha za Maendeleo (Ndani)	0
Fedha za Maendeleo (Nje)	0
JUMLA	3,120,191,000

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

FUNGU 16: OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

MAELEZO	MAKADIRIO YA BAJETI (SH)
Matumizi ya Mishahara	2,650,210,000
Matumizi Mengineyo	5,022,981,000
Fedha za Maendeleo (Ndani)	1,000,000,000
Fedha za Maendeleo (Nje)	0
JUMLA	8,673,191,000

FUNGU 19: OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

MAELEZO	MAKADIRIO YA BAJETI (SH)
Matumizi ya Mishahara	2,658,329,000
Matumizi Mengineyo	7,729,518,000
Fedha iliyolindwa kwa ajili ya uendeshaji wa mashaauri ya Nje ya Nchi	1,743,500,000
Fedha za Maendeleo (Ndani)	0
Fedha za Maendeleo (Nje)	0
JUMLA	12,131,347,000

FUNGU 35: OFISI YA TAIFA YA MASHITAKA

MAELEZO	MAKADIRIO YA BAJETI (SH)
Matumizi ya Mishahara	9,199,868,000
Matumizi Mengineyo	12,068,944,000
Fedha za Maendeleo (Ndani)	3,000,000,000
Fedha za Maendeleo (Nje)	993,616,000
JUMLA	25,262,428,000

FUNGU 41: WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

MAELEZO	MAKADIRIO YA BAJETI (SH)
Matumizi ya Mishahara	6,089,479,000
Matumizi Mengineyo	5,865,271,000
Fedha za Maendeleo (Ndani)	1,000,000,000
Fedha za Maendeleo (Nje)	6,358,598,000
JUMLA	19,313,348,000

FUNGU 55: TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

MAELEZO	MAKADIRIO YA BAJETI (SH)
Matumizi ya Mishahara	2,495,556,000
Matumizi Mengineyo	3,850,280,000
Fedha za Maendeleo (Ndani)	0
Fedha za Maendeleo (Nje)	373,616,000
JUMLA	6,719,452,000

FUNGU 59: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

MAELEZO	MAKADIRIO YA BAJETI (SH)
Matumizi ya Mishahara	820,920,000
Matumizi Mengineyo	2,424,009,000
Fedha za Maendeleo (Ndani)	0
Fedha za Maendeleo	0
JUMLA	3,244,929,000
JUMLA KUU	78,464,886,000

92. Mheshimiwa Spika, vilevile, naliomba Bunge lako liidhinishe kiasi cha **Shilingi 153,228,859,000** kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama ambapo matumizi ya kawaida ni **Shilingi 113,038,859,000** na matumizi ya maendeleo ni **Shilingi 40,190,000,000**. Katika fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 53,066,756,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Mahakama, **Shilingi 2,197,721,000** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na **Shilingi 57,774,382,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Mahakama. Kwa upande wa fedha za maendeleo, kiasi cha **Shilingi 39,100,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,090,000,000** ni fedha za nje. Mchanguo wa matumizi ya bajeti kwa Mfuko wa mahakama ni kama ifuatavyo:

MAELEZO	BAJETI (SH.)
Matumizi ya Mishahara	55,264,477,000
Matumizi Mengineyo	57,774,382,000
Fedha za Maendeleo (Ndani)	39,100,000,000
Fedha za Maendeleo (Nje)	1,090,000,000
JUMLA	153,228,859,000

93. Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa kwenye vitabu vyatya Randama za mafungu husika ambavyo vimegawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge kuitia Mfumo wa Kielektroniki wa Bunge.

94. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa mawasilisho hayo.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MAKAMU MWENYEKITI
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGUE YA KATIBA NA SHERIA:**
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba taarifa nzima ya Kamati yetu iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa tathmini dogo sana ya uchambuzi kwenye suala la uzingatiaji wa usawa wa kijinsia, haki ya mtoto na mazingira Rafiki kwa watu wenye ulemavu, mahitaji maalum katika utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo chini ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa katika kipindi cha mwaka fedha 2015 – 2020 hadi 2020/2021, ujenzi wa majengo ya Mahakama katika kipindi hicho umezingatia mfumo jumuishi wenye kuwaleta karibu wadau wote wa mahakama katika mazingira ya utoaji haki kwa lengo la kumrahisishia mwananchi upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mfumo huu wa uzingatiaji haki jumuishi katika miundombinu ya Mahakama, Kamati imebaini kwamba ujenzi wa miundombinu hiyo imezingatia misingi ya haki ya za kibinadamu kwa kiasi kikubwa ikiwemo usawa wa kijinsia, haki za watoto na mazingira rafiki kwa watu wenye mahitaji maalum ambapo kwenye kila jengo jipya la mahakama kumejengwa nyumba maalum kwa ajili ya Afisa Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya ushauri. Pia kumekuwepo utenganishaji wa mahabusu za wanawake na mahabusu za wanaume na mahabusu za watoto pamoja na Ofisi za Huduma ya Msaada wa Kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ilibaini kuwa katika Mahakama zilizotembelewa zimeajiri Mahakimu na Maafisa wa Mahakama kwa kuzingatia jinsi zote wanawake na wanaume katika ngazi zote za utumishi kwenye mahakama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliweza kutoa ushauri kwenye masuala hayo kwa kutumia ujuzi na mbinu tulizoifunza chini ya Mradi wa Bunge wa *LSP II*, hivyo tunaishukuru Ofisi ya Bunge kwa kuendelea kutumia mradi wa *LSP II* katika kuziwezesha Kamati za Bunge katika kuchambua masuala mbalimbali na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kuridhishwa na hatua hiyo ya kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia na haki za watoto kwenye ujenzi wa miundombinu na uratibu wa shughuli za Mahakama, hivyo tunashauri Wizara nyingine na Taasisi zake ziige mfano mzuri wa Mahakama katika kuzingatia masuala hayo muhimu katika utekelezaji wa bajeti hususani miradi ya maendeleo kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mpango wa bajeti wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi

zake zote umeainisha maeneo 57 ya vipaumbele ukilinganisha na vipaumbele 30 vilivyopangwa kutekeleza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama vilivyoainishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na vipaumbele vilivyowekwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa sababu zinaendana na Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano, awamu ya tatu na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yanaleta mantiki ya kuwepo kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vipaumbele hivyo, Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kuendeleza jitihada zake katika kuhakikisha kwamba utekelezaji wa vipaumbele vyake unaakisi udhibiti wa rasilimali za nchi, uharakishwaji wa utoaji haki, uboreshwaji wa huduma na taaluma ya sheria, uboreshwaji wa mazingira ya utoaji haki na upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu kwa ustawi wa jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022; uchambuzi umebaini kuwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Serikali yameongezeka kwa Sh. 500,668,000, sawa na ongezeko la asilimia 3.96 la bajeti ya maduhuli kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa kiasi cha maduhuli kinachotegemewa kukusanya kwa kila fungu husika ni kama ilivyoainishwa katika jedwali Na.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021; kwa ujumla uchambuzi umebaini kuwepo ungezeko la Sh. 4,780,090,000 kwa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha

2021/2022, kiasi ambacho ni sawa na ongezeko la asilimia 6.49 ya bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, baada ya Kamati kuchambua Mafungu saba yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, ilibaini upungufu wa bajeti ya matumizi mengineyo kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali - Fungu 19; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Fungu 55, pamoja na Tume ya Kurekebisha Sheria - Fungu 59.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa kibajeti uliobainika ultiokana na kuwepo na changamoto katika gharama za usafiri ikiwemo uwepo wa magari chakavu kupita kawaida na uhitaji wa magari mapya kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kesi hizo. Hivyo kwa kuzingatia Kanuni ya 117(3) na (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwasilisha hoja za kibajeti kwa Mafungu mataatu yaliyobainika na hatimaye Serikali ilikubali kuyaongezea fedha Mafungu hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kasma ya bajeti ya gharama za usafiri wa Fungu 19 imeongezeka kutoka Sh. 285,000,000 iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka unaisha hadi Sh. 1,330,000,000 kiasi ambacho ni sawa na ongezeko la asilimia 466.67.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kasma ya bajeti ya gharama za usafiri ya Fungu 55 imeongezeka hadi kufikia Sh. 800,000,000 ikilinganishwa na Sh. 200,000,000 iliyotengwa kwa mwaka unaoisha sawa na ongezeko la asilimia 400. Kasma ya bajeti ya gharama za usafiri kwa Fungu 59 imeongezwa hadi kufikia Sh. 720,000,000 ukilinganisha na Sh. 150,000,000 iliyotengwa kwa mwaka ulioisha sawa na ongezeko asilimia 480.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla bajeti ya matumizi mengineyo imeongezeka kwa Sh. 6,544,863,000, ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 18.77 ya bajeti ya matumizi mengineyo kwa mwaka fedha unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inamshukuru Mheshimiwa Spika na Kamati yake ya Uongozi na Kamati ya Bajeti kwa kuridhia mapendekezo ya Kamati ambayo yalipokelewa na Serikali kuhusu kuboresha bajeti ya matumizi mengineyo kwa ajili ya kuziwezesha taasisi hizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe Hazina inatoa fedha hizo kwa wakati ili kuziwezesha taasisi hizo kupunguza changamoto kubwa ya usafiri gharama nydingine za uendeshaji ambazo zimekuwa zikiathiri utendaji wa taasisi hizo hasa ukichukulia ukweli kwamba kazi kubwa ya taasisi hizo inafanya nje ya ofisi yaani *field work* na hivyo kuhitaji uhakika wa magari yenye kumudu mazingira ya kazi zao pamoja na gharama nydinginezo za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi umebaini kuwa bajeti ya jumla ya maendeleo imepungua kwa shilingi 484,910,000 ambayo ni sawa na upungufu wa asilimia 3.67 ya bajeti ya mwaka unaoisha. Aidha bajeti ya ndani kwa upande wa maendeleo imeongeza kwa asilimia 12.79 huku bajeti ya nje kwa upande wa maendeleo imepungua kwa asilimia 12 ya bajeti ya mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa makadirio wa bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Wizara ya Katiba pamoja na taasisi yake umebainishwa katika jedwali la nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa kamati kwa ujumla kwenye utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2021 pamoja na makadirio ya mapato ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2122 kwa Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye maeneo matatu ya:-

- (i) Kuendelea kuimarisha Mfumo wa uandishi wa Sheria na Usimamizi wa Masuala ya Mikataba inayohusu rasilimali za nchi katika Sekta zote nchini;
- (ii) Kuongeza idadi ya Rasilimali Watu wa Taaluma mbalimbali, kuwajengea uwezo kwa njia ya Uanagenzi kupitia Wadau mbalimbali wa Maendeleo ndani na nje ya nchi, na;
- (iii) Kuboresha stahiki za Wanasheria wa Serikali na mazingira yao ya kazi kwa lengo la kuongeza Weledi na ufanisi zaidi kwa Watumishi hao katika kusimamia maslahi ya nchi na rasilimali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtakakamati inashauri kuwa ofisi ya Taifa ya mashtaka kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria iandae mpango mkakati wa kumiliki ofisi zake katika mikoa na wilaya za Kimkakati.

Aidha mpango wa mkakati huo uainishe ghamama za utekelezaji kwa awamu kwa lengo la kuiwezesha kamati kushauri ipasavyo kuhusu upatikanaji wa fedha za utekelezaji kwa kuzingatia mzunguko wa bajeti ya Serikali kwa pamoja katika Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kukamilisha mchakato wa maandalizi ya sera ya Taifa ya sheria kwa lengo ya kuwa na sera ya Taifa ya masuala ya sekta ya sheria yenye kujumuisha maoni ya wadau mbalimbali ili kuwepo mwelekeo mmoja wakitaifa kuhusu mfumo wa sekta ya sheria nchini kwa maendeleo ya Taifa;
- (ii) Kukamilisha na kutekeleza Awamu ya Pili ya *program* ya maboresho ya sekta ya sheria LSRPII kwa ajili ya lengo la kutatua changamoto zilizopo na kuwezesha sekta ya sheria kutoa mchango stahiki katika kufanikisha malengo ya Kitaifa na kuleta maendeleo nchini;

(iii) Kuendelea na utekelezaji wa programu ya kuendesha mafunzo ya watoaji huduma za msaada wa kisheria kwa kuimarisha ushirikiano na taasisi ya mafunzo ya wanasheria kwa vitendo kwa lengo la kuwa na mtahala wa mafunzo ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria wenye kutambuliwa na Baraza La Taifa la Elimu ya Ufundi yani *NACTE*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafuzo hayo ni muhimu katika kuimarisha huduma ya msaada wa kisheria kwa kuweka mizania ya ubora na kiwango sawa cha aina ya huduma za msaada wa kisheria na hivyo kuongeza wigo na usogezaji wa huduma za kisheria kwa wananchi hususani wananchi wanyonge na kuwawezesha kufikia haki kwa wakati;

(iv) Kusimamia uwekaji wa mfumo ya uangalizi na usimamizi wa masuala ya utajiri asilia na mallasilia za nchi katika sekta mbalimbali nchini ambayo inahakikisha kwamba, Taifa linafaidika na rasilimali na utajiri wake kwa mujibu wa sheria zilizopo kwa kuendelea kuweka utaratibu wa kisheria utakaowezesha Serikali na wananchi wake kufaidi rasilimali hizo kwenye sekta mbalimbali pasipo kuathiri kazi haki za wawekezaji wa nje;

(v) Kuendelea kutekelezamkakati wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu kuititia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini yaani (*RITA*), kwa kuendelea kuimarisha shughuli za usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili kama moja ya haki za msingi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Utekelezaji huo uambatane na jitihada za kuimarisha matumizi ya *TEHAMA* katika utoaji huduma za usajili, Mfumo wa Usajili kwa kutumia mtandao (e-huduma) kwa lengo la kuwfikia wananchi wengi zaidi na kutoa huduma hizo kwa wakati;

(vi) Wizara ya Katiba na Sheria iendelee na ushirikiano wake na Mahakama katika kusimamia ujenzi wa Majengo ya Mahakama yenye mfumo shirikishi wa utoaji haki, kwa lengo la kuendelea kuboresha mazingira ya utoaji haki kwa wananchi, kwa wakati na kwa bei nafuu. Hii ni pamoja na

kuendelea kushirikiana na Mahakama katika kukamilisha mchakato wa maandalizi ya Mpango wa Pili wa kuboresha miundombinu ya utoaji haki kwa Mahakama zote nchini, kwa kuzingatia mzunguko wa Bajeti ya Serikali na mwisho;

(vii) Kamati inaishauri Serikali kuwa, fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na fedha za Matumizi ya Kawaida zitolewe kwa wakati ili kuiwezesha Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi hususan utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu, kwa mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 55 -Tume ya Haki za Binadamu na utawala boraKamati inashauri kuwa:-

(i) Tume ikamilishe na kuanza kutekeleza mpango kazi wa pili wa Taifa wa haki za binadamu wa miaka mitano (5) (2021 hadi 2026), kwa lengo la kuwa na muongozo wa kitaifa wa kutatua changamoto zilizopo katika masuala ya haki za binadamu, kwa lengo la kuboresha usimamizi na uratibu wa masuala yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa mpango kazi wa kwanza. Aidha, mchakato huo ushirikishe wadau wote kutoka pande mbili za muungano, kwa lengo la kuepusha changamoto zisizokuwa za lazima wakati wa utekelezaji;

(ii) Tume iendelee kufanya ukaguzi katika sehemu zote nchini zenyne malalamiko ya ucheleweshaji wa haki na kutoa taarifa kwa mujibu wa sheria ili kutatua changamoto hizo endapo zitabainika kuwepo; na

(iii) Serikali ihakikishe fedha zilizotengewa kwa ajili ya Fungu 55, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 59 Tume ya Kurekebisha SheriaKamati inaendelea kuishauri Tume ya kurekebisha Sheria kuendelea kufanyia kazi mapitio ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na Mifumo

ya Sheria katika Sekta mbalimbali nchini unaozungumza lugha moja yaani (*Uniformity of Law*) na inayoendana na hali halisi kwa sasa, kwa lengo la kuhakikisha Sekta ya Sheria inachochea kasi ya maendeleo ya Taifa, kwa ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nihitimishe taarifa hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Spika, pamoja na wewe mwenyewe Naibu Spika, kwa kuliendesha Bunge hili la Kumi na Mbili na kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutelekeza majukumu mliyopewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa ushirikiano wake mzuri katika kuiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake ikiwemo ushiriki wake katika vikao vy'a kamati, ziara za kikazi na uchambuzi wa Bajeti hii kwa ufanisi uliokusudiwa.

Aidha, ni imani ya Kamati kuwa, Waziri wa Katiba na Sheria aliye po kwa sasa, Mheshimiwa Profesa Palamagamba J.A.M Kabudi na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, pamoja na Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Wizara hii, wataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza ushauri wa kamati na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kamati inamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Profesa Sifuni Mchome pamoja na Naibu wake Ndugu Amon Mpanju, kwa ushirikiano wao mzuri katika kufanikisha shughuli za Kamati, katika kipindi chote walichohudumu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati itaendelea kutambua kazi nzuri iliyotekeliza na aliye kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii katika sekta ya sheria nchini, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, ambaye kwa sasa ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kamati itaendeleza

misingi mizuri aliyoiacha na hivyo tunamtakia mafanikio mema katika majukumu yake mapya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti naomba majina yao kama yalivyo katika taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge, Nd. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kuwashukuru Wakurugenzi wasaidizi wote katibu wa Bunge kama walivyotambuliwa kwenye taarifa hii kwa kufanikisha shughuli za kamati kwa ufanisi mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ilivyo wasilishwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Naibu Spika naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA
SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA
KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA
2020/2021; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO NA
TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022- KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020**, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba

na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Taarifa hii ni majukumu ya Kamati ya Katiba na Sheria kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (2) (b) na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyogeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hizo kwa pamoja zimeweka masharti kuwa, kabla ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kujadailiwa Bungeni, yanapaswa kuchambuliwa na Kamati hii. Noamba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelizwa chini ya Wizara hii kwa mujibu wa **Kanuni ya 117(1)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kudokeza kuhusu Taarifa hii inayohusu uchambuzi wa Bajeti ya Mafungu Saba (7) yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria. Mafungu hayo ni:-

- i) **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama,
- ii) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
- iii) **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,
- iv) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,
- v) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria,
- vi) **Fungu 55**- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na
- vii) **Fungu 59** –Tume ya Kurekebisha Sheria,

Mheshimiwa Spika, katika hatua hiinalijulisha Bunge lako tukufu kuwa Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makuu manne yafuatayo:-

- i) Matokeo ya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa mwaka unaoisha pamoja na hatua ya utekelezaji wa Miradi hiyo hadi kufikia Mwezi Machi, 2021;
- ii) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na;

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

2.0 MATOKEO YA ZIARA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulitokana na masharti ya Kanuni ya wa **Kanuni ya 117(2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hiyo iliweka sharti linalotaka siku zisizozidi Saba zitumike kwa ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ilizingatia masharti hayo kwa kutembelea miradi ya Ujenzi wa majengo ya Mahakama katika Mikoa ya Dodoma Wilayani Kongwa, Njombe, Morogoro na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na ziara hiyo pamoja na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Miradi ya maendeleo, Kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Ujenzi wa Majengo ya Mahakama katika kipindi hicho umezigatia mfumo jumuishi unaowaweka karibu wadau wote wa mahakama katika mazingira ya utoaji haki. Lemgo la kufanya hivyo ni kuwezesha upatikanaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu;

ii) Ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya uzingatiaji haki jumuishi katika miundombinu ya Mahakama, umezingatia misingi ya haki za Binadamu. Miongoni mwa misingi hiyo ni usawa wa jinsia, haki za Watoto na Mazingira rafiki kwa Watu wenye mahitaji maalum. Mfano wa kuzingatia hayo ni ujenzi wa kila jengo jipya la Mahakama uliofanyika kwa kuweka vyumba maalumu kwa ajili ya Afisa Maendeleo ya Jamii. Mfano mwingine ni utenganishaji wa mahabusu za Wanawake, mahabusu za Wanaume na Mahabusu za Watoto, pamoja na kuweka Ofisi za Huduma ya Msaada wa Kisheria.

iii) Tatu, Mahakama zilizotembelewa, zimeajiri Mahakimu na Maafisa wa Mahakama kwa kuzingatia jinsia zote, yaani wanawake na Wanaume katika ngazi mbalimbali za Utumishi kwenye Mahakama hizo.


Mheshimiwa Spika, Kwa matokeo hayo, Kamati imeridhika kuwa Wizara imefanya vizuri kuzingatia Masuala ya usawa wa kijinsia na haki za Watoto kwenye ujenzi wa miundombinu na uratibu wa Shughuli za Mahakama. Kwa sababu hiyo, ni maoni ya Kamati kuwa Wizara na Taasisi nyingine zikiiga mfano wa Mahakama kuzingatia masuala hayo muhimu kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo, zitachochea maendeleo endelevu na ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ziara za kutembelea Miradi ya Maendeleo iliyohusika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Taarifa hiyo ilihusu utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Mahakama katika mikoa yote kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020 na utekelezaji wa miradi inayoendelea kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Madhumuni ya Taarifa hiyo ni kuijulisha Kamati hali ilivyo na kuiwezesha kufuatilia na kushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa hiyo unadhihirisha yafuatayo:-

i) Kati ya Mikoa 26 ya Tanzania Bara, ni mikoa 14 tu karibu sawa na asilimia 54 ndiyo iliyokuwa na majengo na ilitoa huduma ya Mahakamu Kuu. Tafsiri yake ni kuwa tatizo la ukosefu wa majengo na huduma ya mahakama kuu lilituwepo katika mikoa karibu sawa na asilimia 46 ya mikoa nchini kama inavyoonekana katika **Grafu Na.1**.


Grafu Na. 1 Ulinganisho wa mikoa iliyokuwa Mahakama yenyé majengo na huduma za Mahakama kuu na mikoa isiyó kuwa na majengo na huduma hiyo



Chanzo: Taarifa ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi na Programu za Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2015 – 2020

ii) Kati ya wilaya 135, ni wilaya 27 tu sawa na asilimia 19.4 zilikuwa na majengo yaliyomilikiwa na Mahakama, na Wilaya 83 sawa na asilimia 59.7 zilikuwa zikitumia majengo ya taasisi nyingine na nyumba za watu binafsi wakati wilaya 25 zilikuwa zinahudumiwa na wilaya jirani. Tafsiri yake ni kuwa karibu asilimia 80 ya wilaya zote nchini hazikuwa na majengo yanayomilikiwa na mahakama. Aidha, wilaya zilizotoa huduma ya mahakama ni karibu asilimia 82 tu ya wilaya zote nchini kama inavyoonekana katika Grafu Na. 2. Hali hiyo ilipaswa kuboreshwa zaidi ili kuimarisha hali ya upatikanaji wa haki nchini.

Grafu Na. 2 Ulinganisho wa wilaya kwa kuzingatia kuwapo kwa majengo yanayomilikiwa au kutumiwa na Mahakama pamoja na upatikanaji wa huduma za Mahakama wilayani



Chanzo: *Taarifa ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi na Programu za Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2015 – 2020*

iii) kat i ya kata 3,963 zilizokuwapo nchini, kata 834 karibu sawa na asilimia 21 ndizo zilizokuwa zinatoa huduma za mahakama za mwanzo. Tafsiri yake ni kuwa uhaba wa mahakama za mwazo katika kata nchini ni karibu asilimia 79. Hali hii haikuwa nzuri katika kurahisisha upatikanaji wa haki nchini.

Mheshimiwa Spika, uhaba na ubovu wa miundombinu ya Mahakama nchini kama ilivyobainika katika uchambuzi wa taarifa hii, ulisukuma Serikali kuandaa na kuanza utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama, kuanzia 2016/17-2020/2021. Katika kipindi hicho, Bunge kupitia Kamati yake ya Kudumu ya Katiba na Sheria liliendelea kuwa sehemu ya usimamizi wa utekelezaji wa mpango huo, unaoendelea kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, hadi mwezi Julai, 2020, Serikali kupitia Mahakama, ilikuwa imekamilisha ujenzi wa Miradi 35 ya majengo ya Mahakama

nchini ilijojumuisha:- Mahakamu Kuu Tatu (3), Mahakama za Hakimu Mkazi Sita(6), Mahakama za Wilaya Kumi na Nne (14), na Mahakama za Mwanzo Kumi na Mbili (12), katika Mikoa na Wilaya mbalimbali hapa nchini.

Aidha, kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021, Bunge lako Tukufu liliidhinisha Bajeti ya kuiwezesha Mahakama kukamilisha majengo Sita (6) ya mahakama yenye Mfumo wa Haki Jumuishi (*intergrated Justice Centres*) katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Morogoro, Dodoma na Dar Es Salaam. Vile vile bajeti ya kipindi hicho iliwezesha Ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya 33, ikiwemo Mahakama ya Mji wa Kibaigwa, Wilayani Kongwa, ambayo imekamilika, kwa viwango vya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Serikali Imeendelea na juhudzi za kuimarishe miundombinu ya utoaji haki na huduma za kisheria kwa kukamilisha miradi ya ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu Sumbawanga, ujenzi wa jumla ya majengo mawili (2) ya Mahakama za Hakimu Mkazi katika mikoa ya Simiyu na Njombe; Kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya tatu(3) za Kasulu, Makete na Wanging'ombe.

Aidha, Kamati imebaini kukamilika kwa Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo (6); za Ngerengere (Morogoro), Mtae(Lushoto), Msanzi, Laela, Mtowisa (Sumbawanga) na Kibaigwa (Kongwa); na ujenzi wa Nyumba za Mahakimu Loliondo na ujenzi wa Jengo la kuhifadhi Kumbukumbu mkoani Tanga. Vilevile, imebainika kukamilika kwa Ujenzi wa nyumba mbili(2) za Majaji mkoani Kigoma na nyingine mbili(2) za mkoani Mara.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na jitihada za Serikali katika kuzingatia na kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi ya 2015/2020 ambayo iliongoza maandalizi na utekelezaji wa bajeti kama iliyobainishwa katika Ibara ya 118-119) ya Sura ya Sita ya llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025, iliyohusu kuboresha na kuimarishe mazingira ya utoaji haki kwa lengo la kumrahisishia

mwananchi wa kawaida kuipata haki yake kwa gaharama nafuu na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano wa Mahakama (2015/2020), uliolenga kuboresha mazingira ya miundombinu ya upatikanaji wa haki kwa Wananchi. Mpango huo, uliandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, pamoja na llani ya Chama cha Mapinduzi ya 2015/2020. Kwa sababu hiyo, Kamati inamaoni kuwa endapo Serikali itatoa kiasi kilichobaki cha fedha za maendeleo kabla ya tarehe 30 Juni, 2021, ujenzi wa Majengo ya Mahakama unaondelea nchi nzima, unaweza kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa miradi hiyo kutaendelea kuboresha mazingira ya utoaji haki nchini ikiwemo kupunguza usumbufu kwa baadhi ya Wananchi wanaotembea kilomita nyingi kutoka wilaya moja kwenda wilaya nyingine ili kufuata haki ya Mahakama katika mashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali na Mahakama kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa katika Majengo ya Mahakama mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi na mazingira rafiki katika suala zima la utoaji haki kwa wananchi wetu.

3.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge. Taarifa hiyo iliripoti mambo mkuu mawili ambayo ni:-

- i) Utekelezaji wa mpango na Bajeti ya mwaka 2020/2021 hadi kufikia mwezi Februari, 2021; na
- ii) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati uliotolewa wakati Bunge lilipokuwa likijadili makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Sasa naomba kulijulisha Bunge hili kuhusu Matokeo ya Uchambuzi uliofanywa na Kamati kama ifuatavyo:-

4.0 Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya uchambuzi wa taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria khusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ni kulinganisha upatikanaji wa fedha na idhini ya Bunge kuhusu Bajeti. Aidha, uchambuzi huo unakusudia kuonesha mwenendo wa uzingatiaji wa vipaumbele vya kibajeti na kushauri ipasavyo kwa mwaka unaofuata. Kwa madhumuni hayo, njia kuu zilizotumiwa kufanya uchambuzi ni pamoja na kuangalia hali halisi, Kuzingatia takwimu mbalimbali zilizowasilishwa kwenye Kamati pamoja na mahojiano. Matumizi ya asilimia na ulinganisho kitakwimu yalisaidia kupata matokeo na tafsiri ya hali.

5.0 Ukusanyaji wa mapato ya serikali yalikadirwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, kwa rejea ya Bunge lako tukufu katika taarifa hii, matokeo ya uchambuzi yanaonekana katika muhtasari unaodhishwa kwa jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida, Wizara ya Katiba na Sheria ina jumla ya Mafungu Saba (7) yanayokusanya maduhuli ambayo ni:-

- i) **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama;
- ii) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- iii) **Fungu 35**- Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;
- iv) **Fungu 40**- Mfuko wa Mahakama (**Kamati ya Bajeti**);
- v) **Fungu 41**-Wizara ya Katiba na Sheria;
- vi) **Fungu 55**-Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na
- vii) **Fungu 59**-Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati ililinganisha lengo la makusanyo lililowasilishwa Bungeni kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na

makusanyo halisi. Muhtasari wa mchanganuo wa ulinganisho unaonekana katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1 Mchanganuo wa Ulinganisho wa Kiasi cha Mapato Kilichoidhinishwa na Bunge na Kiasi halisi kilichokusanywa hadi kufikia Mwezi Februari, 2021

Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya WKS ya Tarehe 29 Machi, 2021

Mhesimiwa Spika, kutokana na Uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa Kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Februari 2021, Wizara na Taasisi zake ilikusanya jumla ya **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Sita Arobaini na Moja, Hamsini na Nne Elfu na Sitini na Tano, na Senti Hamsini** (5,641,054,065.50), kasi ambacho ni sawa na asilimia **44.60** ya makukusanyo. Kiasi hicho ni pungufu ya lengo la makusanyo yaliyokusudiwa katika robo tatu ya mwaka wa fedha unaoisha, kwa kuzingatia mgawanyo wa makusanyo yote katika robo nne za mwaka mzima.

Mhesimiwa Spika, tafsiri ya uchambuzi huo ni kwamba, mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake katika robo tatu za mwaka unaoisha hauendani na matarajio.

Hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa, kuna umuhimu wa kuzingatia uhalisia wakati wa kupanga lengo la mapato ya serikali. Kutokufanya hivyo, ni kutoa picha isiyo sahihi kuhusu jumla ya mapato ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaohusika.

6.0 Upatikanaji wa fedha za Matumizi

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu, Kamati ilitumia njia ya ulinganisho kwa asilimia kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.**

Jedwali Na. 2 Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na Kiasi Kilichopokewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2021

MATUMIZI	BAJETI ILIOIDHINISWA NA BUNGE	KIASI KILICHOPOKELEWA HADI FEBRUARI, 2021	ASILIMIA
Mishahara (PE)	25,614,416,000.0	13,452,199,948.0	52.52
Matumizi mengineyo (OC)	34,859,640,000.0	25,355,356,845.0	72.74
Miradi ya Maendeleo (DEV) Ndani (4,433,200,000.0) Nje (8,777,540,059.0)	13,210,740,059.0	1,320,677,335.0	11.70
Jumla	73,684,796,059.0	40,128,234,128.0	10.0

Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya WKS ya Tarehe 29 Machi, 2021

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati ulibainisha yafuatayo:-

i) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kawaida za Wizara ulikuwa mzuri kwa kufikia kiasi cha asilimia 72.74 ya lengo. Mwenendo huu haukusababisha changamoto ya utekelezaji wa mipango kwa mwaka wa fedha 2020/2021;

ii) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za kugharimia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ulifika kiasi cha asilimia 11.7 tu ya bajeti iliyoidhinishwa. Hali hii ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa miradi mizuri iliyokuwa imepangwa. Kwa mchanganuo huo, upatikanaji wa fedha za maendeleo umekuwa si wa kutumainiwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, ni maoni ya Kamati kuwa kama Hazina haitatao pesa zilizobakia, uzuri wa mipango yenye nia ya kuboresha utoaji haki na upatikanaji wa haki hautakuwa na tija. Kwa sababu hiyo, upo umuhimu wa kuhakikisha kuwa kabla ya kufika tarehe 30 Juni, 2021, kiasi cha fedha kilichobaki kukamilisha bajeti iliyoidhinishwa kinapatikana kwa mafungu yote ya wizara hii.

7.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezsha Bunge lako tukufu kuwa na mjadala wenye tija kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara hii, Kamati ilichambua makadirio ya mapato na makadirio ya matumizi kama ifuatavyo:-

8.0 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, ili kuona uhalisia na uwezekano wa mapato yanayopendekezwa, Kamati illinganisha ukusanyaji wa mapato hayo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na makadirio ya mapato ya wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Matokeo ya ulinganisho huo yanaonekana kwa muhtasari katika **Jewadali Na. 3** la Taarifa hii.

Jedwali Na. 3 Ulinganisho wa Bajeti ya Mapato kwa mwaka wa fedha unaoisha na Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022

FUNGU	MAPATO 2020/21	MAKADIRIO 2021/22	ONGEZKO/PUNGUZO
Fungu 12	0	0	-
Fungu 16	3,332,000.00	0	-100.0
Fungu 35	15,000,000.00	54,400,000.00	262.7
Fungu 40	12,571,199,000.00	12,571,199,000.00	0.0
Fungu 41	45,000,000.00	20,000,000.00	-55.6
Fungu 55	2,000	2,000,000	0.0
Fungu 59	0	0	-
JUMLA	12,634,533,000	13,135,201,000	4.0

Chanzo: Taarifa ya Bajeti WKS ya Tarehe 29 Machi, 2021

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato unaonesha yafuatayo:-

- i) Makadirio hayo kwa mafungu yote ispokuwa Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashitaka yamezingatia uhalisia na uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha unaoisha;
- ii) Makadirio ya mapato kwa ofisi ya Taifa ya Mashitaka, Fungu 35 huwenda yasiwe na uhalisia kwa kutumia uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha unaoisha, ambapo Ofisi hiyo ilifikia lengo kwa asilimia 40 tu. Kiasi kinachokadiriwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kimeongezeka zaid bila kuzingatia kutofanikiwa kwenye makusanyo kwa lengo liliwekwa katika mwaka wa fedha unaoisha.
- iii) Makadirio ya mapato kwa ujumla hayakuzidi sana ikillinganishwa na mwaka wa fedha unaoisha. Hata hivyo, iwapo mwenendo wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ungezingatiwa, makadirio ya jumla ya mapato yangefaa kushuka badala ya kupanda ili kutoa picha halisi ya jumla ya mapato ya serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa kuna umuhimu wa kuzingatia uhalisia wakati wa kukadiria mapato yanayoweza kukusanya kwa kila mwaka wa fedha. Aidha, mwenendo wa makusanyo kwa mwaka unaoisha unaweza kutumika kama kiashiria kimojawapo cha uwezekano wa lengo linalokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha.

9.0 Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/22

Mheshimiwa Spika, Kabla ya kuchambua makadirio ya matumizi ya wizara hii, Kamati ilifanya mapitio ya malengo na vipaumbele ikillinganishwa Mpango wa miaka mitano. Uchambuzi umeonesha yafuatayo:-

- i) Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/22, umeandaliwa kwa kuzingatia ipasavyo: Dira ya Taifa 2025,

Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/22-2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, na Mpango Mkakati wa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake (2021/22-2025/26) na maelekezo mengine ya Viongozi wa Kitaifa.

- ii) Mpango huo umeainisha maeneo Hamsini na Saba (57) ya Vipaumbele vya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake zote, ikilinganishwa na vipaumbele thelathini (30) vilivyopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa fedha 2020/2021, kama vilivyobainishwa na Mto Hoja.
- iii) Mpango umeainisha vipaumbele kwa kujumuisha maeneo yote ya Msingi yanayoendana na mantiki ya kuanzishwa kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake hapa nchini pamoja na dhima na dhamira ya wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Kwa matokeo hayo, Kamati imeridhishwa na vipaumbele vilivowekwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Naomba kulishauri Bunge lako tukufu kuridhia vipaumbele hivyo vilivyobainishwa na mtoa hoja. Naomba niseme kuwa katika jumla yake, vipaumbele vilivyobainishwa vinaendana na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/22-2025/26), na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vipaumbele hivyo, Kamati ina maoni kuwa ili lengo kuu la serikali ambalo ni ustawi wa wananchi kama liliwyobainishwa katika Ibara ya 8 (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 lifanikishwe, Wizara hii inatakiwa kuendelea kutimiza dhima yake. Kwa mfano:

Wizara bado inapaswa kuhakikisha kwamba, vipaumbele vyake vinaakisi udhibiti wa rasilimali za nchi, uharakishwaji wa utoaji haki, uboreshaji wa taaluma ya sheria, uboreshaji wa mazingira ya utoaji haki na upatikanaji wa haki kwa wakati

na kwa gharama nafuu. Mambo hayo ni muhimu kwa ustawi wa Jamii ya Watanzania na yanaweka msingi wa mamlaka ya nchi na vyombo vyake vyote kuwezesha kuondolewa kwa aina zote za dhulma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu au upendeleo usiyostahili kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 9 (h) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

10.0 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika kfanya uchambuzi wa Makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati ilifanya ulinganisho wa vipengele na kasama mbalimbali katika makadirio hayo. Aidha malengo yaliyokuwa yamepangwa na mwenendo wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha, vilitumika kuwezesha uchambuzi huo ambao muhtasari wake unaonekana katika Jedwali Na. 4 la taarifa hili.

Jedwali Na.4: Mchanganuo wa Kiasi cha Fedha kinachoombwa kwa Mafungu ya Bajeti yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Matumizi	Bajeti iliyoidhinishwa 2020/2021 (Shilingi)	Makadirio ya Bajeti 2021/22 (Shilingi)	Ongezeko(+) au pungufu(-)	Asilimia ya Ongezeko/ Upungufu
Mshahara ya watumishi	25,614,416,000	24,334,553,000	-1,279,863,000	-5.00
Matumizi mengineyo	34,859,640,000	41,404,503,000	+6,544,863,000	+18.77
Mradi ya Maendeleo (Ndani)	4,433,200,000	5,000,000,000	+566,800,000	+12.79
Mradi ya Maendeleo (Nje)	8,777,540,000	7,725,830,000	-1,051,710,000	-11.98
	73,684,796,000	78,464,886,000	+4,780,090,000	+6.49

Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya WKS ya Tarehe 29 Machi, 2021

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, uchambuzi umeonesha kuwa:

- i) Kuna ongezeko la **Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Saba Themanini, na Tisini Elfu (4,780,090,000)**, kwa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria Sheria na Taasisi zake kwa mwaka 2021/22, kiasi ambacho ni sawa na ongezeko la **asilimia 6.49** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa mwaka unaoisha. Hali hiyo inaashiria kuongezeka kwa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya wizara iwapo upatikanji wa fedha utakuwa katika mtiririko unaostahili.
- ii) Bajeti ya jumla ya maendeleo imepungua kwa **Shilingi Milioni Mia Nne Themanini na Nne, Laki Tisa na Kumi Elfu, (493,910,000)**, ambayo ni sawa na pungufu ya **asilimia 3.67** ya Bajeti ya mwaka unaoisha..
- iii) Kwa ujumla, bajeti ya Matumizi mengineyo imeongezeka kwa Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tano Arobaini na Nne, Laki Nane Sitini na Tatu Elfu (6,544,863,000), ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 18.77 ya bajeti ya matumizi mengineyo kwa mwaka wa fedha unaoisha.
- iv) Upo upungufu wa Bajeti ya Matumizi Mengineyo kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Fungu 19), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) pamoja na Tume ya Kurebisha Sheria (Fungu 59). Upungufu wa kibajeti uliobainika ultokana na kubainika kwa changamoto katika gaharama za Usafiri, ikiwemo uwepo magari chakavu kupita kawaida na uhitaji wa magari mapya, kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia **Kanuni ya 117 (3) na (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge**, Kamati iliwasilisha hoja za kibajeti kwa mafungu matatu yaliyobainika, na hatimaye Serikali ilikubali kuyaongezea fedha mafungu hayo kama ifuatavyo:-

Mosi: Kasima ya Bajeti ya gharama za Usafiri kwa Fungu 19 imeongezeka kutoka Shilingi **Milioni Mia Mbili Themanini na**

Tano Elfu (285,000,000) iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka unaoisha hadi Shilingi **Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Thelathini Elfu (1,330,000,000)**, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 466.67 ya ongezeko la Kassima hiyo;

Pili: Kasima ya bajeti ya gharama za usafiri kwa Fungu 55 imeongezwa hadi kufikia shilingi **Milioni Mia Nane(800,000,000)** ikilinganishwa na Milioni Mia Mbili Elfu (200,000,000) iliyotengwa kwa mwaka unaoisha, sawa na ongezeko la asilimia 400; na

Tatu: Kasima ya bajeti ya gharama za usafiri kwa Fungu 59 imeongezwa hadi kufikia **Milioni Mia Saba Ishirini Elfu(720,000,000)** ukilinganisha na **shilingi Milioni Mia Hamsini Elfu (150,000,000)** iliyotengwa kwa mwaka unaoisha, sawa na ongezeko la **asilimia 480.**

Mheshimiwa Spika, Kamati inakushukuru wewe binafsi, Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti, kwa kuridhia mapendekezo ya Kamati ambayo yalipokelewa na Serikali. Mapendekezo hayo yalihusu kuboresha bajeti ya Matumizi mengineyo kwa ajili ya kuziwezesha Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Hivyo, Kamati ina maoni kuwa kuwa, kama Hazina haitatoa fedha hizo kwa wakati, Taasisi hizo hazitaweza kupunguza changamoto kubwa ya usafiri, na gharama nyingine za uendeshaji. Hali hiyo itaendelea kuathiri utendaji wa Taasisi hizo, na hasa kwa kuwa, kazi kubwa ya Taasisi hizo inafanyika nje ya Ofisi (*Field Work*), jambo linalohitaji uhakika wa magari yenye kumudu mazingira ya kazi zao, pamoja na gharama nyinginezo za uendeshaji.

11.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitekeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake.

12.0 Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa:-

- i) Kuendelea kuimarisha Mfumo wa uandishi wa Sheria na Usimamizi wa Masuala ya Mikataba inayohusu rasilimali za nchi katika Sekta zote zinchni
- ii) Kuongeza idadi ya Rasilimali Watu wa Taaluma mbalimbali, kuwajengea uwezo kwa njia ya Uanagenzi kupitia Wadau mbalimbali wa Maendeleo ndani na nje ya nchi, na
- iii) Kuboresha stahiki za Wanasheria wa Serikali na mazingira yao ya kazi kwa lengo la kuongeza Weledi na ufanisi zaidi kwa Watumishi hao katika kusimamia maslahi ya nchi na rasilimali zake.

13.0 Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, iandae mpango mkakati wa kumiliki Ofisi zake katika Mikoa na Wilaya za kimkakati. Aidha, mpango mkakati huo uainishe gharama za utekelezaji kwa awamu, kwa lengo la kuiwezesha Kamati kushauri ipasavyo kuhusu upatikanaji wa fedha za utekelezaji, kwa kuzingatia mzunguko wa bajeti ya Serikali kwa kila mwaka.

14.0 FUNGU 41-Wizara ya Katiba na Sheria

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza yafuatayo:-

- i) Kukamilisha mchakato wa maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria, kwa lengo la kuwa na Sera ya Taifa ya masuala ya sekta ya Sheria yenye kujumuisha maoni ya wadau mbalimbali, ili kuwepo muelekeo mmoja wa Kitifa kuhusu mifumo ya Sekta ya Sheria zinchni kwa maendeleo ya Taifa;

- ii) Kukamilisha na kutekeleza awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria (LSRPII) kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo na kuiwezesha sekta ya Sheria kutoa mchango stahiki katika kufanikisha malengo ya kitaifa ya kuleta maendeleo nchini;
- iii) Kuendelea na utekelezaji wa programu ya kuendesha mafunzo ya watoaji huduma za msaada wa kisheria kwa kuimarissha ushirikiano na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, kwa lengo la kuwa na Mtaala wa mafunzo ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria wenye kutambuliwa na Baraza la Taifa ya Elimu ya Ufundji (NACTE). Mafunzo hayo ni muhimu katika kuimarissha huduma ya msaada wa kisheria kwa kuweka mizania ya ubora na kiwango sawa cha aina ya huduma za msaada wa kisheria, na hivyo kuongeza wilgo wa usogezaji wa huduma za kisheria kwa wananchi, hususan wanyonge na kuwawezesha kuifikia haki kwa wakati;
- iv) Kusimamia uwekaji wa mifumo ya Uangalizi na usimamizi wa masuala ya utajiri asilia na maliasilia za nchi katika sekta mbalimbali nchini, ambayo inahakikisha kwamba Taifa linafaidika na rasilimali na utajiri wake kwa mujibu wa Sheria zilizopo, kwa kuendelea kuweka utaratibu wa kisheria utakaoiwezesha Serikali na Wananchi wake kufaldi rasilimali hizokwenye sekta mbalimbali, pasipo kuathiri haki za wawekezaji wa nje;
- v) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu kuititia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), kwa kuendelea kuimarissha shughuli za usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili kama moja ya haki za msingi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Utekelezaji huo uambatane na jitihada za kuimarissha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma za usajili, Mfumo wa Usajili kwa kutumia mtandao (e-huduma) kwa lengo la kuwfikia wananchi wengi zaidi na kutoa huduma hizo kwa wakati;

- vi) Wizara ya Katiba na Sheria iendelee na ushirikiano wake na Mahakama katika kusimamia ujenzi wa Majengo ya Mahakama yenye mfumo shirikishi wa utoaji haki, kwa lengo la kuendelea kuboresha mazingira ya utoaji haki kwa Wananchi, kwa wakati na kwa bei nafuu. Hii ni pamoja na kuendelea kushirikiana na Mahakama katika kukamilisha mchakato wa maandalizi ya Mpango wa Pili wa kuboresha miundombinu ya utoaji haki kwa Mahakama zote nchini, kwa kuzingatia mzunguko wa Bajeti ya Serikali; na
- vii) Kamati inashauri Serikali kuwa, fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na fedha za Matumizi ya Kawaida zitolewe kwa wakati ili kuiwezesha Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi hususan utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu, kwa mwaka wa Fedha 2021/2022.

15.0 FUNGU 55 -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa:

- i) Tume ikamilishe na kuanza kutekeleza Mpango Kazi wa Pili wa Taifa wa Haki za Binadamu wa miaka mitano (5) (2021 hadi 2026), kwa lengo la kuwa na Muongozo wa Kitaifa wa kutatua changamoto zilizopo katika masuala ya haki za binadamu, kwa lengo la kuboresha usimamizi na uratibu wa masuala yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa kwanza. Aidha, mchakato huo ushirikishe wadau wote kutoka pande mbili za Muungano, kwa lengo la kuepusha changamoto zisizokuwa za lazima wakati wa utekelezaji;
- ii) Tume iendelee kufanya ukaguzi katika sehemu zote nchini zenye malalamiko ya ucheleweshaji wa haki na kutoa taarifa kwa mujibu wa Sheria ili kutatua changamoto hizo endapo zitabainika kuwepo; na
- iii) Serikali ihakikishe fedha zilizotengewa kwa ajili ya FUNGU 55, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

16.0 FUNGU 59 -Tume ya Kurekebisha Sheria

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Tume ya kurekebisha Sheria kuendelea kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na Mifumo ya Sheria katika Sekta mbalimbali nchini unaozungumza lugha moja (*Uniformity of Law*) na inayoendana na hali halisi kwa sasa, kwa lengo la kuhakikisha Sekta ya Sheria inachochea kasi ya maendeleo ya Taifa, kwa ustawi wa Jamii.

17.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesa Bunge la Kumi na Mbili (12) katika kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania, Aidha, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, (Mb), kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niipongeze pia Kamati yako ya Uongozi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesa Bunge la Kumi na Mbili. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, (Mb), kwa ushirikiano wake mzuri katika kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ikiwemo ushiriki wake katika vikao vya Kamati, ziara za kikazi na uchambuzi wa Bajeti hii kwa ufanisi uliokusudiwa. Aidha, ni imani ya Kamati kuwa, Waziri wa Katiba na Sheria aliyepo kwasasa, Mhe.Prof.Palamagamba J.A.M Kabudi (Mb), Naibu Waziri, Mhe.Geophrey Mizengo Pinda, (Mb) pamoja na Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa wa Wizara hii, wataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Prof.Sifuni Mchome pamoja na Naibu wake Ndg. Amon Mpanju, kwa ushirikiano wao mzuri katika kufanikisha shughuli za Kamati, katika kipindi chote walichohudumu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati itaendelea kutambua kazi nzuri iliyotekeliza na aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii katika sekta ya sheria nchini, Mhe.Mohamed Omary Mchengerwa, (Mb), ambaye kwa sasa ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kamati itaendeleza misingi mizuri aliyoiacha na hivyo tunamtakia mafanikio mema katika majukumu yake mapya.

Mheshimiwa Spika,kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake. **NAOMBA MAJINA YAO KAMA YALIVYO KATIKA TAARIFA HII YAINGIE KATIKA TAARIFA RASMI ZA BUNGE (HANSARD):-**

1. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. – Mjumbe
3. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb. – Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.-Mjumbe
5. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.-Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb -Mjumbe
7. Mhe. Zainabu Athumanji Katimba, Mb,-Mjumbe
8. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb,-Mjumbe
9. Mhe. Lemburis Saputu Mollel Noah, Mb, -Mjumbe
10. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb, -Mjumbe
11. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb, -Mjumbe
12. Mhe. Omar Ali Omar, Mb, -Mjumbe
13. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb, -Mjumbe
14. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb, -Mjumbe
15. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.-Mjumbe
16. Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb,-Mjumbe
17. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb,-Mjumbe
18. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb,-Mjumbe
19. Mhe. Jackline Ngonyani Msongozi, Mb, -Mjumbe

20. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb, -Mjumbe
21. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb,-Mjumbe
22. Mhe.Agnes Elias Hokororo, Mb,-Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Gerald S.Magili na Michael Chikokoto, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kushukuru Watendaji wote wa Idara husika za Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati hii kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba klishauri Bunge lako Tukufu likubali kujadili na na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Najma Murtaza Giga, Mb.
MAKAMU MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA
28 Aprili, 2021

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa nimuite sasa Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti Mheshimiwa Daniel Barani. (*Makofii*)

MHE. DANIEL B. SILLO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika,

naomba taarifa yangu iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mfuko wa mahakama (Fungu 40) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (1)(c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 pamoja na Kifungu cha 59 cha Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya mwaka 2011, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadilana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2020/21 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Tanzania ni moja kati ya Mihimili mitatu ya Dola na majukumu yake yameanishwa katika Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kama chombo kikuu cha kusimamia utolewaji wa Haki nchini. Hivyo, ni wazi kwamba chombo hichi ni muhimu sana katika ustawi wa jamii na maendeleo endelevu. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 lbara 107(a)(1) Mahakama ndio chombo pekee chenye mamlaka ya mwisho katika kutoa haki kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Mfuko wa Mahakama kuanzia Mwezi Julai, 2020

hadi Mwezi Februari, 2021, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2020/2021; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa Mahakama – Fungu 40 uliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 176.4 Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 55 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama bilioni 2.26 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto shilingi 53.8 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 69.875 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. katika fedha za Maendeleo, shilingi bilioni 39,000,000,000.00 ni fedha za ndani na bilioni 30.9ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2021, Mahakama ilipokea jumla ya Shilingi bilioni114.5 ambazo ni sawa na asilimia 64.88 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2020/21. Kati ya fedha hizo, shilingi 35.8 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, shilingi 32.7 bilioni ni kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama, shilingi 1.3 bilioni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na shilingi bilioni 44.6 ni fedha za maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo sh.23.5 bilioni ni fedha za ndani na shilingi 21 bilioni ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2020/2021 ulipanga kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 12.8 ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2021 kiasi kilichokuwa kimekusanya ni shilingi 5.6 bilioni ikiwa sawa na asilimia 45 ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama hadi kufikia mwezi Februari, 2021 ni wa kuridhisha, ambapo Serikali kwa kiasi kikubwa imekuwa ikitoa fedha kwa Mahakama kama zilivyoidhinishwa na Bunge na hivyo kuwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo huu unaonyesha hadi kufikia mwezi Juni, 2021 Fungu hili linaweza kuwa limepokea Bajeti kat i ya asilimia 80 hadi 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, pamoja na mwenendo huu bado jitihada kubwa zinahitajika za rasilimali fedha ili kuhakikisha kuwa Mahakama inafikia malengo yake ya utoaji wa huduma pamoja na ujenzi wa miundombinu yake. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa Mahakama inaendelea kuidhinishiwa Bajeti inayokidhi mahitaji yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jedwali Na. 1. Katika taarifa yangu inaonesha Mwenendo wa Bajeti wa Mfuko wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2020/2021 katika mwaka wa fedha 2020/2021, Mahakama katika kutekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia utoaji haki kwa wakati nchini, ilijiwekea vipaumbele mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuharakisha usikilizaji wa mashauri; kuimarisha utawala bora, maadili na uwajibikaji; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; kujenga miundombinu na kuongeza matumizi ya TEHAMA ili kupeleka huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza vipaumbele hivyo, mafanikio yaliyofikiwa na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni kama ifuatavyo:-

- a) Kumalizika mashauri 159,153 yaliyokuwa yamesajiliwa mwanzoni mwa mwezi Julai, 2020 hadi Februari, 2021;
- b) Kusikiliza mashauri 7,968 kwa njia ya *Video Conferencing* na kufanikiwa kuokoa shilingi 796.7 kwa upande wa Mahakama na shilingi millioni120 kwa upande wa Jeshi la Magereza;

- c) Kumaliza usikilizaji wa mashauri 192 kwa Mahakama inayotembea yaani (*Mobile Courts*) katika mikoa ya Mwanza na Dar-es-Salaam;
- d) Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji Maduhuli ya Serikali kuititia mfumo wa *GePG*;
- e) Kufanya Ukaguzi wa Mahakama nchi nzima, ambao ulibaini masuala mbalimbali ambayo yamepatiwa ufumbuzi na mengine kuwekewa mikakati ya muda mfupi na muda wa kati kwa ajili ya utekelezaji;
- f) Kuendelea kuboresha Mfumo wa Kielekitroniki kwa Kusajili na Kuratibu Mashauri ambao unawezesha mawasiliano na wadau wa Mahakama kwa kuwawezesha kupata mawasiliano kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi na barua pepe, hivyo kutohitajika kufika mahakamani shauri linapoahirishwa. Vilevile, Mfumo umerahisisha Malipo ya Ankara kwa kuunganishwa na Mfumo wa Ulipaji wa Serikali (*GePG*);
- g) Kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu kanda za Kigoma na Musoma;
- h) Kukamilika kwa ukarabati wa Mahakama Kuu kanda ya Sumbawanga. Kuendelea kukamilisha ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi na Katavi, Lindi; Mahakama za Wilaya za Bahi na Chemba; na Mahakama za Mwanza za Kibaigwa, Mlimba na Mang'ula;
- i) Kuendelea kukamilisha ujenzi wa vituo jumuishi vya kutolea haki katika mikoa ya Arusha, Morogoro, Mwanza, Dodoma, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayokatika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2020/21, Mahakama inaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Uhaba wa Mahakama za Mwanzo, ambazo ndio ngazi ya chini kabisa katika muundo wa Mahakama yenyе mamlaka ya kushughulikia mashauri ya jinai, madai, ndoa na usimamizi wa mirathi pamoja na rufaa kutoka mabaraza ya kata;

(ii) Upungufu wa watumishi kwa kada mbalimbali ikilinganishwa na mahitaji;

(iii) Changamoto ya Ucheleweshaji wa Mashauri bado ipo, hususani mashauri yanayohusu masuala ya biashara, mikopo, kesi za rufaa za kodi, rushwa, uhujumu uchumi na mashauri ya ardhi ambayo yanazorotesha ukuaji wa uchumi wa nchi.

(iv) Uchache na uchakavu wa Miundombinu ya Mahakama hususani Majengo ya Ofisi na Makazi ya Majaji na Watumishi;

(v) Uhaba wa vitendea kazi, hususani Magari kwa ajili ya shughuli za Ukaguzi wa mahakama zote nchini; na

(vi) Ukuaji mdogo wa matumizi ya TEHAMA katika kuongeza kasi ya usikilizaji wa kesi na uwekaji mzuri wa kumbukumbu. Aidha, katika kipindi cha mwaka jana ni mashauri 2435 tu yalifunguliwa kwa kielektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mapato na matumizi ya mfuko wa mahakama katika mwaka wa Fedha 2021/2022, Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na malengo ya mpango mkakati na ya kitaifa. Aidha, maeneo ambayo yamepewa kipaumbele ni yafuatayo: -

(i) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashahuri ya muda mrefu;

(ii) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (*TEHAMA*) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji huduma;

- (iii) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;
- (iv) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;
- (v) Kuanza kwa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania ili kuhamia Dodoma; na
- (vi) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mfuko wa Mahakama umepewaa ukomo wa jumla ya shilingi bilioni 153.2 Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 53 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama, bilioni 1.2 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, shilingi 57.8 bilioni ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo na shilingi 40.2 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo bilioni 39.1 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1.09 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya fungu hili imepungua kwa shilingi 23.2 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2021/2022 kutokana na fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya kesi na mapingamizi wakati wa uchaguziwa mwaka 2020 pamoja nafedha za maendeleo kutoka nje kupungua kutokana na kukoma kwa Mradi wa Maboresho ambaao uliokuwa unafadhiliwa na fedha za Mkopo kutoka Benki ya Dunia. Hata hivyo, Mahakama inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia ili kuona uwezekano wa kuendelea kupata fedha hizo kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mashauriano kati, Mahakama na Waziri wa Fedha na Mipango, Mahakama ilipewa nyongeza ya fedha ya jumla ya Shilingi bilioni 7.6 katika ukomo wa awali. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,000,000,000 zilliongezwa kwenye Bajeti ya Matumizi Mengineyo ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza hiyo ni kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zilizopo ikiwemo kugharamia uendeshaji wa vituo vipyta vya Mahakama Kuu na Mahakama za Wilaya pamoja na uhamisho wa watumishi waliokaa katika kituo kimoja kwa muda mrefu. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Mahakama iliongezewa shilingi bilioni 3.6 kwenye fedha za ndani ikilinganishwa na ukomo ultolewa ikiwa ni mahsusini kwa ununuzi wa magari. Nyongeza hiyo ya kibajeti nje ya ukomo ulifikiwa ili kutatua changamoto za kibajeti zinazoikabili Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, maduhuli; kwa upande wa mapato, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Mahakama imepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi bilioni 12.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Uhaba wa Mahakama za Mwanzo. Kati ya changamoto zinazoikabili Mahakama ni pamoja na uhaba wa Mahakama za Mwanzo. Kimuundo kila Kata nchini inatakiwa kuwa na Mahakama ya Mwanzo. Hata hivyo, mpaka sasa kati ya Kata 3,963 zilizopo kuna Mahakama za Mwanzo 960 tu na zinazofanya kazi ni 799 tu. Nyingine hazifanyi kazi na kufungwa kutoptana na uchakavu wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kasi ndogo ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika kila kata kutoptana na changamoto ya rasilimali fedha, Mahakama imechukua uamuzi wa kuanza na ujenzi wa Mahakama katika kila Tarafa, uamuzi ambao ni wa busara. Matarajio ya mpango ujao ni kujenga Mahakama za Mwanzo katika Tarafa 142 kati ya Tarafa 570 zilizopo nchini. Hii inashiria bado kutakuwa na changamoto ya Mahakama ukilinganisha na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaishauri Mahakama wakati wa ujenzi huu katika Tarafa, ujenzi uzingatie idadi ya watu katika Tarafa husika, umbali kati ya Tarafa, shughuli za kiuchumi za Tarafa lakini pamoja na ukubwa wa mashauri yanayoshughulikiwa na Mahakama hizo ili ujenzi huo uwe na tija na kuondoa adha kwa wananchi.

Hivyo, ushirikiano kati ya Mhimili wa Mahakama, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ni wa muhimu na lazima ili kuhakikisha viashiria hivyo muhimu vinazingatiwa. Vilevile, kipaumbele kitolewe katika ujenzi wa hizi Mahakama za Mwanzo ambazo ndiyo zenyé uhaba mkubwa na mahitaji makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa watumishi. Mahakama inaendelea kukabiliwa na uhaba wa watumishi katika kada mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Mahakama ambazo zimeendelea kuongezeka. Mahakama ina uhitaji wa watumishi 4,728 ambapo hadi sasa ina watumishi 5,623 kati ya watumishi 10,351 wanaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kusaidia Mahakama katika kupata watumishi wenye sifa kwa kuipatia kibali cha kuajiri ili kuweza kukidhi mahitaji ya watumishi, hasa ukizingatia utekelezaji wa mradi wa maboresho wa ujenzi wa Mahakama ambao baada ya kukamilika kwake lazima utahitaji watumishi. Suala hili liende sambamba na kuteuliwa kwa Majaji wapya pindi waliopo wanapomaliza muda wao ambapo kwa pamoja hatua hizi zitapunguza mlundikano wa mashauri ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya uhaba wa miundombinu ya Mahakama. Kuna changamoto kubwa ya uhaba na uchakavu wa miundombinu ya Mahakama zinazotokana na ukosefu wa rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama. Kutokana na changamoto hizi, Mahakama inalazimika kukodi majengo ya watu binafsi au ya chama ili kuendesha shughuli zake. Hali hii ni hatari sana kwa chombo kama Mahakama kwa sababu utaratibu huu unahatarisha misingi ya utolewaji wa haki. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kusaidia kuendelea kutenga fedha za maendeleo za ndani za kutosha ili kusaidia kutekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Mahakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Maboresho wa Mahakama. Mahakama

imekuwa ikitekeleza Mradi wa Maboresho wa Mahakama kupitia mkopo kutoka Benki ya Dunia. Aidha, mradi huu, kufika Juni, 2021 utakuwa umefikia ukomo wake na ndiyo sababu ya msingi ya kushuka kwa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ilijulishwa kuwa Serikali inafanya mazungumzo na Benki ya Dunia ili kupata nyongeza ya fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi huo. Kamati inapenda kuisisitiza Serikali kuhakikisha nyongeza hiyo inapatikana ambayo imekuwa msaada mkubwa katika maboresho na ujenzi wa miundombinu ya Mahakama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari. Mahakama imekuwa inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na upungufu wa magari. Baada ya Mahakama kujadiliana na Serikali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali imeuongezea Mfuko kiasi cha Sh. 3,600,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa magari. Hakika nyongeza hii ya fedha itaenda kutatua sehemu ya changamoto hiyo na hivyo kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mahakama. Aidha, kwa kuwa fedha hizi zimetengwa kwenye fedha za maendeleo za ndani, Kamati inaisisitizia Serikali kuhakikisha kuwa fedha zote hizi zinatolewa kama zilivyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya TEHAMA. Kamati inapongeza Mahakama kwa kuanza kutumia mifumo ya TEHAMA katika kusajili na kuratibu mashauri, kusikiliza mashauri, kusimamia Mawakili, kuhifadhi maamuzi ya mashauri mbalimbali ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani na kukusanya maduhuli. Pamoja na mafanikio hayo, bado kasi ya matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kufungua na kusikiliza mashauri ni ndogo. Hivyo, Kamati inaishauri Mahakama kuendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA kwa kutumia wataalam wa ndani ili kuongeza ufunguaji na usikilizaji mashauri kupitia kupitia mifumo ya TEHAMA. Hatua hii itaongeza kasi ya utoaji haki kwa wakati na kusogea huduma za Mahakama karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshwaji wa Mabaraza ya Kata. Serikali iangalie suala la Mabaraza ya Kata kuunganishwa kwenye Mfumo wa Mahakama kwani kumekuwa na udhaifu wa kiutendaji katika kutoa haki na kutatua migogoro. Mabaraza ya usuluhishi yalianzishwa kwa Sheria Na.5 (Sura 216) kwa nia njema ya kusaidia utoaji haki katika maeneo ambayo hayajafikiwa na Mahakama, lakini Mabaraza haya badala yake yamekuwa yakiongoza katika kuwanyima wananchi haki kutockana na baadhi yake kutawala kwa rushwa na kushughulikia kesi ambazo hawana mamlaka ya kisheria ya kuzishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mabaraza haya yanasmamiwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata na miongoni mwa Kanuni za Baraza ni Baraza kuundwa na wananchi wa kawaida tu wasio na uelewa wa sheria, suala ambalo linasababisha haki kutotolewa kwa usawa. Hivyo, Kamati inashauri Mabaraza haya kuunganishwa kwenye Mfumo wa Mahakama na hivyo kuruhusu utoaji haki ikiwa ni pamoja na ukataji rufaa Mahakama ya Mwanzo pindi itakapobidi. Aidha, maboresho haya yafanyike pia kwa Mabaraza mengine yanayotumika kutoa haki, mathalani Mabaraza ya Ardhi ili kuleta haki na usawa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho za Wazee wa Mahakama. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhusu kurejewa upya kwa viwango vya posho za wazee wa Mabaraza ambao wanalipwa Sh. 5,000 tu kwa kesi, kiasi ambacho ni kidogo hasa ukizingatia muda unaochukua kesi kuamuliwa. Hatua hii itasaidia kuziba mianya ya rushwa lakini pia itaongeza motisha, tija na ufanisi katika kazi za Mabaraza husika. Vilevile, matumizi ya wazee hawa katika ngazi za Kata na Mahakama za Mwanzo na baadhi ya mashauri ya Mahakama Kuu yaangaliwe upya ili kuendana na mazingira yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Naomba nihitimishe kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika na wewe kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango,

aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango ambaye sasa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na Ndg. Mathias Kabunduguru, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama walivyoorodheshwa katika Taarifa yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Pia napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, Ndg. Michael Kadebe, kwa kuipatia ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya Sh. 153,228,859,000, kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA
MFUKO WA MAHAKAMA (FUNGU 40) KWA MWAKA WA
FEDHA 2020/21 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 - KAMA
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (1)(c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 pamoja na Kifungu cha 59 cha Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya mwaka 2011, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania ni moja kati ya Mihimili mitatu ya Dola na majukumu yake yameanishwa katika Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kama chombo kikuu cha kusimamia utolewaji wa Haki nchini. Hivyo, ni wazi kwamba chombo hichi ni muhimu sana katika ustawi wa jamii na maendeleo endelevu. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara 107(A)(1) Mahakama ndio chombo pekee chenye mamlaka ya mwisho katika kutoa haki kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Mfuko wa Mahakama kuanzia Mwezi Julai, 2020 hadi Mwezi Februari, 2021, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu

yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2021/22.

2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2020/21 Mfuko wa Mahakama – **Fungu 40** uliidhinishiwa na Bunge jumla ya Sh. **176,437,977,000.00**. Kati ya fedha hizo **Sh. 50,543,824,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama (PE), **Sh. 2,264,771,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto (IJA), **Sh. 53,754,382,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na **Sh. 69,875,000,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Maendeleo, **Sh. 39,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh. 30,875,000,000.00** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2021, Mahakama ilipokea jumla ya **Sh. 114,466,996,766.79** ambazo ni sawa na **asilimia 64.88** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2020/21. Kati ya fedha hizo, **Sh. 35,836,254,666.64** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **Sh. 32,731,249,044.00** kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama, **Sh. 1,272,370,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto (IJA) na **Sh. 44,627,123,056.15** ni fedha za maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 23,547,403,186.40** ni fedha za ndani na **Sh. 21,079,719,869.75** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2020/21 ulipanga kukusanya maduhuli ya **Sh. 12,571,199,000** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2021 kiasi kilichokuwa kimkusanywa ni **Sh. 5,619,786,196.72** ikiwa sawa na **asilimia 45** ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama hadi kufikia mwezi Februari, 2021 ni wa kuridhisha, ambapo Serikali kwa kiasi kikubwa imekuwa inatoa fedha kwa Mahakama kama zilivyoidhinishwa na

Bunge na hivyo kuwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake. Mwenendo huu unaonyesha hadi kufikia mwezi Juni, 2021 Fungu hili linaweza kuwa limepokea Bajeti katika asilimia **80 hadi 90**. Aidha, pamoja na mwenendo huu bado jitihada kubwa zinahitajika za rasilimali fedha ili kuhakikisha kuwa Mahakama inafikia malengo yake ya utoaji wa huduma pamoja na ujenzi wa miundombini yake. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa Mahakama inaendelea kuidhinishiwa Bajeti inayokidhi mahitaji yake.

Jedwali Na. 1. Mwenendo wa Bajeti wa Mfuko wa Mahakama

Matumizi	Bajeti	Fedha zilizotolewa Hadi Februari	Asilimia ya Bajeti
Mshahara	50,543,824,000	32,731,249,044	64.8
Mshahara (UA)	2,264,771,000	1,272,370,000	56.2
Matumizi Mengineyo	53,754,382,000	35,836,254,666.64	66.7
Maendeleo (a+b)	69,875,000,000	44,627,123,056.15	63.9
a Fedha za Ndani	39,000,000,000	23,547,403,186.40	60.4
b Fedha za Nje	30,875,000,000	21,079,719,869.75	68.3
Jumla Kuu	176,437,977,000.	114,466,996,766.79	64.88

3.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mahakama katika kutekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia utoaji haki kwa wakati nchini, ilijiwekea vipaumbele mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuharakisha usikilizaji wa mashauri; kuimarisha utawala bora, maadili na uwajibikaji; kuboresha mazingira ya kufanya kazi; kujenga miundombini na kuongeza matumizi ya TEHAMA ili kupeleka huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza vipaumbele hivyo, mafanikio yaliyofikiwa na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2020/21 ni kama ifuatavyo:-

- a) Kumalizika mashauri 159,153 yaliyokuwa yamesajiliwa mwanzoni mwa mwezi Julai, 2020 hadi Februari, 2021.
- b) Kusikiliza mashauri 7,968 kwa njia ya Video Conferencing na kufanikiwa kuokoa **Sh. 796,681,486** kwa upande wa Mahakama na **Sh. 120,016,093** kwa upande wa Jeshi la Magereza.
- c) Kumaliza usikilizaji wa mashauri 192 kwa Mahakama inayotembea (Mobile Courts) katika mikoa ya Mwanza na Dar-es-salaam.
- d) Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji Maduhuli ya Serikali kuititia mfumo wa GePG.
- e) Kufanya Ulaguzi wa Mahakama nchi nzima, ambao ulibaini masuala mbalimbali ambayo yamepatiwa ufumbuzi na mengine kuwekewa mikakati ya muda mfupi na muda wa kati kwa ajili ya utekelezaji.
- f) Kuendelea kuboresha Mfumo wa Kielekitroniki wa Kusajili na Kuratibu Mashauri (Judiciary Statistics Dashboard System II), ambao unawezesha mawasiliano na wadau wa Mahakama kwa kuwawezesha kupata mawasiliano kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi na barua pepe, hivyo kutohitajika kufika mahakamani shauri linapoahirishwa. Vilevile, Mfumo umerahisisha Malipo ya Ankara kwa kuunganishwa na Mfumo wa Ulipaji wa Serikali (GePG).
- g) Kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu kanda za Kigoma na Musoma.
- h) Kukamilika kwa ukarabati wa Mahakama Kuu kanda ya Sumbawanga. Kuendelea kukamilisha ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi za Katavi, Lindi; Mahakama za Wilaya za Bahi na Chemba; na Mahakama za Mwanzo za Kibaigwa, Mlimba na Mang'ula.
- i) Kuendelea kukamilisha ujenzi wa vituo jumuishi vya kutolea haki katika mikoa ya Arusha, Morogoro, Mwanza, Dodoma, Dar es Salaam (Kinondoni na Temeke).

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2020/21, Mahakama inaendelea kukabiliwa na **changamoto** zifuatazo:-

- i. Uhaba wa Mahakama za Mwanzo, ambazo ndio ngazi ya chini kabisa katika muundo wa Mahakama yenye mamlaka ya kushughulikia mashauri ya jinai, madai, ndoa na usimamizi wa mirathi pamoja na rufaa kutoka mabaraza ya kata;
- ii. Upungufu wa watumishi kwa kada mbalimbali ikilinganishwa na mahitaji;
- iii. Changamoto ya Ucheleweshaji wa Mashauri bado ipo, hususani mashauri yanayohusu masuala ya biashara, mikopo, kesi za rufaa za kodi, rushwa, uhujumu uchumi na mashauri ya ardhi ambayo yanazorotesha ukuaji wa uchumi wa nchi.
- iv. Uchache na uchakavu wa Miundombinu ya Mahakama hususani Majengo ya Ofisi na Makazi ya Majaji na Watumishi;
- v. Uhaba wa vitendea kazi, hususani Magari kwa ajili ya shughuli za Ukaguzi wa mahakama zote nchini; na
- vi. Ukuaji mdogo wa matumizi ya TEHAMA katika kuongeza kasi ya usikilizaji wa kesi na uwekaji mzuri wa kumbukumbu. Aidha, katika kipindi cha mwaka jana ni mashauri 2435 tu yalifunguliwa kwa kielektroniki.

4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa Fedha 2021/22, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na malengo ya mpango mkakati na ya kitaifa. Aidha, maeneo ambayo yamepewa kipaumbele ni yafuatayo: -

- a) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashahuri ya muda mrefu (backlog);

- b) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji huduma;
- c) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;
- d) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;
- e) Kuanza kwa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania ili kuhamia Dodoma; na
- f) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki.

4.1. Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2021/22

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2021/22 Mfuko wa Mahakama umepewa ukomo wa jumla ya **Sh. 153,228,859,000**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 53,066,756,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama, **Sh. 2,197,721,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, **Sh. 57,774,382,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo (OC) na **Sh. 40,190,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 39,100,000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 1,090,000,000** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya fungu hili imepungua kwa **shilingi 23,209,118,000.00** ukilinganisha na mwaka wa fedha 2021/22 kutokana na fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya kesi na mapingamizi wakati wa uchaguzi wa mwaka 2020 pamoja na Fedha za maendeleo kutoka nje kupungua kutokana na kukoma kwa Mradi wa Maboresho ambao uliokuwa unafadhiliwa na fedha za Mkopo kutoka Benki ya Dunia. Hata hivyo, Mahakama inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia ii kuona uwezekano wa kuendelea kupata fedha hizo kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mashauriano kati, Mahakama na Waziri wa Fedha na Mipango, Mahakama ilipewa

nyongeza ya fedha ya jumla ya **Sh. 7,600,000,000** katika ukomo wa awali. Kati ya fedha hizo, **Sh. 4,000,000,000** zilizongezwa kwenye Bajeti ya Matumizi Mengineyo ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2020/21. Nyongeza hiyo ni kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zilizopo ikiwemo kugharamia uendeshaji wa vituo vipyta ya Mahakama Kuu na Mahakama za Wilaya pamoja na uhamisho wa watumishi waliokaa katika kituo kimoja kwa muda mrefu. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Mahakama iliongezewa **Sh. 3,600,000,000** kwenye fedha za ndani ikilinganishwa na ukomo ultolewa ikiwa ni mahsusni kwa ununuzi wa magari. Nyongeza hiyo ya kibajeti nje ya ukomo ulifikiwa ili kutatua changamoto za kibajeti zinazoikabili Mahakama.

4.2. Maduhuli

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato katika mwaka wa fedha 2021/22 Mahakama imepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh. 12,571,199,235**.

5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

5.1. Uhaba wa Mahakama za Mwanzo

Mheshimiwa Spika, kati ya changamoto inazozikabili Mahakama ni pamoja na uhaba wa Mahakama za Mwanzo. Kimuundo kila Kata nchini inatakiwa kuwa na Mahakama ya mwanzo. Hata hivyo, mpaka sasa kati ya Kata **3963** zilizopo kuna Mahakama za mwanzo **960** tu na zinazofanya kazi ni **799** tu. Nyingine hazifanyi kazi na kufungwa kutokana na uchakavu wa majengo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kasi ndogo ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika kila Kata kutoptaka na changamoto ya rasilimali fedha, Mahakama imechukua uamuzi wa kuanza na ujenzi wa Mahakama katika kila Tarafa uamuzi ambao ni wa busara. Matarajio ya Mpango ujao ni kujenga Mahakama za Mwanzo katika **Tarafa 142** kati ya **Tarafa 570** zilizopo nchini hii inashiria bado kutakuwa na changamoto ya mahakama ukilinganisha na mahitaji. Aidha, Kamati inaishauri Mahakama wakati wa ujenzi huu katika Tarafa ujenzi uzingatia idadi ya watu katika tarafa husika,

umbali kati ya tarafa, shughuli za kiuchumi na tarafa lakini pamoja na ukubwa wa mashauri yanayoshughulikiwa na Mahakama hizo ili ujenzi huo uwe na tija na kuondoa adha kwa wananchi. Hivyo, ushirikiano kati ya Muhimili wa Mahakama, Ofisi ya Rais Tamisemi na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ni wa muhimu na lazima ili kuhakikisha viashiria hivyo muhimu vinazingatiwa. Vilevile, kipaumbele kitolewe katika ujenzi wa hizi Mahakama za Mwanzo ambazo ndio zenyе uhaba mkubwa na mahitaji makubwa.

5.2. Uhaba wa Watumishi

Mheshimiwa Spika, Mahakama inaendelea kukabiliwa na uhaba wa watumishi katika kada mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Mahakama ambazo zimeendelea kuongezeka. Mahakama ina uhitaji wa **watumishi 4,728** ambapo hadi sasa ina **watumishi 5,623** kati ya **watumishi 10,351** wanaohitajika. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuisaidia Mahakama katika kupata watumishi wenyе sifa kwa kuipatia Mahakama kibali cha kuajiri ili kuweza kukidhi mahitaji ya watumishi hasa ukizingatia utekelezaji wa mradi wa maboresho wa ujenzi wa Mahakama ambao baada ya kukamilika kwake lazima utahitajii watumishi. Suala hili liende sambamba na kuteuliwa kwa majaji wapya pindi waliopo wanapomaliza muda wao ambapo kwa pamoja hatua hizi zitapunguza mlundikano wa mashauri ya muda mrefu (back logs).

5.3. Changamoto ya Uhaba wa Miundombinu ya Mahakama

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto kubwa ya uhaba na uchakavu wa miundombinu ya Mahakama zinazotokana na ukosefu wa rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama. Kutokana na changamoto hizi Mahakama inalazimika kukodi majengo ya watu binafsi au ya Chama ili kuendesha shughuli zake. Hali hii ni hatari sana kwa chombo kama Mahakama kwa sababu utaratibu huu una harisha misingi ya utolewaji wa haki. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kusaidia kuendelea kutenga fedha za maendeleo za ndani za kutosha ili kusaidia kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Mahakama.

5.4. Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Mradi wa Maboresho wa Mahakama

Mheshimiwa Spika, Mahakama imekuwa ikitekeleza Mradi wa Maboresho wa Mahakama kuitia mkopo kutoka Benki ya Dunia. Aidha, Mradi huu kufika Juni, 2021 utakuwa umefikia ukomo wake na ndio sababu ya msingi ya kushuka kwa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama ya mwaka 2021/22. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa Serikali inafanya mazungumzo na Benki ya Dunia ili kupata nyongeza ya fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi huo. Kamati inapenda kuisisitiza Serikal kuhakikisha nyongeza hiyo inapatikana ambayo imekuwa msaada mkubwa katika maboresho na ujenzi wa miundombinu ya Mahakama nchini.

5.5. Nyongeza ya Fedha kwa ajili ya Ununuzi wa Magari

Mheshimiwa Spika, Mahakama imekuwa inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vitendea kazi lkiwa ni pamoja na upungufu wa magari. Baada ya Mahakama kujadiliana na Serikali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2021/22, Serikali imeuongeza Mfuko kiasi cha **Sh. 3,600,000,000** kwa ajili ya ununuzi wa magari. Hakika nyongeza hii ya fedha itaenda kutatua sehemu ya changamoto hiyo na hivyo kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mahakama. Aidha, kwa kuwa fedha hizi zimetengwa kwenye fedha za maendeleo za ndani, Kamati inaisisitiza Serikali kuhakikisha kuwa fedha zote hizi zinatolewa kama zilivyoidhinishwa.

5.6. Matumizi ya TEHAMA

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Mahakama kwa kuanza kutumia Mifumo ya TEHAMA katika kusajili na kuratibu mashauri (JSDS II), kusikiliza mashauri (Video Conferencing), kusimamia Mawakili (TAMS), kuhifadhi maamuzi ya mashauri mbalimbali ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani (Kanzidata ya TanzLii) na kukusanya maduhuli (GePG). Pamoja na mafanikio hayo, bado kasi ya matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika kufungua na kusikiliza mashauri ni ndogo. Hivyo, Kamati inaishauri Mahakama kuendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA kwa kutumia wataalamu wa ndani ili kuongeza ufunguaji na usikilizaji mashauri kuitia kuitia mifumo ya TEHAMA. Hatua hii itaongeza kasi ya utoaji haki

kwa wakati na kusogeza huduma za Mahakama karibu zaidi na wananchi.

5.7. *Uboreshwaji wa Mabaraza ya Kata*

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie suala la Mabaraza ya Kata kuunganishwa kwenye Mfumo wa Mahakama kwani kumekuwa na udhaifu wa kiutendaji katika kutoa haki na kutatua migogoro. Mabaraza ya usuluhishi yalianzishwa kwa Sheria namba 5 Sura 216 kwa nia njema ya kusaidia utoaji haki katika maeneo ambayo hayajafikiwa na mahakama lakini mabaraza haya badala yake yamekuwa yakiongoza katika kuwanyima wananchi haki kutokana na baadhi yake kutawala kwa rushwa na kushughulikia kesi ambazo hawana mamlaka ya kisheria ya kuzishughulikia. Aidha, mabaraza haya yanasmamiwa na kamati ya maendeleo ya kata na mionganoni mwa kanuni za baraza ni baraza kuundwa na wananchi wa kawaida tu wasio na uelewa wa sheria suala ambalo linapelekeea haki kutotolewa kwa usawa. Hivyo, Kamati inashauri Mabaraza haya kuunganishwa kwenye Mfumo wa Mahakama na hivyo kuruhusu utoaji haki ikiwa ni pamoja na ukataji rufaa Mahakama ya Mwanzo pindi itakapobidi. Aidha, maboresho haya pia yafanyike pia kwa mabaraza mengine yanayotumika kutoa haki mathalani Mabaraza ya Ardhi ili kuleta haki na usawa kwa wananchi.

5.8. *Posho za Wazee wa Mahakama*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhusu kurejewa upya kwa viwango vya posho za wazee wa mabaraza ambaao wanalipwa **shilingi 5,000 tu** kwa kesi, kiasi ambacho ni kidogo hasa ukizingatia muda unaochukua kesi kuamuliwa. Hatua hii itasaidia kuziba mianya ya rushwa lakini pia itaongeza motisha, tija na ufanisi katika kazi za Mabaraza husika. Vilevile, matumizi ya Wazee hawa katika ngazi za Kata na Mahakama za Mwanzo na baadhi ya mashauri ya Mahakama Kuu yaangaliwe upya ili kuendana na mazingira yaliyopo.

6.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango ambaye sasa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda, (Mb), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na Ndg. Mathias Kabunduguru Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

- | | |
|--|--------------|
| 1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Shallly Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. Mhe. Subira Khamis Mgaliu, Mb | Mjumbe |
| 11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb | Mjumbe |
| 12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb | Mjumbe |
| 14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |

17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Halima James Mdee, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe kwa kuipatia ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 jumla ya **Sh. 153,228,859,000** kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

Sillo Daniel Baran (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

28 Aprili, 2021

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshamaliza mawasilisho. Sasa ninayo majina hapa ya Wabunge mbalimbali ambao wameomba kuchangia; tutaanza na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati ajiandae.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja ya Wizara ya Katiba na Sheria. Nianze kwa kuishukuru na kuipongeza sana Wizara kwa wasilisho zuri, nina imani kabisa kwamba mwalimu wangu, Mheshimiwa Prof. Kabudi, pamoja na timu yake, watakwenda vizuri katika kuiendesha Wizara hii ambayo inabeba sehemu kubwa sana ya maisha ya kila siku ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia Wizara ya Katiba na Sheria kwa ajili ya maboresho mbalimbali ambayo yamefanyika ya kutenganisha ile Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka. Naamini kabisa kwamba hatua hii italeta ufanisi mkubwa sana kwa sababu itakuwa imepunguza mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia maboresho ya miundombinu ya Mahakama, hasa suala la majengo. Nadhani tumemaliza wakati ule sasa wa kuona kwamba Mahakama lazima zikae kwenye majengo machakavu na yaliyochoka, sasa yanajengwa majengo mazuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru hata katika Jimbo langu la Mwanga ujenzi wa Mahakama ya Wilaya umeanza, tunasubiri sasa kama ambavyo wenzetu wa Kamati ya Bajeti wameomba kwamba sasa Mahakama za Mwanzo ziboreshwewe kwa sababu ndiyo zipo karibu zaidi na wananchi. Hivi sasa kwa vile Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanapelekwa wale wenye shahada, naamini kabisa mambo sasa yatakwenda vizuri na Mawakili watakwenda, haki itatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado ziko changamoto na malalamiko mengi sana juu ya suala zima la utoaji haki, hasa katika maeneo haya ambayo yamekuwa yakilalamikiwa ya watu kuwa na kesi ambazo hazina dhamana na hizi kesi za utakatishaji fedha ambazo watu wengi wanazilalamikia. Mara nydingi malalamiko haya yanapotokea watu wanalaumu kwamba sheria ni mbovu

lakini kuna wakati fulani Mheshimiwa Jaji Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Barnabas Samatta, aliwahi kusema kwamba tunahitaji zaidi Mahakama imara kuliko sheria kali. Sheria zinaweza zikawa kali sana lakini kama hatuna Mahakama ambayo iko thabitii ikatusumbua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama yetu ni nzuri, ina uwezo mkubwa sana na mimi nimefanya nao kazi muda mrefu lakini hapa katikati Mahakama yetu imeingiwa na katatizo fulani, Mahakama yetu imeishiwa na wivu. Nasema hivyo kwa sababu wote waliosoma sheria wanafahamu iko kanuni moja inayotumika katika sheria inasema kwamba *The Court must be jealous of its jurisdiction* (Mahakama lazima iwe na wivu na mamlaka yake). Hata hivyo, hapa katikati Mahakama imekosa wivu na mamlaka yake, imeachia mamlaka yake ifanywe na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta shauri linakuja Mahakamani, ile Sheria ya Utakatishaji Fedha inasema kabisa kwamba lazima kuwe na kosa la msingi halafu ndiyo la *money laundering* lifuate. Hata hivyo, shtaka la *money laundering* linakuja, Mahakama inaona kabisa kwamba hapa siyo sahihi na wale washtakiwa wanalia na kuomba kwamba jamani mbona hapa hakuna kesi ya *money laundering*, lakini zinaendelea na zinaendelea kuumiza watu. Ukweli wa mambo ni kwamba Mahakama hapa inatakiwa ikae kwenye sehemu yake ili twende mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 107A ya Katiba ya Jmahuri ya Muungano wa Tanzania, imeipa mamlaka Mahakama kuwa ndiyo yenye kauli ya mwisho pale ambapo kunakuwa na jambo lolote linalolalamikiwa. Sasa Mahakama irudi kwenye nafasi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala hili kwa mfano la *certificate* ya *DPP* inayozuia dhamana. Mahakama inafahamu kabisa kwamba mkija Mahakamani watu wawili, mmoja ni *DPP* ambaye ni mshtaki na mshatakiwa, hawa watu wote wawili wako sawa mbele ya Mahakama ili iwaamulie shauri lao. Sasa mmoja anatoa wapi mamlaka ya kumzuia

mwenzake asipate dhamana kwa *certificate*? Yule analalamika kwamba jamani huyu mwenzangu ni *party*, yaani amekuja mbele ya Mahakama kama mimi; anapata wapi ye ye mamlaka ya kunizua mimi dhamana kwa *certificate*? Sheria kweli inaweza ikawa inampa mamlaka lakini sheria inayompa mamlaka haizidi Katiba, Mahakama bado ina uwezo kabisa wa kuingilia kati na kusimama kwenye nafasi yake na kuweza kutenda haki. Sisemi kwamba lazima wapewe dhamana, lakini kama wananyimwa wanyimwe na Mahakama.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tadayo.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, naam.

NAIBU SPIKA: Kaa kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, napata changamoto kidogo na mchango wako maana unauzungumzia Mhimili wa Mahakama na kwamba kuna mambo mhimili ule haufanyi sawasawa. Sasa kwa taratibu tulizonazo humu ndani, Serikali huwa inasemwa kwa sababu inao hapa watu wa kuisemea, sasa tukiingia huko kwenye kuisema Mahakama kwa namna ambavyo unachangia, ni tofauti na kama ungekuwa unatoa ushauri kwamba kuna jambo fulani labda unaona liko hivi.

Kwa sababu ikiwa kuna watu ambao wameonewa na Mahakama wote tunafahamu utaratibu; unakata rufaa kulekule Mahakamani. Kwa sababu ukileta kesi ambayo iko kule, mtu hakutendewa haki kule, ukileta hapa Bungeni, hapa Bungeni siyo chombo ambacho Kikatiba kimewekwa kusikiliza mashauri ambayo Mahakama haijafanya sawasawa.

Sisi wenyewe tumeapa hapa kuilinda Katiba, kwa hiyo, kama ambavyo sisi Wabunge hatutegemewi huko nje tukaanzze kujadiliwa kwa namna fulani hivi, ni vilevile mihimili

mingine pia haiyumkiniki. Kama sheria ina shida, ni kazi yetu sisi kubadilisha sheria, siyo kazi ya Mahakama, ni kazi yetu sisi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Tadayo, mwanasheria mbobezi kabisa, hebu jielekeze mchango wako kwa mipaka ile ambayo tunawekewa na Katiba yetu.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maelekezo yako na nayapokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia, nilishawahi kulitaja tena hapa Bungeni ni juu ya suala la Wizara mbili kuzungumza, Wizara ya Sheria na Wizara ya Ardhi ili Mabaraza yale ya Ardhi yaweze kurudi chini ya Mhimili wa Mahakama. Nasema hivyo kwa sababu ukienda Mahakama Kuu, pamoja na kwamba kuna Kitengo cha Ardhi ambacho kilianzishwa lakini pia Mahakama Kuu hii ya kawaida inapokea mashauri ya ardhi. Sasa tunapata changamoto kwenye zile Wilaya ambazo hazina Mabaraza ya Ardhi ambazo ni nydingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba Wizara hizi mbili zizungumze ili mashauri ya ardhi yaweze kusikilizwa kwenye Mahakama za kawaida kupunguza mzigo mkubwa wa mashauri ya ardhi ambayo ndiyo yanayoleta matatizo na changamoto nydingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikifika hapo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja; ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilishamtaja Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza ajiandae.

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kwanza kukishukuru Kiti chako. Vilevile naomba nishukuru Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuweza kuwasilisha kwetu hapa bajeti

hii ambayo ndani yake mna changamoto nyingi, lakini naamini Bunge hili ndiyo sehemu sahihi kwa ajili ya kupatia ufumbuzi baadhi ya matatizo yao mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaapishwa hapa ulitukabidhi Katiba na Katiba hii kabla ya kuikabidhiwa tulikula kiapo. Maana yake kama sikosei ni wajibu wa Bunge hili, kwa sababu Katiba hii inako ilikotoka mpaka ikaja hapa pamoja na changamoto zote, lakini kubwa ni kwamba tuliapa kuilinda Katiba hii, nadhani mwenyewe umesema hivyo.

Kwa hiyo, mimi naomba kwa wenzetu wa Wizara ya Katiba na Sheria, mimi si mwanasheria *by profession* lakini najaribu kuisoma hii kwa sababu ushauri wako umesema someni, someni, someni, nilikuwa najaribu kuangalia hasa vitu vinavyoitwa changamoto na hapa nataka njielekeze kwenye changamoto za mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ikikupendeza ninukuu Katiba yako hii kwenye Sura ya Saba, Sehemu ya Kwanza na Sehemu ya Pili. Inasema: "Sehemu ya Kwanza, Mchango na Mgawanyo wa Mapato ya Jamhuri ya Muungano".

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zahor, tusomee Ibara.

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara inasema...

NAIBU SPIKA: Ibara namba ngapi?

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 133.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu, inasema hivi: "133. Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti maalum itakayoitwa "Akaunti ya Fedha ya Pamoja"..." Naomba kuishia hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba twende kwenye Sehemu ya Pili, Ibara ya 135, inasema: "135.-(1)Fedha zote zitakazopatikana kwa njia mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isipokuwa fedha za aina iliyotajwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara hii, zitawekwa katika mfuko mmoja maalum ambao utaitwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali." Naomba niishie hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yangu ni nini? Nimesema tulikubaliana kuilinda Katiba hii, ombi langu kwa wenzetu wa Wizara ya Katiba na Sheria; nimekuwa nikifuatilia na nikisikiliza maeneo mengi sana ibara hizi kila siku vinapigiwa kelele. Kwa hiyo, naomba Kiti chako na Bunge lako, endapo tutaona kwamba ibara hizi ni tatizo tokea Katiba hii imetengenezwa na ibara hizi kuwekwa kama sikosei ni mwaka 1984, maana yake tunalo tatizo sisi wenyewe kama Bunge kutokusimamia Katiba ambayo tumeapa kuilinda; ombi langu kwako, tulinde Katiba hii; hilo la kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, nimefuatilia mijadala mingi kuanzia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mpaka hotuba ya leo ya kaka yangu, Mheshimiwa Prof. Kabudi, lakini nimefuatilia michango ya Waheshimiwa Wabunge, wengi wakizungumzia juu ya ukosefu wa fedha za vitendea kazi na ukosefu wa fedha za maendeleo kwenye maeneo mbalimbali.

Sasa ambalo nimeliona kwa haraka haraka, inawezekana nitakosea mtanisahihisha, kubwa ni kwa sababu sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano tumeacha kufanya kazi yetu ya kuilinda Katiba hii ya kwamba ni kusimamia na kuishauri Serikali. Ndiyo maana tumeiacha Wizara ya Fedha kuchukua nafasi kubwa ya Serikali Kuu wenyewe kuamua nini ifanye nini isifanye. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ambalo nimeliona kwa haraka haraka, inawezekana nakosea, mtanisahihisha; kubwa ni kwa sababu sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano tumeacha kufanya kazi yetu ya kuilinda Katiba hii ya kwamba ni kusimamia na kuishauri Serikali. Ndiyo maana

tumeiacha Wizara ya Fedha kuchukua nafasi kubwa ya Serikali Kuu yenyewe ya kuamua nini ifanye nini isifanye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapitisha bajeti hapa kama Wabunge, lengo letu na imani yetu ni kwamba tunakwenda kutekeleza kitu ambacho tumekipanga. Sasa ushauri wangu ni mdogo tu, kwamba kwa sababu Katiba hii imetupa nafasi ya kuunda *Joint Financial Account* na *Joint Financial Committee*. Ombi langu ni kwamba turudi kwenye *basics* hizi za sheria, kwamba Katiba hii tukiisimamia Wizara ya Fedha ifanye kazi zake mbili tu; moja, kutengeneza *policy* ambayo itatuwezesha kutafuta fedha na pili, ifanye kazi ya kukusanya fedha, *period*. Ili tuwaondolee wenzenetu wa fedha makelele kwamba hamtupi, hampendi, hamtaki. Siyo kama hawapendi, lakini fedha haitoshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Bunge hili lifanye kazi yake ya kusimamia na kushauri ili liwe na nafasi ya kuweza kusema; kwa sababu nadhani tunayo *Appropriation Committee* hapa, sasa hii ifanye kazi ya kusema tumekusanya mbili; hizi zitakuwa za kazi hii na hizi zitakuwa na kazi hii. Wizara ya Fedha ifanye kazi zake mbili tu ya kutengeneza *policy* na kukusanya fedha ili Bunge hili liamue kwamba fedha hizi zitumike kwa aina eneo gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza na Mheshimiwa Restituta Taska Mbogo, ajiandae.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kuhusiana na hoja iliyopo mbele yetu. Nianze kwanza kwa kumpongeza Waziri wa Sheria na Katiba pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wote wa Mahakama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kupongeza Bunge lako, kukpongeza wewe na Mheshimiwa Spika kwa ajili ya kutunga Sheria ya Matumizi ya Kiswahili katika Mahakama zetu na vyombo vingine vya utoaji haki. Kwa kweli kutunga sheria huku kumesaidia sana wananchi wengi kupata haki kwa sababu wengi walikuwa wanahukumiwa kwa kutojua tu lugha inayozungumziwa katika Mahakama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie kuhusiana na kesi za ubakaji hasa katika Mkoa wetu wa Iringa. Tuna kesi zaidi ya 400 katika mkoa wetu, lakini naona zinachukua muda mrefu sana. Nilikuwa najiuliza ni kwa nini kesi hizi zisiwe na *limit*? Kwa sababu kuna nydingine ambazo zinakuwa tayari zimeshakuwa na vidhibiti, lakini tunaona kwamba zinachukua muda mrefu. Kesi hizi zimekuwa zikiwadhalilisha sana watoto na hata akina mama wanaobakwa, kwa sababu zimekuwa zinanyima hata haki zao za binadamu kwa kuchukua muda mrefu. Sasa naona ifike sehemu ziwe na *time limit*. Ziwekewe *limit* za kuhukumiwa hizi kesi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie kuhusiana na msaada wa kisheria. Pamoja na kuwa nimeona kwamba limezungumziwa katika hotuba ya Waziri, lakini bado msaada wa kisheria umekuwa ukiwanyima wananchi wanaoshindwa kuweka Wakili kwa ajili ya kupatiwa haki. Sasa tulipitisha hapa Bungeni kwa nia nzuri kabisa na tulikuwa tunajua kwamba baada ya kupitisha, zile changamoto pengine zingeweza kukamilika kwa wakati, lakini unaona bado kabisa wananchi wanakosa msaada wa kisheria na wanakosa haki zao na kwa sababu wanashindwa kuweka Wakili kwa ajili ya kuwatetea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tathmini ifanyike katika mikoa na hasa sehemu ambazo zina kesi nydingi, kwa mfano mkoa wetu wa Iringa ambao una kesi nydingi sana na tunaona kuna mashirika ambayo yanasaidia msaada wa kisheria, lakini bado wananchi wanalamika kwa kukosa haki kwa kutokuwa na Wakili wa kuwatetea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pale Mkoani kwetu Iringa kuna changamoto. Tuna kesi nyngi sana za mauaji ambazo kutokana na kutokuwa na fungu la kutosha kuendesha hizi kesi, basi unaona wale wafungwa kule mahabusu wanaka muda mrefu, kesi hazikamiliki. Naomba kesi za mauaji pia zipewe kipaumbele, fungu lipelekwe ili zihukumiwe haraka. Kama mtu amefanya kosa, basi aweze kuhukumiwa na kama hana hatia aweze kuondolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie pia kuhusiana na sheria kandamizi kwa wanawake. Wanawake wengi wanakandamizwa sana kwenye mambo ya mirathi, ndoa, talaka; maeneo haya matatu tunaona yanaongoza, hasa kuna sheria tatu. Kwanza, kuna sheria ambayo tumekuwa tukiitunga hapa Bungeni kuna sheria nyngine ni za kidini na sheria za kimila.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria za Bunge siyo mbaya sana, lakini sheria za kidini sitaki kuzisema kwa sababu zenyewe zinaenda kiimani zaidi. Sheria ambazo ni kandamizi ni hizi za kimila kwa sababu zinafuata mfumo dume kwa kuwa zimejikita sana katika mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalni je, Sheria za Kimila haziwezi kurekebishwa ziendane na wakati? Ni dhahiri kuwa Sheria hizi za Kimila utaona nyngi sana zinafafana, yaani hazipo *uniform* katika kila maeneo. Kwa kutambua hilo, nafikiri sheria zilizoingizwa kwenye sheria ya kimila ndani ya mfumo wa Sheria za Tanzania (*Judicature and Application of Laws Act*) ya 11 na 12 zimeeleza kwamba Halmashauri za Wilaya ziwe na utaratibu wa kupitia hizi sheria na maeneo ya halmashauri zao, lakini tunaona bado halmashauri nyngi hazijaweza kuzipitisha hizi sheria za kimila. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona sasa wanawake wengi sana na hata watoto wanapata shida kwa sababu sheria hii bado hajjaweza kupitiwa ili iendane na mila na desturi ambazo wananchi tumo. Je, sasa ni lini Waziri wa Sheria ataweka huu mfumo kwamba ziweze kupita katika

halmashauri zetu ili zitendr haki kwa wananchi ambao tunaoishi nao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja kuhitimisha hoja yake hapa, atueleze kwa sababu hizi Sheria za Kimila zimekuwa zikimkandamiza sana mwanamke kwenye mambo mengi, kwenye mirathi na mambo mengi sana. Kwa hiyo, naomba atakapokuja hapa kutuelezea, aelezee kuhusiana na hii Sheria ya Kimila kuingizwa katika sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nielezee kuhusiana na uadilifu wa kutoa haki katika vyombo vyta haki. Ni muhimu sana na ninaomba suala hili liende moja kwa moja na maboresho ya maslahi ya wafanyakazi au Mahakimu ambao wanahukumu kesi zetu. Tunaona kwamba watumishi wa kada hii ya sheria au Mahakimu ni muhimu wakaboreshewa, hata alivyokuwa anaelezea Mwenyekiti wa Katiba na Sheria ameona kuna tatizo kwamba bado hawajaboreshewa maslahi yao. Sasa inakuwa ni shida sana kutenda haki kama Mahakimu wenyewe. Wanahukumu kesi za mabilioni ya fedha lakini wao wenyewe bado hawana mshahara wa kutosha, pengine bado hata mazingira yao hayako vizuri, ni rahisi sana kuweza kukubaliana kuchukua rushwa na kutotenda haki kwa yule mtu wanayemhukumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nielezee kuhusu miundombinu na maboresho katika Mahakama hasa ya Mwanzo. Mahakama za Mwanzo kwa kweli katika sehemu nyingi, hata katika Mkoa wetu wa Iringa zina hali mbaya sana. Mahakama za Mwanzo nyingi wamepangisha au nyagine zina majengo ambayo siyo mazuri. Kwa hiyo, naomba kuwepo na maboresho makubwa katika Mahakama zetu za Mwanzo kwa sababu ndicho chombo cha kwanza ambacho mwananchi anakwenda kudai haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta Mahakama ina nyufa, hata anaye hukumiwa anaweza akafiri jengo linaweza likambomokea wakati wowote hata bado haki haijatolewa. Kwa hiyo, ni muhimu sana hizi Mahakama zikaboreshwa kwa

sababu ndizo Mahakama ambazo mwananchi anakwenda kudai haki yake na ni Mahakama ya Mwanzo kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa kuja kuboresha hasa Mahakama zetu za Mkoa wa Iringa ambazo nyingi kabisa zipo katika hali mbaya na kwa kweli ni kitu ambacho naomba kizingatiwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya niliyozungumza, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, atafuatiwa Mheshimiwa Restituta Taska Mbogo na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, ajiandae.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami kwa uchache niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Katiba na Sheria. Mchango wangu utajikita katika mafungu mawili tu, kwa maana ya Fungu la 59 na Fungu la 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Magereza yetu nchini kumekuwepo na changamoto kubwa ya mlundikano wa wafungwa pamoja na mahabusu. Mlundikano huu siyo kwamba Tanzania tuna wahalifu wengi sana, siyo kwamba Watanzania hatutekelezi sheria ambazo tunaelekezwa. Sababu kubwa sana ya milundikano ni kwa sababu kesi au tuseme mashauri yanachukua muda mrefu sana kufanyiwa upelelezi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mlundikano huu, wakati mwengine mahabusu yanazidiwa nguvu na kupelekeea watoto wa chini ya miaka 18 kwenda kuungamanishwa au kuchanganywa katika Magereza au Mahabusu ya Watu Wazima. Inawezekana ikaonekana kwamba ni maajabu ninaposema kwamba inafika wakati watoto wa chini ya miaka 18 wanawekwa pamoja na mahabusu watu wazima, lakini hii inatokea kwa sababu kama mahabusu yamezidiwa na kuna watoto ambao wanapaswa

kuingia mle ndani, *automatically* kwa sababu mabweni hayatoshi, tutajikuta watoto wetu wanaingizwa, wanachanganya na watu wazima na mwisho wa siku wanajifunza tabia mbaya ambazo hawakuungia nazo katika yale Magereza au Mahabusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nydingine inayopelekea mlundikano mwingi katika Magereza haya ni kwa sababu kumekuwepo na kubambikiziwa kesi nydingi sana za jinai, yaani kila inapoitwa leo unasikia fulani ana kesi ya uhujumu uchumi. Ukitikia mtu fulani amepigana tu na mwenzake; ni mke na mume wamepigana nyumbani wakifikishwa tu kule Mahakamani unaambiwa umehujumu uchumi. Kwa sababu mambo haya yapo katika jamii na tunayaishi, ni wazi kabisa kwamba mlundikano hauwezi kumalizika katika Magereza na Mahabusu zetu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nydingine na mlundikano katika Magereza zetu inatokana na uwepo wa masharti magumu ya upatikanaji wa dhamana. Najaribu kuangalia au kuwaza huko vijijini, tuachie kwanza mjini; huko vijijini ambapo changamoto hizi za watu kubambikiwa kesi, hivi na vile, zimeshika kasi sana kuliko mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kuwaza kwamba ili mtuhumiwa aweze kudhaminiwa, anapaswa kuwa na watumishi wawili wa Serikali kwenda kumdhampuni; na ikumbukwe kule vijijini ni ngumu sana, siyo rahisi sana kama mjini kwamba utapata Watumishi wa Umma, ni ngumu sana. Hata ukiwakuta hao wachache, hawana utayari wa moja kwa moja wa kudhamini watuhumiwa, kwa sababu unakuta mtu ametolewa Tanga anakwenda kufanya kazi huko Kagera kwetu huko ndani kabisa, hafahamiani na mtu, hana ushiriki mzuri wa moja kwa moja na wale watu, kwa hiyo, ni ngumu sana kumdhampuni mtu ambaye hamfahamu vizuri kabisa. Hili linakuwa ni changamoto sana, nimesema zaidi sana vijijini kwa sababu mjini unaweza ukapata kidogo unafuu wa kumpata mdhamini kwa sababu Watumishi wa Umma wapo wengi ukililinganisha na vijijini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweka pembedi hilo la uhaba wa watumishi vijiji ni kwenda kuwadhamini watuhumiwa, sheria inamtaka mtuhumiwa aweke dhamana ya hati ya nyumba, kwa maana ya mali isiyohamishika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapowaambia watuhumiwa hao kwamba wanapaswa kuwa na hati ili waweze kujidhamini wakati tunafahamu kwamba hati hizi siyo tu vijiji ni *less than fifty percent* ya watu ambao wana hati za nyumba.

Kwa hiyo, unaweza kuona mlolongo huu ambao nimeweza kuulezea, sababu hizi chache kati ya nyindi ambazo nimeweza kuzielezea zinazopelekea mlundikano mwingu katika Magereza yetu unatokana moja kwa moja na kuwepo kwa masharti magumu ya dhamana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika hili, Tume ya Kurekebisha Sheria ilete maboresho hapa Bungeni; kwanza, tupitishe sheria ya kuwepo na ukomo wa upeletezi wa hizi kesi ambazo zinachukua muda mrefu. Tukifanya hivyo, tutapunguza moja kwa moja mlundikano usiokuwa wa lazima katika Magereza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja sasa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Bado dakika tano. Dakika kumi kuchangia.

NAIBU SPIKA: Wawili dakika tano tano, ndio taarifa niliyonayo hapa mezani. Kengele imegonga Mheshimiwa Agnesta Lambert.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja basi ni-summarize.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, shukrani. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Restituta Taska Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamanina Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo Ishengoma, ajiandae. (*Makofii*)

MHE. RESTITUTA T. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, nakushukuru. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai leo tupo hapa Bungeni tunachangia mada kwenye Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia mambo mawili matatu, lakini napenda kwanza nianze na suala la sheria ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu, zimetungwa muda mrefu, lakini nafikiri zilipokuwa zinatungwa kwa wakati ule zilikuwa zinahitajika kwa namna hiyo lakini sasa zinahitaji mabadiliko. Labda sababu ilizofanya zitungwe kwa wakati ule zilihitajika zitungwe kwa namna ile, lakini kwa sasa hivi zinahitaji mabadiliko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971. Ilipotungwa mwaka 1971 sheria hiyo ilikidhi mahitaji ya mwaka 1971 kwa kuonyesha kwamba mtoto wa kike anaweza akaolewa na miaka 15. Kwa sasa hivi watoto hawa wa kike wanasona, wanakwenda shule, wanakwenda kozi mbalimbali na pia Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejenga mashule mengi mpaka vijijini.

Kwa hiyo basi, mahitaji ya wakati ule wa mwaka 1971 siyo mahitaji ya sasa hivi ya kuwepo na sheria hiyo ambayo ina kipengele hicho ambacho kinaweka tofauti ya mtoto wa kiume na mtoto wa kike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 13 cha Sheria ya mwaka 1971 na Kipengele cha 17 kinatoa ile tofauti ya mtoto wa kike kuolewa na mtoto wa kiume. Sasa ili twende na usawa na kwa sababu tulimsikia pia Mheshimiwa Rais pale

alisema kwamba akili za mtoto wa kike na wa kiume ni sawa, naomba kipengele hiki kibadilishwe umri wa kuoelewa wa mtoto wa kike uwe sawa na umri wa kuo wa mtoto wa kiume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Sheria ya Mirathi ambayo kwa wakati ule mila zilikuwa zimeshamiri na zilikuwa zinafuatwa sana nchini kwetu Tanzania. Miaka ya 1963 wakati wa Uhuru, tulihitaji sana kufuata mila. Maamuzi mengi ya Mahakama yalikuwa yanafuata mila za eneo lile au mila za kabila ile, ndiyo maana kukaja na hiyo *customary Law*, sheria zikaletwa wale watawala wetu wakaona watahukumu zile sheria kufuatana na mila na desturi za eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hiyo Sheria ya Kimila ina *section* ambayo ina ubaguzi wa hali ya juu kwa mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano nikichukua *Section* ya 27 ambayo inaelezea kwamba, mwanamke anaweza akatumia zile mali za familia, lakini hawezি kurithi mali za familia. Ijapokuwa Mheshimiwa aliyechangia aliyeppita, alijaribu kuzielezea, lakini naomba nidadavue kidogo. Sheria hiyo inamfanya kwanza, mwanamke *aji-feel* ni *inferior* kwa mwanaume kwa sababu, katika ubongo wake anakuwa anaelewa kwamba mali hii anahitajika kuitumia tu, lakini sio kuirithi. Pia, sheria hii imekuwa ikiendeleza ule ubaguzi wa jinsia ya kike na ya kiume. Tunayo Tume ya Kurekebisha Sheria lakini hajachukulia ule mkazo thabiti wa kubadilisha sheria hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu, nimekuwepo hapa Bungeni miaka mitano iliyopita, niliona sheria ambazo zililetwa na tukazibadilisha humu Bungeni, lakini kwa sheria hizi mbili kumekuwa na kigugumizi cha aina fulani kuchelewa kuletwa kuja kubadilishwa. Kwa hiyo, niombe kwa sababu, hiyo Tume ya Kurekebisha Sheria ipo izifuatilie hizo sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, zipo pia sheria nyingine nyingi tu ambazo siwezi nikazitaja humu Bungeni lakini pia, *either* zinawanyima haki wananchi au vile vile labda zinatengeneza mazingira magumu kwa wananchi ambao wanakuwa hawawezi kupata haki zao vizuri. Kwa mfano, Sheria ya Usalama Barabarani nayo pia ina vipengele ambavyo mwananchi anakosa haki pale anapogongwa na gari au ajali inapotokea barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuzungumzia suala la Wanasheria wa Serikali. Wanasheria wa Serikali wanafanya kazi ngumu sana kuhakikisha kwamba, wanaitetea Serikali mahakamani. Naomba miundombinu yao iboreshwe, Wanasheria hawa wa Serikali wanakwenda mahakamani kutetea kesi za pesa nyingi, lakini unakuta anapotoka pale anakwenda kukaa kwenye nyumba ya kupanga na unakuta hata usafiri hana. Naomba waboreshewe makazi yao, lakini pia waboreshewe mishahara yao. Hawa watu wanatetea Serikali, lakini wanatetea kesi kubwa za madawa ya kulevyta, za ugaidi hivyo wanahitaji kuwa na ulinzi na wanahitaji wafahamike wanakaa wapi ili angalau hata inapotokea jambo waweze kusaidiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye mahakama zetu. Kama alivyosema hata Mwenyekiti wa Bajeti hapa, mahakama nyingi hasa zile Mahakama za Mwanzo zimechoka. Wizara ya Katiba na Sheria ichukue jukumu la kuziboresha hizi mahakama *either* kubomoa zile mahakama ambazo zilijengwa na watawala wetu na zijengwe mahakama ambazo tutasema sisi tumejenga. Litengwe fungu zijengwe mahakama, zinazohitajika kuboreshwa ziboreshwe. Vile vile miundombinu ya mahakama iboreshwe, kwa mfano, niliuliza swali hapa Bungeni Hakimu na Jaji anachukua jukumu la kusikiliza kesi, kukusanya ushahidi na pia anakuja kuandika ile hukumu yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini isianzishwe *division ya stenographerili* wawe pale mahakamani waweze

kuandika yale mambo ambayo yanazungumzwa pale mahakamani. Hii itasaidia sana wananchi kupata hukumu zao mapema, sasa hivi kumekuwa na usumbufu kesi inahukumiwa leo tarehe 28, lakini hukumu mpaka iandikwe ni baada ya mwezi mmoja. Mwananchi anatembea anakanyaga kwenda kule mahakamani kufuatilia hukumu hii. Hii inaweza ikatengeneza mazingira ya rushwa kwa sababu, unaweza kusema kwamba, naomba uniandikie hukumu yangu ili niweze kwenda kufuatilia. Labda una kesi ya madai, sasa itabidi ufatilie ile hukumu, upate ile hukumu ili uweze ukatekeleze ile kesi yako ya madai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba sana hiyo *division* wangejaribu kufikiria hii Wizara ya Katiba na Sheria ili kuwarahisishia kazi hawa Majaji na Mahakimu, wanafanya kazi kubwa sana. Mishahara yao iboreshwe, wanahukumu kesi nzito na wanafanya kazi ngumu sana pale mahakamani, vile vile wanakuwa na jukumu la kukaa kuanza kuandika ile hukumu ili kumpa mwananchi. Ukiangalia na sasa hivi tunakwenda kutafsiri hizi sheria kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili, basi jukumu lao la kazi litakuwa ni kubwa mno wanahitaji kuwa na hiyo *division*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumza leo, ningependa kuwaambia wananchi lakini pia kujiambia sisi wenyewe kwamba, tuishi kwa kutii sheria. Tuklishi kwa kutii sheria nchi yetu itaendelea kuwa na amani lakini pia, sisi wenyewe tunakuwa na uhuru zaidi. Naamini kwamba, Polisi au mtu hawezi akapelekwa mahakamani na akawekwa rumande kwa muda mrefu kama hana kosa. Kwa hiyo, naomba tunapokwenda kusema kwamba, sheria kwa nini imefanya hivi, tujaribu pia na sisi kujielekeza kwamba, tuishi kwa kutii sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana kwamba, tusiishi kwa kufanya makosa ili tukitegemea kutafuta upenyo wa kutolewa kwenye lile kosa. Ukivunja sheria, sheria itakushughulikia, lakini pia sheria ndio inayoweza kudumisha amani nchini kwetu, vinginevyo humu barabarani Mwenyezi Mungu asingeweka sheria sisi tusingepita barabarani, wewe

ungepita barabarani yaani mtu angekutemea mate, mtu angekugonga, kwa hiyo, sisi wenyewe tufuate sheria na tuziheshimu sheria zetu ili tusiweze kuvunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.
(*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Osca Kikoyo Ishengoma na Mheshimiwa Salome Wyclife Makamba ajiandae.

MHE. NG'WASI D. KAMANI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Nianze kwa *ku-declare interest*, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na hivyo nianze kwa kuipongeza Wizara hii ambayo imefanya kazi kubwa sana katika kuboresha miundombinu ya mahakama. Mahakama zimejengwa, mahakama jumuishi zinazojali haki za binadamu usawa wa kijinsia na haki za watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia, nizidi kupongeza Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya. Tunatambua kwamba, wamekuwa na mifumo mingi ambayo imeanzishwa ikiwemo mifumo ya mitandao, mahakama za kimtandao ambayo itasaidia sana sana wananchi wetu kwenye suala zima la upatikanaji wa haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu wa leo kwa kutoa tu ushauri. Langu leo ni ushauri. Kila kinachofanyika kwenye nchi hii ni katika misingi ya sheria na kanuni, maana yake sisi wote tuko hapa leo kwa sababu kuna sheria au kuna kanuni inaturuhusu kuwepo hapa na kufanya haya tunayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa mfano wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au CAG. Ofisi hii imepewa mamlaka chini ya Ibara ya 143 ya

Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi hii kazi yake au jukumu lake kubwa, ni kudhibiti na kukagua mipango yote na matumizi ya pesa za Serikali katika Taasisi zote kuona kama zinatumika kama mipango yote ilivyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wote na sisi Wabunge tunakuwa tuna imani kwamba, kila kitu kinakwenda sawasawa pamoja na mipango yote ya pesa mpaka tutakapopokea ripoti hii ya huyu Mkaguzi, ituonyeshe *either* kuna sehemu pesa hizi hazikutumika vizuri au kuna sehemu zilipelekwa kinyume na utaratibu au kuna sehemu zimetumika vizuri au kuna sehemu labda tunapata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa mfano huu, lakini sasa nirudi katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Inabidi tujulize ni chombo gani, Taasisi gani au ni mtu gani mwenye mamlaka ya *ku-assess whether* sheria tunazotunga kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinatekelezwa sawasawa na maelekezo ya sheria hizo. Pia ni Tume gani inayoangalia kwamba, sheria hizi *either* zinakuwa zinawapa haki wananchi, au zinawakandamiza, au sheria imekuwa *short* kwa kitu fulani tuiongeze wigo sehemu fulani au tuipunguzie mamlaka sehemu Fulani. Pia tunaweza kuona kwamba, Tume fulani iliyotengenezwa kwa mujibu wa sheria inafanya kazi zake sawasawa au haifanyi kazi zake sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba, jukumu la kutunga sheria lipo ndani ya Bunge hili Tukufu, lakini kuna *principle* ya *natural justice* inayosema kwamba, *you cannot be a judge of your own case*. Ni chombo gani kinachotuonesha kwamba sheria tulizopitisha sisi kama Bunge, zinafanya kazi yake sawasawa au zinafuatwa sawasawa kule nje. Tunatambua kwamba, kuna chombo ambacho ni mahakama, mhimili ulioanzishwa kwa ajili ya *ku-enforce* sheria hizi, lakini mahakama tunatambua wote kwamba, haiwezi *ika-move on its own motion* lazima iwe *moved* na mtu, *either* kuna mgogoro umetokea au kuna mtu anaenda kutafuta tafsiri ya sheria mahakamani. Vile vile

tuangalie je, kuna sheria ngapi ambazo tumezitunga leo hii ni *source* ya *grievance* nyangi sana kwenye jamii yetu na si wote tuna nguvu ya kwenda mahakamani kufungua kesi kwa ajili ya kupata tafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba, Bunge hili mwaka 1980 lilitunga Sheria ya kuanzisha chombo kinachoitwa *The Law Reforms Commission*, ambacho kimsingi majukumu yake ni haya sasa; ya kuonesha kwamba, sheria zinazotungwa zinaendelea kuendana na wakati? Au sheria zinazotungwa zinatekelezwa sawasawa wapi tuungeze, wapi tupunguze maana yake kulishauri Bunge na Serikali sheria zetu ziendeje?

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hiki nasukumwa kusema bado hakijafanya kazi yake sawasawa, aidha kuna upungufu wa bajeti au kuna upungufu kwenye utendaji wa chombo hiki au *composition* ya chombo hiki. Nitoe mfano, kuna sheria kwa mfano, sheria *inayo-deal*/na Bodi ya Mikopo. Kuna mambo mengi sana ambayo Wabunge wengi wamesimama na kuzungumza juu ya Sheria hii ya Bodi ya Mikopo. Suala zima la kupandisha *interest* kutoka asilimia nane (8) kwenda 15. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hiki kingekuwepo hili lilikuwa ni jukumu lake la *ku-assess* na kuihoji Serikali kwamba, *justification* ya kutoa asilimia nane *interest* kwenda 15 imepatikana wapi? Je, kima cha chini cha mshahara wa Kiserikali tukitoa asilimia 15, tukatoa *PAYE*, tukatoa makato ya *NSSF* au *PSSSF* kinamtosha kijana kuweza kumudu maisha yake na ndio maana tukatoa nane kwenda 15? Pia, chombo hiki kingekuwa na mamlaka ya kuihoji Serikali katika utungaji wa sheria hii, ni wapi wamepata *justification* ya kuweka asilimia sita kama *retention fee* ya mikopo hii, wakati tunajua kwamba *inflation* ya pesa yetu katika nchi yetu mwaka 2019 tulikuwa na 3.4 percent, 2020 tulikuwa na 3.2 na mwaka 2021 mpaka Machi tumekuwa na kama 3.2 mpaka sasa Machi mwaka huu, lakini wenyewe tumewekewa asilimia sita kama kulinda thamani ya pesa hii, *justification* hii imetoka wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *justification* nyingine ya kuweka *grace period* ya miaka mwili ndio mtu aanze kulipa, je, tumekusanya takwimu za kututosha ili kuona kwamba katika nchi hii kijana akihitimu ana *windowya* miaka miwili tu atakuwa amepata ajira! Kuna watu wanakaa mpaka miaka saba mpaka 10 hawajapata ajira. Maana yake chombo hiki kingekuwa na uwezo wa kuhoji utekelezaji wa baadhi ya sheria, ikatupa maoni yake na kikawa na nguvu na ripoti hizi zikaletwa Bungeni tukazijadili na zikatumika kama ushauri wa moja kwa moja *kuli-guide* Bunge na *kui-guide* Serikali namna gani tunarekebisha sheria zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe mfano wa mfumo mzima wa upatikanaji wa haki hasa kwenye mfumo wa makosa ya jinai. Mahakama zetu zina mamlaka ya kutoa hukumu ya mwisho, lakini hazina mamlaka ya *ku-guide* namna gani uchunguzi au *Investigation* zinafanyika kule kwenye hizi kesi zetu. Kwa hiyo, unakuta kuna kesi inakaa miaka miwili, mitatu, minne au mitano bado uchunguzi unafanyika, aidha mtu yuko ndani au yuko nje, lakini anazidi kupoteza muda wa msingi wa kuwa anahudhuria mahakamani kila siku na haki yake haijapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hiki kingekuwa na mamlaka ya moja kwa moja katuonesha kwamba, wapi turekebishe, wapi tuongeze nguvu katika mahakama zetu ili ziweze kusukuma vyombo vya kufanya uchunguzi wa haraka. Chombo hiki kingetuonesha kwamba kwenye sheria labda kuna makosa tuweke *time limit investigation*, ili iwabane watu wale wafanye uchunguzi kwa muda mfupi ili haki za watu ziweze kutendeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yote hii ni kuonesha kwamba chombo chetu cha *Law Reforms Commission* kipo na majukumu yake yapo kisheria lakini hakijafanya kazi yake sawasawa. Mmigogoro mingi inayotokea katika Serikali na wananchi ni katika utekelezaji wa sheria. Sheria zetu zipo, ndio kuna baadhi zina upungufu lakini zile ambazo zipo sawasawa, labda hazitekelezwi sawasawa huko kwenye jamii zetu. Chombo hiki kingekuja na ripoti ya kila mwaka kama

sheria inavyosema, ili kutueleza kwamba sheria hizi ziko hivi, lakini hazitekelezwi na wapi turekebishe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuatilia, ni muda wa miaka mingi sana tangu chombo hiki kitii takwa la kisheria la kuleta ripoti yake kwenye Bunge hili Tukufu. Nimekwenda kwenda Kitengo cha *Hansard* wameshindwa hata kupata *record* halisi ya lini ripoti imepokelewa hapa Bungeni, kitu ambacho ni kinyume cha sheria. Ripoti ya CAGinapokelewa kila mwaka na *inatu-guide* kama Serikali kuona kwamba wapi mapato yetu hayakwenda vizuri, wapi turekebishe, wapi tufanye vizuri zaidi. Kwa hiyo, naishauri Wizara hii ya Serikali kuangalia namna ya kukifufua chombo hiki, aidha tukifumue tukiweke sawa ili kipate nguvu ya kuwa kinaleta ripoti katika Bunge hili Tukufu, ili tuweze kuona utekelezaji wa sheria unakwenda kama ambavyo sheria zetu zimetungwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niipongeze tena Wizara hii, kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake ambaao unaendelea kufanyika na tunaamini kwamba kama llani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 inavyotuelekeza, hasa katika ukurasa wa 167 upatikanaji wa haki utaendelea kuwepo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wyclife Makamba na Mheshimiwa Godwin Kunambi ajiandae.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami nichangie kidogo hii hoja ambayo iko mbele yetu. Niwapongeze Mawaziri kwa kazi yao nzuri, lakini ninazo hoja mbili. Nitaongelea Sheria ya Bima, tunapoisoma pamoja na Sheria ya Usalama Barabarani. Sheria ya Bima hasa inapokuja kwenye makosa yanayotokana na ajali za barabarani, inayo matatizo makubwa sana na ukiisoma hii sheria ya bima, ajali

inapotokea barabarani, Jeshi la Polisi watakwenda watapima, kesi itapelekwa mahakamani, tutasubiri hukumu itoke na wote tunajua, ni mashahidi hukumu zetu zinachukua muda gani! Hukumu ikishatoka yule muhanga wa ajali ya barabarani ndio anaweza akaambatanisha ile hukumu kwenda kudai fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ni kwamba anapokwenda kudai ile fidia, Sheria ya Bima iko kimya anakwenda kulipwa kiasi gani, ni maamuzi ya kampuni ya bima. Tumeshuhudia ndugu zetu wengi wakipoteza maisha yao kwa sababu, ajali inapotokea baadhi ya familia zetu tunazijua ni masikini, hawana hata pesa ya kumtibia huyu muhanga wa ajali ya barabarani. Wanaanza kuchangishana ukoo mzima ili kupata hela ya kumpeleka hospitalini. Anapokwenda sasa kudai ile fidia/*compensation* ambayo inalipwa na kampuni ya bima, anakwenda pale wanamwambia tunakupa shilingi laki tano. Ni maamuzi ya kampuni ya bima ndio inaanua amlipe kiasi gani, mtu ametoka Kagera na tunajua makampuni makubwa ya bima yapo Dar es Salaam au hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anatoka Kagera analipa nauli anakwenda Dar es Salaam anaambiwa tunakupa shilingi laki tano, hatuwatendei haki watu wetu. Niwaombe Sheria ya Bima ya Tanzania itoe kima au kiwango cha chini, ambacho mtu anapopoteza maisha katika ajali ya barabarani anapaswa kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria nyininge si kwamba hatuna mifano, tunayo mifano. Usafiri wa anga mtu anapokufa akiwa kwenye ndege, sheria zetu pamoja na kanuni za *TCAA* za usafiri wa anga za mwaka 2008 zinatoa kima cha chini ambacho mtoa huduma anapaswa kumlipa muhanga wa ajali anapokuwa kwenye ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma *regulation 24* ni 120,000 *USD* tunajua hiyo hatuna shida nayo. Lakini usafiri wa majini, nayo ukisoma *Shipping Merchant Act* kipengele cha 352 kimetoa kima cha chini ambacho muhanga wa ajali

ya usafiri wa majini anapaswa kulipwa endapo atapata kifo au ajali au kupoteza mali zote akiwa kwenye meli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hiyo Sheria ya Usafiri wa Majini (*Merchant Shipping Act*), ukiisoma ni kichekesho tu, haitekelezeki. Niwaombe Tume ya Kurekebisha Sheria; twenda tukaipitie hiyo Sheria. Unaposema mtu akifa kwenye meli anapaswa kulipwa *units* wanasema laki 333 *units of account* nikalifuatilia kuangalia hizi laki 333 *units of account* maana yake ni nini? Nikaenda kupata kwamba hizo ni sawasawa na *one special drawing like the SDR*. Na *SDR* moja ni sawasawa na *Euro* moja, ni kampuni gani ya Kitanzania inayoweza ikalipa hizi fedha? Haipo!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, na Sheria hiyo tunayo, likitokea la kutokea, hatuwezi kuya-*enforce* kwasababu ya ugumu wake. Lakini tunajua kwamba hii Sheria ukiisoma na Sheria ya Australia ni *cut and paste*. Kwa hiyo, niiombe Tume ya Kurekebisha Sheria ipitie hii sheria iweze kuiweka katika viwango ambavyo ni vya kitanzania ambavyo ikitokea ajali hii inaweza ikalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye masuala la ajali za barabarani. Naomba niishauri wizara, twenda tukapitie Sheria ya Bima tuioanishe na Sheria ya Usafiri wa Barabarani *Road Traffic Act*, tuje na mapendekezo au kiwango ambacho kinahimilika ili watanzania wenzetu wanapopata ajali waweze kulipwa kama sheria inavyosema *to compensated adequately* lakini sheria ilivyo hatuwatendei haki Watanzania. Tusiyaachie Makampuni ya Bima yaamue juu ya maisha ya Watanzania wenzetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri mwingine kuhusiana na hii, wananchi wetu wanapopata ajali wakati wanasubiri kesi iende mahakamani ihukumiwe, hapa katikati hatuna chombo cha kuwashudumia tunajua wengi hawawezi kujihudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri wizara tuunde chombo ambacho kitachangiwa na makampuni yote ya

Bima mtu anapopata ajali leo, kile chombo kitoe fedha zikamuhudie huyu mhanga wa ajali wakati tunasubiri Shirika/ Makampuni ya Bima kumlipa, atakapolipwa zile fedha ambazo tutakuwa tumempatia kumuhudumia basi tutazikata kurudisha kwenye mfuko ambao nashauri na kupendekeza uundwe chini ya sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo janga lingine, tunayo Sheria ya *TASAC*. Tulitunga hapa Bungeni lakini ukiisoma leo katika mazingira ambayo leo tunasema tunakwenda kujenga uchumi shindani; ile sheria ni janga la Kitaifa. Nashauri hii sheria tukaipitie upya, haileti ustawi wa sekta binafsi kwenye usafiri wa majini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema *TASAC* ni mdhibiti na tunajua udhibiti tulionao Tanzania tuliochagua kuuchukua ni udhibiti wa pamoja; lakini *TASAC* yenyewe ukialangalia imeunganisha shughuli za kiudhibiti na shughuli za kutoa huduma. Huwezi ukawa referee wakati huo huo unacheza mpira uwjanjani ni makosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza na kushauri, shughuli za kiudhibiti ambazo ziko chini ya hii sheria zitenganishwe tuwe na mamlaka na chombo ambacho kinaangalia masuala ya udhibiti wa usafiri wa majini na tuwe na kampuni ambayo itatuangalizia kwa nia ileile ambayo tulikuja na hii sheria ya *TASAC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua zamani tulikuwa na *NASACO*, turudishe mfumo uleule lakini tuwe na chombo ambacho kinafanya kazi ya udhibiti peke yake na chombo ambacho kinafanya biashara. Na misingi ya udhibiti, mdhibiti ana hadhi ya kimahakama na hawa wengine wote ambao wanafanya zile shughuli wanapokuwa na matatizo wanakuja kwa mdhibiti ili akawapatie suluhu ya matatizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapokuwa na Taasisi ambayo kimsingi ni mdhibiti, ni mahakama, lakini na yeze anafanya zile shughuli inakuwa ni kinyume na utawala bora inapokuja kwenye kusuluuhisha matatizo yanayojitokeza

kwenye hiyo sekta. Niombe Tume ya Kurekebisha Sheria, iiangalie hii sheria; badala ya kuleta ustawi nadhani maoni yangu inakwanza ustawi wa sekta hii ya usafiri wa majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naomba niunge hoja mkono. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin E. Kunambi, Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi ajiandae.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, Nakushukuru kunipa nafasi nichangie wizara hii ya muhimu ya Katiba na Sheria. Mwaka 2018/2019 kwa niaba ya Wabunge wenzagu wanaotetea haki za mtoto wa kike, nilishika shilingi ya waziri ndani ya Bunge hili nikintaka waziri kufuata maelekezo ya Mahakama ya Rufaani kuleta mabadiliko ya Sheria ya Ndoa; kwa kubadilisha Kifungu cha 13 na 17 ambacho kina mruhusu mzazi kumuozesha mtoto chini umri wa miaka 18, Waziri alitoa majibu ambayo kwa kweli sikuridhika nayo lakini kwasababu wengi wape, walishinda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Samia Suluhu Hassan, amejipambanua kwamba ni mwanamke anayetetea haki, demokrasia, utu na usawa. Namtaka waziri, atekeleze hukumu iliyotolewa mwaka 2017, Kesi Na. 204 kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na *Attorney General*. Ambayo mahakama ya Rufaa the sealing ilielekeza ndani ya mwaka mmoja, sheria hii iletwe ndani ya Bunge, Vifungu hivi vifutwe na mtoto wa kike apate haki sawa ya kuamua kuhusu ndoa yake akiwa na miaka 18. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumuozesha mtoto wa kike chini ya miaka 18 si tu inamuhatarisha maisha yake ni unyanyasaji wa kijinsia, kwasababu hawezi kusimama mahakamani kama haitaki ndoa ile iko chini ya umri. Inamletea madhara ya uzazi anaweza kuzaa Watoto njiti, anaweza kupata fistula; walijitetea Serikali kwamba haya ni mambo ya kidini lakini kipekee kabisa nitoe nukuu ya Baraza

Ia Ulamaa lililokaa mwaka 2019 walisema; "Uislamu umezingatia kuwa hili mwanamke aweze kuolewa ni lazima awe tayari kikili na kimwili. Hatuwezi kuwanyanya Watoto wa kike kwa kuwa ozesha katika umri mdogo kuna tofauti kubwa sana kati ya umri wa kufanya mapenzi na umri wa kuhimili mikiki mikiki ya ndoa." (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namtaka waziri alete marekebisho haya kudhirihishia sisi Bunge tunaheshimu utawala wa Sheria, tunaheshimu Mihimili mingine kwa kutekeleza maelekezo ya Mahakama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo changamoto kubwa ya Sheria ambayo imetungwa ndani ya miaka mitano. Sheria katika mwenendo wa makosa ya jinai inayohusiana na mambo ya *plea bargain* yaani kumpa mamlaka Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali kufanya makubaliano na watuhumiwa na kulipwa fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipinga ndani ya Bunge hili kuhusiana na sheria hii, kwasababu kwanza; Mahabusu umemuweka ndani, umemuweka kwenye mazingira magumu, amepoteza rasilimali, amepoteza uwezo wa kutafuta fedha, halafu unamuita unamwambia njoo tukubaliane unilipe kiasi kidogo ili nikuachie. Hakuna usawa katika makubaliano hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yalifanyika, ilitekelezwa sheria ile, fedha zikakusanywa kilichotokea kwa mara ya kwanza na cha kushangaza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilivamiwa na fedha zikaibiwa hatujui ziliibowi shilingi ngapi! hatujui fedha zilikwenda wapi! Mpaka leo hakuna kinachoendelea wamekaa kimya na hakuna anayewajibika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifuata Sheria ya *Plea Bargain* mzizi wake ulikuwa ni Marekani, India waka-*adopt* mfumo ule, Tanzania tukauchukua tukauingiza Bungeni. Lakini wenzetu walioanzisha Wamarekani waligundua, kwenda ku-

negotiate na mtuhumiwa aliyeko mahabusu aliye poteza kila kitu mpaka utu wake, kwenda ku-*negotiates* iyo haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wamekwenda mbali sasa hivi ni lazima watuhumiwa wafkishwe mahakamani, kama DPP anataka kufanya makubaliano na mtuhumiwa waende mahakamani, mahakama ijiridhishe kwamba makubaliano yale yanazingatia kwamba mtuhumiwa yule hajalazimishwa na hakuna mazingira ya mashinikizo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama tunataka kwenda suala ya *plea bargain* nimuombe Mheshimiwa Prof. Kabudi turudishe hapa hii sheria, isiwe wanajifungia chumbani mtuhumiwa na Mwendesha Mashtaka wa Serikali wanakubaliana wanakwenda kufanya *plea bargain*. Iwe ni kati ya mtuhumiwa, mahakama na DPP wakubaliane ione kane uwanja wa makubaliano ulikuwa sawa ndio mtuhumiwa aweze ku-*bargain*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tena naomba nishauri twende mbali zaidi, twende tukafanye *evaluation* ya utekelezaji wa sheria ya *plea bargain* tangu tumeitekeleza. Wote hapa tuna *smart phone* mnaona *twitesza* watu ambao wamefanya *plea bargain*, mambo ya kinyama yanayofanyika kwenye hizo magereza mpaka wale watu wanakubaliana kulipa zile fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, iundwe tume Maalum, kwa ajili ya kwenda kufanya uchunguzi na kupima ufanisi wa sheria hii. Watu wamenyanyaswa, watu wamenyang'anywa mali zao, wameporwa kuititia *plea bargain*, fedha zetu zimepotea hizo ambazo zimeshatolewa kwenye *plea bargain*, iundwe Tume Maalum kuangalia ufanisi wa sheria hii ambayo tumeitunga ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na twende mbali zaidi nimuombe Mheshimiwa Prof. Kabudi anapokuja kuhitimisha atueleze fedha zetu za *plea bargain* zimepoteaje! *Attorney*

*General/akafanye uchunguzi kwanza zile pesa zilikuwa shilingi ngapi? Ambazo zilifanyika kwenye *plea bargain*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umenipunguzia muda wangu mpaka dakika tano na naheshimu Kiti chako. Naomba niende kumalizia hoja moja tu. Au umeniongeza mama! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie hoja moja ya Katiba mpya; Mama amesema vizuri na amesema kwa kututia matumaini kwamba tusubiri kidogo, sisi wengine ni wasukuma kidogo hatuelewi maana yake ndio mpaka amalize au nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kikubwa ninachotaka kusisitiza na kumuomba mama yetu suala la Katiba Mpya ye ye alikuwa ni Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Anajua shauku ya Watanzania kwenye Katiba Mpya. Anajua gharama zilizotumika kuhakikisha Katiba imefikia ilipofikia na pengine ipo hatua za mwisho kabisa. Tunaheshimu kauli yake basi kidogo hii ya Mheshimiwa mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan angalau basi isitufikishe kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kwa sababu hapo ndipo tunapoanza kuchefuana, tusifike huko, ajitahidi kidogo hii iwe ndani ya hii miaka miwili akishakuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi basi asimamie ilani yenu ya Chama Cha Mapinduzi. Nakushukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba hapo mwisho umesema anakwenda kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi; ni kweli, lakini wakati huo huo unasema asimamie utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi. Hapo napo upo sawa sawa, llani hiyo unayoizungumzia ungekuwa umeisoma ungegundua ina kurasa 303 hakuna mahali pametaja Katiba Mpya.

Kwa hiyo, tuweke kumbukumbu vizuri sana hapa katika kurasa zote hizo hakuna mahali pametajwa Katiba Mpya. Enheee! Ni vizuri sana kuweka kumbukumbu vizuri. (*Makofi*)

Lakini pia lingine Waheshimiwa Wabunge ngoja, ngoja, ngoja, twende vizuri wakati unachangia tukumbuke jukumu letu la Kikatiba ni kuishauri na kuisimamia Serikali. Sasa kuishauri na kuisimamia Serikali ukisema unaiagiza Serikali, yaani usitoe maagizo ambayo hayatekelezeki; kwa hiyo, wewe Mbunge mmoja huwezi kuiagiza Serikali. Ni sawa na kutumia maneno kama unaitaka Serikali, yaani ukitumia maneno ambayo jambo unalolisema halifanyiwi kazi yaani unaonekana sasa wewe ulikuwa unaongea nini! Kwasababu halitatekelezeka. Kwa hivyo unatoa ushauri, Serikali ikichukua ama isichukue umefanya kwa sehemu yako kuliko ukawa unatoa maelekezo yako hakuna mtu atayafanya. (*Makofii*)

Maelekezo ya humu ndani ni yale ambayo Wabunge tunakuwa tumehojojiwa Serikali lazima ikayafanye. Lakini yale ya kwako mwenyewe jaribu kutumia ile lugha ambayo hata Serikali isipofanya huonekani wewe kwamba ulisema jambo ambalo halifanyiki ama halitekelezeki. Huo ni ushauri tu wa matumizi ya lugha. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Godwin Kunambi atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi tutamalizia na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, Nikushukuru kwa dhati kabisa lakini niipongeze Wizara hii ya Katiba na Sheria ina Waziri mahiri kabisa, mbobezi wa masuala ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kidogo nikumbushe jambo kama binadamu. Katika jambo ambalo ni gumu na linahitaji umakini mkubwa kwenye maamuzi ni suala la utoaji wa haki. Nadhani kama unafanya *ranking*, suala la utoaji wa haki linashika *number one* duniani; kwasababu ni jambo ambalo mungu ameamini mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Sheria hizi mbili ya Utakatishaji wa Fedha na Uhujumu Uchumi, Bunge letu Tukufu lilitunga hizi sheria kwa nia njema kabisa; changamoto inayotukuta sasa ni utekelezaji wa sheria hizi. Naomba nikumbushe, wanadamu hapa duniani kwa Mujibu wa Biblia

kizazi chetu ni cha nne, na uhai wetu hapa duniani ni miaka 70 hakuna anayeishi hapa milele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sitaki kujua umri wa kila mmoja kila mmoja anaweza kutafakari aangalie miaka 70 *a-minus* umri wake sasa aone kipande alichobaki nacho duniani. Mtume Paulo kwa Habari ya Wakorinto aliwaeleza habari hii, aliwaeleza kwamba nikiitazama dunia ni ubatili mtupu. Hapa duniani tuwe na mali, fedha na kila kitu ni ubatili mtupu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali. Ofisi hii kama ni chakula ndio mpishi, akikosea huyu hii haki pale haitendeki na akipatia haki inatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika kuna jambo moja la ajabu sana limetokea pale jimboni kwangu yamkini ni kweli wananchi wale wamefanya makosa, vifaa vyao matreka yamekutwa kwenye hifadhi na inasadikika kwamba wamekutwa wakifanya shughuli za kilimo kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii wananchi hawa wapo mahabusu na kesi walizonazo ni Uhujumu Uchumi ni jambo la kushangaza kweli! Jambo la kushangaza kweli! Duniani kwamba kuna jambo linalohitaji umakini narudia kusema, ni jambo la utoaji wa haki. Kama mwanadamu akionewa, kama alitenda kosa mungu ametuumba lakini ndio *guilty conscious* yaani kuna adhabu ukipewa na umetenda nafsi yako hata kama hutasema inasema kweli nilikosea, nafsi inasema. Lakini ukionewa nafsi ina masikitiko na manung'uniko hakika aliyefanya makosa haya anachangamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, manung'uniko ya wanadamu mungu anasikia; leo hii kuna watoto, wake, Mheshimiwa Waziri, wake, watoto; hawasomi walikutwa tu kwenye hifadhi, matrektu hayo wanalima uhujumu uchumi, eeeh! Tumefika hapo! Kwa hiyo, ofisi ya DPP tusaidie, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali tusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimekuwa kiongozi wa taasisi tena kubwa tu; ukiwa kiongozi wa Jiji la Dodoma tena nafasi ya Mkurugenzi ni nafasi kubwa ya juu. Sasa nataka kusema nini? Kuna umakini mkubwa unatakiwa kwenye ushauri wa wasaidizi wetu kama husomi *documents* aaah! Unaletelewa tu, kuna wengine wana *compromise* rushwa huko, wameshindwa kupata rushwa anasema ngoja nimkomeshe huyu anakuletea na wewe unakubali. Kwa hiyo kuna jambo la umakini sana Ofisi ya DPPtusaidie. Watanzania wanalamika, watanzania wanunung'unka hasa wananchi wa Jimbo la Mlimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri na yeye binafsi alifuatilie, kama ikisadikika wananchi ni kweli wana makosa sheria ichukue mkondo wake. Mimi nishauri, Mheshimiwa Waziri ikikupendeza usiende tu kutembelea magereza nenda kalale! Usiende kutembelea kama *visitor*, nenda kalale, amka asubuhi utaona habari ya kule ndani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna jambo gumu ni magereza. Ukimpeleka mwanadamu kule hana hatia kilio na masikitiko yake hutabaki salama. Kwa hiyo, naomba tuwe na umakini mkubwa katika suala zima la utoaji wa haki. Sheria hazina makosa, makosa ni namna ya utekelezaji wa sheria. Narudia kusema Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, tafadhalii!

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye Mabaraza ya Ardhi. Yameelezwa hapa na Kamati imeshauri...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa hebu weka vizuri hiyo sehemu ili tuwasaidie hata upande wa Serikali inapokuja kujibu hoja. Katika maelezo yako nilikuwa najaribu kufuatilia njue unaelekea wapi lakini umeeleza kwamba matrekta yamekutwa kwenye hifadhi.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Naam!

NAIBU SPIKA: Ni uhalisia kwamba yamekutwa huko?

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Sasa hayo ndiyo yanayoelezwa kwenye ile...

MBUNGE FULANI: *Charge sheet.*

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: *Not charge sheet, nilipitia taarifa ya DPP, pamoja na mambo mengine kwenye facts alikuwa akitoa taarifa...*

NAIBU SPIKA: Sawa.

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana nilieleza mwanzoni yale mambo yaliyoko kule ukiyaleta hapa na sisi hatunayo unatupa wakati mgumu sana. Hata Serikali ukitaka ikujibu itakujibu kwenye hoja ipi? Kwa sababu katika maelezo yako wewe mwenyewe unayewatetea wale watu walioko ndani unasema hivi; wamekutwa na matrekta kule kwenye hifadhi. Sasa kama amekutwa na trekta kwenye hifadhi, lile trekta kwenye hifadhi linafanya nini?

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika.

NAIBU SPIKA: Ngoja, ngoja, nakuelezea hoja simaanishi uanze kujibizana. Ni hivi; ukiwa na jambo mahsusimwaeleze wakalifuatilie. Ukillieleza wewe kwa namna ya kwamba na wewe unalifahamu kwa kadri Ofisi ya DPP inavyofahamu, Serikali inavyofahamu utapata wakati mgumu ndiyo maana hata hapa umeanza kusema ndicho walichoeleza maana yake ndicho walichoeleza Serikali lakini watu wako wewe walikutwa kule au hapana? Rekodi za Bunge hapa zitaonesha kwamba Mbunge umesema walikutwa na matrekta kule kwenye hifadhi.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Nimesema inasadikika.

NAIBU SPIKA: Mimi nilikuwa nasikiliza na huwa nasikiliza kila neno ndiyo maana nakueleza. Sasa mchango kama huo ukibaki hapa halafu wale wakaamua kwamba ni ushahidi

Mbunge wenu mwenyewe alisema kwamba imekutwa kule. Kwa hiyo, ndiyo maana huwa najaribu kuonesha kwamba tuchangie kwa namna ambayo unaieleza hoja hiyo kwamba Serikali ikafuatilie. Taarifa za ziada waache wao watazipata na wewe kama Mbunge ni haki yako kabisa kwenda kwenye ofisi ya *DPP*, kwenda kwa Waziri kumueleza watu wangu wako kule hawajafanya kosa ama kwa namna yoyote ile unayotaka kuwatetetea. Ukiweka humu kwa mtindo huo inaonekana kwamba katika taarifa rasmi na wewe unasema wamekutwa kule. Mimi nilikuwa nasikiliza kwa makini kabisa.

Nenda kwenye hoja yako ya pili, hii ya kwanza nakushauri uonane na *DPP* kwa sababu ofisi yake iko wazi Mheshimiwa Waziri pia yuko hapa. Karibu sana umalizie mchango wako.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa ufanuzi na kama *Hansard* iko sawasawa nimetumia neno inasadikika.

Mheshimiwa Naibu Spika, njielekeze kwenye eneo hili la Mabaraza ya Ardhi. Mengi yameelezwa hapa kwa habari ya Mabaraza ya Ardhi kwamba yawe sehemu ya Mahakama. Mimi nitakuwa na mchango wa tofauti kidogo, isingefaa Mabaraza haya yawe sehemu ya Mahakama isipokuwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria atusaidie kama kuna eneo kwa mujibu wa Kanuni kwenye ile sheria iliyoanzisha Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya lionezwe kabla hajatoa maamuzi Mwenyekiti wa Baraza ni lazima athibitishie kwamba amefika eneo la tukio.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto inayojitokeza kwenye haya Mabaraza kwenye utoaji wa hati unakuta Mwenyekiti wa Baraza anajifungia kwenye chumba anatoa maamuzi na mgogoro wa ardhi ni lazima ufile eneo la tukio, ndiyo changamoto hiyo tu. Kwa bahati mbaya ukienda Mahakama Kuu inayoshughulika na masuala ya ardhi, haina nafasi ya kukusanya ushahidi. Kwa hiyo, hata maamuzi ya Mahakama Kuu ukimueleza mlalamikaji au mlalamikiwa, mdai au mdaiwa akate rufaa Mahakama Kuu haina nafasi

tena ya kukusanya ushahidi. Kwa hiyo, matokeo yake huyu mtu atendewe haki tu, hata rufaa bado ni changamoto tu. Kwa hiyo, msingi wa jambo lenyewe ni pale linaposikilizwa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na sasa hivi inakuwa ni utashi tu tena mlalamikaji anaambiwa nipe fedha ya kwenda *site*, Mtanzania wa kawaida hana. Sasa namna gani haki inatendeka, changamoto iko hapo. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa mujibu wa Kanuni au sheria yenyewe kuwe na eneo linalosema kwamba kabla hajafanya maamuzi ya mwisho ahakikishe amefika eneo la tukio. Ndiyo essence ya migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru kwa dhati na Mwenyezi Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Amin, amin, amin. Tena hiyo umemalizia vizuri sana maana umri wangu mimi nina mpango wa kutoa kwenye umri wa Mzee wetu Mwinyi kuliko huu wa miaka 70. (*Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Shaafi Mohamed Salum, tutamalizia na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

MHE. SALUM MOHAMMED SHAIFI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu lakini nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunajadili Wizara ya Katiba na Sheria ambayo ndiyo msingi wa Taifa letu. Nchi yetu inaongozwa na misingi ya Katiba na Sheria ambayo kila mmoja wetu anapaswa kuifuata na kuiheshimu. Hii ni Katiba ambayo sisi sote humu ndani tuliapa kuilinda na kuiheshimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa sababu kuna mambo ambayo binafsi nadhani sio sawa kuendelea kufanyika. Nikaanza kujiuliza, je, ni watu gani au

chombo gani ambacho kina mamlaka ya kuzitumia sheria na kutoa hukumu? Wapo baadhi ya viongozi wa Serikali wanatumia sheria, wanatoa hukumu mikononi mwao pasi na kuheshimu Katiba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona namna gani baadhi ya watu wanavyodhalilisha na baadhi ya viongozi wa Serikali. Tunaona kuna baadhi ya viongozi wa Serikali wanawadhalilisha kwa kuwapiga bakora watumishi wengine wa Serikali. Sidhani kama viongozi hawa wamepewa mamlaka, ni kwa sababu wameshindwa kuheshimu Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kwenye mitandao, tuliona Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa mmoja...

MBUNGE FULANI: Wa Wilaya.

MHE. SALUM MOHAMMED SHAIFI: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nazungumzia Mkuu wa Mkoa kule Zanzibar, acha huyu Mkuu wa Wilaya huku, anampigisha *pushup* mtumishi wa Serikali mbele ya vyombo vya ulinzi na usalama likiwemo Jeshi la Polisi halafu tunakaa tunasema tunaheshimu Katiba wakati wao ndio wanaoivunja Katiba hii. Mimi nitoe rai kwamba ipo haja kwa viongozi hawa kupewa elimu juu ya Katiba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kusema tuna kila sababu sisi Wabunge kuhimizana na kuheshimu mhimili mikuu ya Serikali. Mhimili Mkuu wa Bunge sisi lazima tuwe na kazi moja tu ya kutunga sheria. Mhimili mwingine ambao ni wa Mahakama, tuipe kazi yake ya kutafsiri sheria na Serikali kwenda kutekeleza sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu Serikali ilione hili juu ya watu hawa wanaowadhalilisha wananchi jambo ambalo halikupaswa kuwa hivyo. Walitakiwa wawachukue wapeleke polisi na polisi ifuate taratibu nyingine za kisheria. Ndiyo utaratibu kwa mujibu wa Katiba hii, tukiiangalia ukurasa wa 92 Ibara ya 107A inasema: "Mamlaka yenze kauli ya

mwisho ya utoaji wa haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama na siyo Mkuu wa Mkoa wala Mkuu wa Wilaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Tunafahamu kwamba utaratibu na mwenendo wa kesi umeandaliwa sheria zake lakin tuna kundi kubwa la watu ambao kesi zao ziko ndani ya upelelezi. Sasa tufike mahali uletwe Muswada wa sheria Bungeni tubadilishe baadhi ya mambo. Hatuwezi kila siku tukasema upelelezi unaendelea, miaka nane, tisa hadi kumi wakati hao ambao upepelezi wao unaendelea wameacha familia, tunawaathiri kisaikolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tufahamu sasa Taifa letu leo linapiga vita chokoraa, wana Watoto, nini faida yetu, wale watoto watakuwa chokoraa. Wameacha wake, wale wake watakuwa wajane. Taifa linahitaji uchumi, wale ambao tumewaweka ndani upelelezi wao unaendelea Taifa litakosa mapato kwa sababu baadhi yao walikuwa ni wafanyabiashara na kila Mtanzania anachangia mapato ndani ya Taifa hili. Naomba sana tutumie fursa tuliyonayo kupitia Bunge hili na vyombo vyenye mamlaka ya kubadilisha sheria, tulete Muswada tubadilishe sheria tuweke ukomo wa upelelezi, tusiende tu kama tunakata kamba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuchangia, tuna Katiba mbili; Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar. Ibara ya 93 ya Katiba ya Zanzibar imeeleza kwamba Zanzibar ina Mahakama Kuu na tukirudi kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeelezea kwamba nako kuna Mahakama Kuu, kila Mahakama inajitegemea, inafanya kazi pasi na kuingiliwa na Mahakama nyingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya kusikitisha, hali ya maajabu tunaidhalilisha nchi yetu na tunaonekana si watu wenye kufuata Katiba. Leo Mahakama upande mmoja inaingilia Mhimili wa Mahakama nyingine. Wako baadhi ya watu wametoka upande mmoja wa Zanzibar wameshtakiwa,

kesi zao wamehamishiwa Mahakama Kuu ya Bara. Naiomba Serikali ikija hapa ieleze Bunge hili na Watanzania ni mamlaka gani ambayo imepewa Mahakama Kuu ya Bara kuingilia Mhimili wa Mahakama Kuu ya Zanzibar watuhumiwa wa Zanzibar kushtakiwa Mahakama Kuu ya Bara. Tuelezeni kwa ufanisi kabisa ili tufahamu na wananchi wetu wajue kwamba kumbe Mahakama Kuu ya Bara ina uwezo wa kusikiliza kesi ya Mahakama Kuu ya Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nishukuru sana kwa kunipa nafasi hii na niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chonga kwa kuniamini kwamba naweza kuwatumikia. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa dakika tano hizi nimalizie mchango kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niunge mkono hotuba hii lakini kwa sababu ya muda nijielekeze moja kwa moja kwenye mada. Ni ukweli usiopingika tunalo tatizo la watumishi. Hili ni tatizo la Kitaifa kwamba kila Idara kuna upungufu mkubwa wa watumishi. Sasa leo mimi nitazungumzia Idara ya Mahakama hasa Ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na upungufu mkubwa wa watumishi kwenye Idara hii lakini kuna unyanyasaji mkubwa sana wa watumishi kwenye Idara hii hasa kwenye upandishwaji wa madaraja. Watumishi wengi wa Idara ya Mahakama wanahangaika kutafuta madaraja, hawapandishwi madaraja kwa wakati. Hili nalo limekuwa ni donda kubwa kwenye Ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano hapa, nina mtumishi aliyeajiriwa tarehe 4 June, 1990 anaitwa Rashid Ally

Libago, mtumishi huyu tangu mwaka 1990 mpaka leo nasimama hapa hajawahi kupanda daraja. Sasa hebu chukulia mshahara wa mwaka 1990, huyu anadumu nao mpaka leo atapata mafao ya shilingi ngapi? Jambo hili linasikitisha sana na barua zake ninazo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barua ya mwisho ameandika tarehe 12 Mei, 2020 nayo haijapata majibu mpaka leo. Jambo hili ni la kusikitisha sana na barua yake ya uthibitisho ilikuwa ni tarehe 14 Julai, 1999. Mshahara hapa siusemi lakini jamani tufikirie, hawa watumishi wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana sasa inapotokea mtumishi anaifuata haki zake, hili suala la kuzungushwazungushwa nalo sio jambo jema. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni la kisera. Ilani yetu inasema tumekusudia kila Wilaya iwe na Mahakama ya Wilaya; Ikila Kata kama sio Tarafa iwe na Mahakama ya Tarafa au Kata. Wilaya ya Liwale ni Wilaya tangu mwaka 1975 lakini mpaka leo hatuna jengo la Mahakama ya Wilaya. Jengo linalotumika sasa ni lile lilitokuwa na mkoloni ambalo ndiyo ilikuwa Mahakama ya Mwanzo ya Liwale Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo masika hii ukienda ofisi ya masijala wamefunika maturubai kwa sababu jengo lile linavuja. Kibaya zaidi au cha kusikitisha zaidi bajeti ya mwaka 2017/2018 nililiza swali la nyongeza hapa Mahakama ya Wilaya ya Liwale itajengwa lini? Mheshimiwa Waziri alitumia sekunde moja tu kunijibu, Mahakama ya Wilaya ya Liwale tunaijenga mwaka 2018, akafunga kitabu akaenda kukaa leo tunazungumza ni mwaka 2021 haijajengwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, tunapouliza maswali hapa na kujibiwa, kama Waziri huna uhakika wa jambo hilo basi jipe muda lakini unapowaambia watu kwamba Mahakama ya Wilaya ya Liwale itajengwa mwaka 2018 watu wanakusikiliza. Mpaka leo mimi wananiuliza, Mheshimiwa Waziri alikudanganya? Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imeshaanza kusema uongo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naiomba sana Serikali tunapo jibowi maswali kwanza i jilikanje kwamba sisi tumeagizwa na wananchi na tunachokisema hapa tunasema kwa ajili ya wananchi, tunaomba tujibiwe kama wanavyotaka waajiri wetu. Wilaya ya Liwale ina Kata 21, Mahakama za Mwanzo mbili tu; ya Liwale Mjini na Tarafa ya Makata, tunaiomba Serikali itufikirie. Nililisema hili wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu. Miongoni mwa majengo niliyoyataja ambayo hayana sura ya kuitwa Ofisi ya Wilaya ya Liwale, hayana sura hiyo ni pamoja na jengo la Mahakama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nzungumzie suala la Wazee wa Baraza la Mahakama mpaka leo posho yao ni Sh. 5,000 na posho yenyewe haitoki mpaka siku ya hukumu ya kesi. Kuhudhuria kesi hawalipwi, wanalipwa pale kesi inapohukumiwa. Sasa tufikirie hili Sh. 5,000 ni ya mwaka gani na leo tunazungumzia mwaka gani. Hawa watu hawaruhuswi kukosa, kila kesi ikiitwa wao wanaenda, kesi isipohukumiwa wanatoka kama walivyokuja mpaka hukumu ya hiyo kesi. Kwa shida iliyopo ya kuwa na Mahakimu wachache na vitendea kazi vichache, kesi zetu zinachukua hata miaka minne au mitano, wewe Mzee wa Baraza unasi mamia kesi miaka mitano una fukuzia Sh. 5,000. Ombi langu kwa Serikali tufikirie mambo mawili; aidha, kuwaajiri au kuwoangezea hako ka posho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa ajili ya michango yenu Waheshimiwa Wabunge. Upande wa Serikali naamini umeyachukua mawazo yenu kwa ajili ya kuboresha mambo mbalimbali ambayo mmeyachangia. Kwa hiyo, tuwashukuru Wabunge mliopata fursa ya kuchangia.

Ninayo matangazo mawili. Tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa kampuni ya *Angelic Handlers* wakishirikiana na Shirika la Ndege la *Precision Air*

wameongeza safari ya ziada kutoka Dodoma kwenda Mwanza siku ya Ijumaa tarehe 30 April, 2021 saa 11.30 jioni. Hivyo kwa Wabunge wanaotaka kutumia usafiri wa ndege wa Shirika la Ndege la *Precision Air* siku hiyo ya tarehe 30 Aprili, 2021 wanashauriwa kwa utaratibu wa kawaida wa kukata tiketi kuwasiliana na dada anayeitwa Mercy ili kufanya *booking* ya safari hiyo. Sasa hapa kuna namba za simu, naamini Waheshimiwa Wabunge mna kalamu hapo ni 0754972173 na 0787845200. Wale watakaokuwa wanaenda kwenye Mei Mosi nadhani ndege hii itawafaa zaidi.

Pia liko tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Umoja wa Wanawake (UWT) unawaalika Wabunge wanawake wa CCM kushiriki futari ya pamoja siku ya tarehe 29 Aprili, 2021 katika ukumbi wa *Dodoma Hotel* kuanzia saa 12.00 jioni. Aidha, Umoja huo pia unawaalika Wabunge wa Viti Maalum wa CCM kushiriki kikao cha Uongozi wa UWT Makao Makuu kitakachofanyika tarehe 3 Mei, 2021 katika ukumbi wa *NEC* kuanzia saa 7.00 mchana hadi saa 8.30 mchana.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo. Hivyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 07.06 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni, Bunge lilirejea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa majadiliano yanaendelea. Tutaanza na Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, halafu nitamwita Mtoa Hoja ahitimishe hoja yake.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nипитie maeneo machache ambayo Waheshimiwa Wabunge katika mjadala wa leo walijaribu kuibua hoja. Kwa ujumla wake tunawashukuru sana Wabunge wote waliochangia na ninadhani Mheshimiwa

Waziri wakati atakapokuwa anahitimisha atatambua kwa majina mchango wa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa eneo langu nitazungumzia hoja mbili; moja, ni msongamano wa mahabusu katika Mahakama zetu ambapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walichangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi ni kweli kwamba kumekuwepo na msongamano wa mahabusu katika Magereza zetu. Hii kwanza ni kutokana na Magereza zetu kutokumudu hiyo namba ya wahalifu wanaopelekwa pale. Hii ni kwa sababu Magereza nyingi nchini zimejengwa muda mrefu sana na nyingi zilijengwa siku za nyuma, hata nchi yetu kabla ya kupata uhuru. Kwa hiyo, utakuta Magereza ilijengwa wakati ambapo Tanzania haina idadi ya Watanzania ambaao sasa tuko millioni 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa tu mfano, Gereza la Mpanda pale ambalo ilijengwa 1947 lilikuwa na uwezo wa kuchukua watu chini ya 200, lakini kwa sasa lina watu zaidi ya 800. Magereza kama hii, ziko nyingi hapa nchini na hivyo kusababisha mlundikano wa watu, lakini juhudhi mbalimbali zinafanyika na kwa kushirikiana na taasisi nyingine kama Magereza ambayo iko Wizara ya Mambo ya Ndani, sasa hivi kuna program za kujenga Magereza mapya na yale yaliyopo kuyaongezea uwezo ili tuweze kumudu idadi ya wahalifu ambaao kila uchwao wanaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kitu cha kuongezeka kwa wahalifu hatuwezi kukikwepa kwa sababu idadi yenye ya Watanzania ni kubwa na ukubwa huu unasababisha misukumano ya hapa na pale ambayo inasababisha kwenda kwenye vyombo vyaya utoaji haki; na wakati wa taratibu zile za kusubiri kukamilisha eneo hili la utoaji haki, basi yule aliyetuhumiwa anakuwa amehifadhiwa mahali ambapo vilevile kwake ni salama kwa upande mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Wabunge wote tushirikiane kwa sababu tunatoka kwenye maeneo hayo

tuone namna nzuri ya kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wetu ili wasiendelee kuingia kwenye makosa ambayo hawakuyatarajia, kusudi pamoja na mambo mengine tuendelee sasa kupunguza uhalifu nchini. Kwa sasa katika juhudzi za kupunguza msongamano, tuna vyombo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo cha kwanza ambacho kinatusaidia sana kupunguza msongamano ni pamoja na Mheshimiwa Rais kutoa msamaha kwa wale ambao vifungo vyao vinaonekana kufikia mwisho na kimsingi huko kumekuwa na idadi kubwa ya wafungwa ambao wanapata msamaha wa Rais.

Vilevile kwa kupidzia Mahakama, kujaribu kuziondoa kesi ambazo hazina mashiko. Vilevile tuna mfumo wa *plea bargaining* ambapo DPPkwa mamlaka aliyopewa amekuwa akijaribu sana kupunguza idadi ya wale mahabusu wetu ambao wengine wanasubiri kesi huko Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende eneo lingine la kubambikiwa kesi. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamesema kumekuwa na utaratibu wa kubambikiwa kesi kwa wananchi. Napenda kusema tu kwamba Serikali yetu tukufu kupidzia chombo chake cha utoaji wa haki hakina utaratibu wa kumbambikia mtu kesi. Hizi kesi mara nyingi kama kuna sura ya kubambikiwa, wanaanzana huko walikoanzia safari ya kuchokozana, lakini huwezi kukamatwa kwa kesi ya wizi wa kuku, ukafika Mahakamani ukaambiwa unashitakiwa kwa kosa la kuiba ng'ombe, haiwezekani. Kwa Serikali yangu hiki kitu hakipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye eneo hili la ubambikizwaji kesi, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, ushirikiano ni kitu muhimu sana. Tushirikiane kwenye mazingira, kwa sababu unaposema kubambikiwa kesi, inahitaji ushahidi wa kutosha kuonesha kwamba kweli mtuhumiwa au mlalamikiwa kabambikiwa kesi. Kwa sababu, mbambikiaji, yule anayefanya zoezi la kumbambikia kesi ni mhalifu kama wahalifu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukipata taarifa za mapema, maana yake huyo aliyehusika kubambika kesi atatueleza nia yake, naye anatakiwa kwenye vyombo vyaheria ili tukamwelewe vizuri, kwa nini aliweka nia ya kubambika kesi? Kama ni sehemu ya watumishi wetu wa Serikali, tunachukua hatua za haraka sana, kwa sababu kwanza huko ni kuidhalilisha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile suala la kubambika kesi lina uwezo wa kumalizika katika maeneo ya ngazi ya chini sana. Tukipata ushahidi wa kutosha kwamba, kweli katika mazingira yaliyo wazi au kulingana na mazingira yake inaonekana kuna watumishi wamejihusisha na kuwabambikia kesi wananchi wetu, kama nilivyosema mwanzo, hatua kali sana zinachukuliwa dhidi yao. Kwa hiyo, naomba sana tushirikiane.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwenye ngazi ya Mahakama, sisi tuna Kamati ya Maadili ya Mikoa ambayo Mwenyekiti wake ni Mkuu wa Mkoa na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na kwenye wilaya hali kadhalika. Sasa mambo haya yanapotokea katika ngazi hizo, tukiwa na uhakika sisi Wabunge, tupeleke haya maelezo kwa Wakuu wa Mikoa ili kama ni Hakimu amehusishwa na jambo hili, basi kamati zile zipitie kupitia ile Kamati ya Maadili, ili tuweze kumbaini na baadaye hatua za kisheria dhidi yake ziweze kuchukuliwa. Kama ni Idara ya Polisi, nako huko vilevile. Tunapopata Ushahidi inasaidia kwa sababu, jambo la kubambikia linahitaji ukaribu sana katika suala la kulithibitisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ile tu kwamba wamebambikiwa kwa maelezo ya mlalamikaji anapokuja kwako, inawezekana likawa na ukweli au lisiwe na ukweli. Hivyo, basi nawaomba tuwe na ushirikiano wa karibu sana. Mahakama ndio sehemu ambayo haki zote zinatolewa kwa kuzingatia sheria ambazo sisi Waheshimiwa Wabunge tumekaa hapa na tunazitunga ili ziende zikatumike vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyaeleza haya mawili kwene maeneo yangu sasa niache nafasi kwa Mheshimiwa Waziri ambaye kwa kweli, ndiye alikuwa mtoha hoja, aweze kutusaidia kukamilisha hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, ahitimishe hoja yake. (*Makofii*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hotuba ya Makidirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge 12 wamechangia hotuba hii, kati ya hao Waheshimiwa Wabunge 10 wamechangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge wawili wamechangia kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri. Tumepokeea maoni na ushauri wao ambao unalenga kuboresha utendaji wetu na utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ujumla. Maoni na ushauri wao uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni wenye tija na tunaahidi kufanya kazi. Aidha, tunaishukuru sana Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria na Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa maoni yao mazuri ambayo tutayazingatia na kuyatekeleza katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Wabunge wakati wa michango yao na nyingine tutaziwasilisha kwa maandishi kwa ufanuzi zaidi. Mheshimiwa Joseph Anania Thadayo kuhusu suala lake la

Mabaraza ya Ardhi, lile la upande wa Mahakama, uliliweka vizuri nami nisingependa tena kulizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mabaraza ya Ardhi na changamoto, napenda kufafanua kwamba Mabaraza ya Ardhi yameanzishwa rasmi na sheria inayotawala mabaraza hayo. Mwaka 2000 Serikali ilifanya tathmini kuititia Tume ya Kurekebisha Sheria kuhusu utendaji wa Mabaraza ya Ardhi hayo na kubaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo: changamoto za kimfumo, changamoto za kimaadili na changamoto ya uhaba wa rasilimali mali na changamoto ya kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, uamuzi wa Serikali ni kuwa mabaraza hayo yabaki chini ya Wizara ya Ardhi na TAMISEMI na yaboreshwe. Kwa hiyo, Wizara ya Katiba na Sheria inaendelea kushirikiana na Wizara husika ili kuboresha mifumo ya utendaji wa Mabaraza hayo ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji masuala yote aliyoyaainisha yanayohusu vifungu vya Katiba vya 133 na Ibara ya 135 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mambo hayo tumeyapokea, ni mambo yanayohusu Muungano na yatawasilishwa Serikalini ili yajadiliwe na Ofisi ya Makamu wa Rais, lakini pia Tume ya Pamoja ya Ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napenda nitoe indhari kwake kwamba Katiba hajitekelezi yenyewe, inatekelezwa na sheria, ndio maana yako mambo ndani ya Katiba ambayo huchukua muda kutekelezwa kwa sababu lazima sheria zijielekeze katika utekelezaji mzuri wa aina hiyo. Mambo ambayo ndani ya Katiba yamechukua muda kutekelezwa siyo kwa sababu Serikali haitaki yatekelezwe, lakini ni mambo ambayo yanahitaji mashauriano, majadiliano, maelewano ili hatomaye yatakapotekelezwa yatekelezwe kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yaliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespha Kabati, kwanza ni kuhusu

kucheleweshwa kwa mashauri bila sababu za msingi na ametoa mifano ya mashauri ya mauaji na ubakaji hasa huko Iringa. Hata hivyo, ningependa kusema kwamba, zipo sababu nyingi za mashauri hayo kuchelewa na sababu hizo ni mtambuka zinazohusu Mahakama, wadaawa, mawakili, mashahidi na wadau wote wa utoaji haki kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikija katika mashauri ya ubakaji na hasa yanapohusu wanafamilia, moja ya changamoto kubwa zinazopatikana ni ndugu kutokutaka kupelekana Mahakamani ili kulindana na Mahakama haiwezi kutoa maamuzi kuhusu masuala hayo bila mashahidi kwenda Mahakamani na kutoa ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naafikiana na Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba, kesi za mauaji ni nyingi kiasi katika Mkao wa Iringa na sababu zake Inafaa zibainishwe na wataalamu wa sosholojia na anthropolojia, kwa nini Iringa kesi za mauaji ni nyingi ili twende kwenye kiini cha matatizo ya watu wa Iringa kwa mujibu wa maelezo yake kwamba mauaji ni mengi, hatimaye pia tupunguze idadi ya kesi zinazokwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika kesi za mauaji nazo zinahitaji uchunguzi wa kutosha kabla ya kutoa maamuzi yanayohusika. Kwa hiyo, nalo ni eneo ambalo litafanyiwa utafiti zaidi ili kujua ni kwa kiasi gani tutapunguza idadi ya mashauri ya mauaji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maoni ya Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, moja ningependa kumweleza kwamba sababu za mahabusu kulundikana mahabusu, siyo moja tu, ziko sababu nyingi sana ambazo ameshazieleza Naibu Waziri. Kuhusu masharti ya dhamana katika mashauri ya jinai yameainishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 148 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Aidha, kifungu hicho kinaeleza wazi kuwa pale ambapo masharti ya dhamana yanataka kuweka Mahakamani mali isiyohamishika, siyo lazima kuweka hati ya

umiliki wa mali hiyo, bali ushahidi wowote unaothibitisha umiliki wa mali hiyo. Kwa hiyo, wananchi hawahitaji kupeleka hati hiyo, isipokuwa ushahidi wowote unaothibitisha umiliki wa mali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama pia imetoa mwongozo wa utoaji dhamana unaoelekeza mambo muhimu ya kuzingatia katika kutoa dhamana. Hata hivyo, kama mdaawa yejote hakuridhika na tafsiri ya Mahakama ya kifungu hicho katika mchakato wa kutoa dhamana, ana haki ya kukata rufaa katika Mahakama ya juu. Wote tunafahamu kwamba Mahakama ya Rufaa ya Tanzania katika uamuzi wake uliotolewa tarehe 5 Agosti, 2020 katika Shauri la Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Dickson Paul Sanga kupitia shauri la rufaa namba 175 la 2020 ilioa uamuzi wa kueleza kuwa Kifungu cha 148 (5) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashitaka ya Jinai ni kifungu halali kwa kujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ilieleza kuwa kifungu tajwa kinalenga kushughulikia zuvio la dhamana kwa washitakiwa wote waliofunguliwa mashitaka Mahakamani ambapo endapo wataruhusiwa kupata dhamana kunaweza kusababisha kuvurugika kwa amani, utulivu na usalama wa nchi, raia na watuhumiwa wenyewe. Ni rai yangu kwa niaba ya Serikali kwamba, watu wajiepushe na makosa haya na waendelee kuwa raia wema. Siyo nia ya Serikali wala Mahakama kuwanyima watu uhuru wao, lakini Serikali na Mahakama huchukua hatua hizo pale inapobidi na kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni yaliyotolewa na Mheshimiwa Mwasi Damas Kamani; moja, Tume ya Kurekebisha Sheria imekuwa inafanya mapitio ya mifumo ya sheria mbalimbali ili sheria hizo ziakisi mabadiliko yanayotokea na anayeweza kupeleka maombi hayo ni pamoja na Serikali yenyeve pamoja na Mahakama na hata raia anaweza akaiomba Wizara ya Katiba na Sheria kama mlivyofanya sasa, kupeleka maoni hayo kwa Tume ya Kurekebisha Sheria ili iyafanyie utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusitiza kwamba Sheria ya Tume ya Marekebisho ya Sheria haiielekezi tume hiyo kuleta ripoti yake Bungeni. Kwa hiyo, tume haileti ripoti zake Bungeni badala yake, inapeleka ripoti zake kwa Waziri wa Katiba na Sheria ambapo huziwakilisha Serikalini ili zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo mambo mengi aliyoyaeleza yanahu su sekta ya uchukuzi, sekta ya bima, lakini kwa sababu ameyaelekeza kwa upande wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Waziri wa Katiba na Sheria atayaangalia hayo; na kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, tutahakikisha kwamba mambo hayo nayo tunayatazama na kuona namna gani yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Mheshimiwa Salome Wyclife Makamba; moja ni kuhusu kupitia sheria za kusimamia mambo ya umri wa ndoa. Kwenye jambo hili ningependa nieleze kwa makini sana kwamba, maelezo yaliyotolewa huko nyuma kuhusu Sheria ya Ndoa ni vizuri tukazingatia kwamba Sheria ya Ndoa isihukumiwe kwa kifungu kimoja tu. Ule msemo wa samaki mmoja akioza, wote wameoza, siyo sahihi kwa Sheria ya Ndoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema niliyawahi kuyasema, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ndio sheria ya kimapinduzi ya ndoa katika bara la Afrika, *is the most progressive law of Marriage in Africa* kwa hiyo tusiihukumu kwa kifungu kimoja tu. Kifungu hicho kwa maoni yangu wakati ule na bado nayasimamia shauri hilo hilo lingeweza kupelekwa Mahakama ya Rufaa sio kupitia kifungu cha 13 cha ubaguzi bali kupitia kifungu cha haki ya kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa kama ni afya ni *the right to life*, lakini kwa kutumia sheria ya kifungu cha ubaguzi, tunaingia katika mtego kusahau kwamba kwa hali halisi ya Tanzania lazima tuwe na ubaguzi chanya kwa faida ya wanawake, lazima tuendelee kuwa na ubaguzi chanya kwa faida ya wanawake, ndio hiyo inaitwa *affirmative action*

ambayo pia ni ubaguzi lakini ni ubaguzi wa aina gani? Ni ubaguzi chanya na hadhari yetu ilikuwa tukiendelea kutumia mwanya wa ubaguzi kwa kifungu hiki tunaweza kuwa tunavunja msingi muhimu ambao umefanya wanawake wa Tanzania wapate ubaguzi chanya ili waendelee, wawakilishe Bungeni na ili wawe katika sehemu mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama ni kuhatarisha Maisha, ningekuwa mimi napeleka shauri hilo Mahakamani, ningepeleka chini ya *the right to life* na sio *the right against discrimination*. Hata hivyo, uamuvi wa shauri la Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Rebecca Jumi, Rufaa Na. 204 ya mwaka 2017 – 2019, Wizara ilianzisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Ndoa na Sheria ya Usimamizi wa Mirathi ili kuainisha umri wa kuolewa au kuoa kwa mwanamke na mwanaume mtawalia na hatimaye Februari, 2021, Serikali iliwasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ndoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara iliwasilisha mapendekezo ya kubainisha wasimamizi na warithi wa mali moja wa mwenza anapofariki. Kwa kuwa marekebisho ya Sheria ya Ndoa yanaihusisha jamii kwa ujumla wake, Serikali ilishauriwa kuwashirikisha wananchi ili kupata maoni kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo. Kwa hiyo tarehe 17 Machi, 2021, Wizara ilianza tena kufanya mikutano baina yake na viongozi wa dini na baadaye makundi mengine ili kupokea maoni husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeandaa mpango kazi wa kuyafikia makundi yote katika jamii ili kupata maoni yatakayowezesha kapatikana kwa sheria iliyoridhiwa na wote. Hadi sasa Wizara imeweza kukusanya maoni kutoka Mkoa wa Arusha, Mwanza na Dar es Salaam kutoka kwa baadhi ya viongozi wa kimila na kidini. Wizara itakapokamilisha zoezi la kukusanya na kupokea maoni katika eneo la mirathi na ndoa itayawasilisha mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Ndoa na Mirathi ili kuendana na hali ya maendeleo tuliyonayo bila kuathiri mila, desturi, tamaduni na dini zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yaliyotolewa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi tumeyapokea na ushauri wa Mbunge umezingatiwa isipokuwa ule wa kwenda kulala gerezani huo ni mgumu kidogo, lakini mengine yote tumeyapokea, tutaona jinsi ya kuyakamilisha. Yale matatizo ya wale waliodhaniwa wamevamia hifadhi na matrekta yafuate utaratibu wa kawaida ili kuona ukweli uko wapi, lakini kama kweli waliinggia katika hifadhi na hayo matrekta na ni hifadhi ambayo ipo katika bonde la Mto Kilombero ambalo ndilo linalolisha kiasi kikubwa cha maji Mto Rufiji, yaweza ikawa ni uhujumu uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mheshimiwa Mohamed Salum Mohammed Shaafi, Mbunge wa Chonga, kwanza sijawahi kusikia Mahakama Kuu ya Tanzania imeinyang'anya Mahakama Kuu ya Zanzibar shauri lolote, kwa sababu Mahakama haifungui kesi inapelekewa kesi. Kwa sababu Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi ni Mswahili anayekifahamu kiswahili vizuri nataka kuamini hakukosea aliyyoyasema na kama ni sahihi aliyyoyasema hata mara moja hakuna mahakama ye yote inayoinyang'anya mahakama nyingine kesi kwa sababu mahakama sio *ambulance*, haifuati mgonjwa, mahakama inapelekewa kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna kesi inayohusu raia wa Tanzania wenye asili ya Zanzibar katika Mahakama Kuu ya Tanzania basi yupo aliyeipeleka, lakini haiyumkini kabisa Mahakama Kuu ya Tanzania, ikainyang'anya Mahakama Kuu ya Zanzibar kesi. Hakuna mahakama inayojipelekea kesi, lakini kama ni shauri linalosemwa, ningependa niseme hivi, shauri ambalo lipo mahakamani na linaendelea ni shauri la Mashekhe wa Uamsho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 15 Septemba, 2020, shauri la jinai namba 21 la 2014 lilitokuwepo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Mkoa wa Dar es Salaam lilifunguliwa rasmi katika Mahakama Kuu ya Kanda ya Dar es Salaam mara baada ya upelelezi kukamilika. Mnamo tarehe 17 Septemba, 2020, mchakato wa kuhamisha kesi husika Mahakama Kuu yaani zinaitwa *committal*

proceedings ulikamilika, kesi hiyo ilikuwa ianze kusikilizwa tarehe tarehe 25 Machi, 2021, lakini kutokana na msiba uliotupata ilisogezwa mbele hadi mwanzoni mwa mwezi Aprili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Mahakama Kuu imeanza kusikiliza kesi hiyo namba 121 ya 2021 kuanzia tarehe 12 Aprili, 2021 na mahakama yenye wa uwezo wa kusema ina uwezo wa kusikiliza kesi hiyo au haiwezi, sio mimi wala mtoa hoja. Kwa hiyo tuiachie Mahakama Kuu ya Tanzania ambayo sasa imeanza kusikiliza shauri hilo, yenye we itajua mwenendo unavyokwenda na yejote ambaye hataridhika na maamuzi ya Mahakama Kuu bado anayo nafasi ya kukata rufaa Mahakama ya Rufani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo madam suala sasa lipo mahakamani, mikono yetu na midomo yetu sasa imefungwa suala hilo ni *sub judice* tuiachie Mahakama Kuu sasa lisikilizile shauri hilo na ile video inayotembea sana ilikuwa ni video ya maneno hayo niliyoyasema mwaka 2018 kabla ushahidi haujakamiliika. Sasa ushahidi umekamiliika *committal proceeding* zimekamiliika, kesi ipo Mahakama Kuu, tuiachie Mahakama Kuu itoe uamuzi wake na baada ya kutoa uamuzi wake asiyeridhika ipo Mahakama ya Rufani na mahakama hii ni Mahakama ya Muungano ndio maana yapo mashauri kutoka Mahakama Kuu Zanzibar yanakwenda Mahakama ya Rufani na yapo mashauri kutoka Mahakama Kuu ya Tanzania yanakwenda Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar mashauri ambayo hayaji huko ni mashauri yaliyoanza kwenye Mahakama za Kadhi au mashauri yanayohusu tafsiri ya Katiba ya Zanzibar, mengine yote yanakwenda mpaka Mahakama ya rufani na ndio pekee mahakama ya Muungano na inasikiliza rufani kutoka pande zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena, Mahakama Kuu ya Tanzania haijainyang'anya Mahakama Kuu ya Zanzibar kesi yoyote, ila kesi zimepelekwa na hizi mahakama mbili zina kitu kinaitwa *concurrent jurisdiction*, sasa

haiwezekani mmoja amnyang'anye mwagine, sasa tumtafute mwagine lakini kama yalikuwa ni makosa ya tafsiri, maana yake kesi imefunguliwa huku basi hilo ni jambo linguine, Mahakama yenye itaamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nilieleze hilo ili tuondoe munkari katika jambo ambalo linahitaji umakini mkubwa kabisa ili lisileté dhahama katika nchi yetu. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makosa yasiyokuwa na dhamana; kama nilivyo sema uhuru wa mtu yeote ndani ya Katiba yetu umewekewa mipaka. Tunazungumzia uhuru bila kwenda kwenye Ibara ya 30 ya Katiba yetu. Ibara ya 30 imeweka mipaka kwa uhuru wowote ule na mpaka wa kwanza mkubwa ni mwanzo wa uhuru wa mwenzako, ndio mwisho wa uhuru wako kwa hiyo hakuna uhuru usiokuwa na mipaka. Uhuru wowote una mipaka na hayo yameelezwa kwenye Ibara ya (30) ya Katiba yetu na pia kwenye maamuzi ya Mahakama ya Rufani ya kesi ya kukuchia ambayo Mahakama ya Rufani iliweka vigezo vya kuwekwa kwa mipaka hiyo ambavyo viro wazi kabisa. kwa hiyo hata kwenye suala la dhamana mipaka ipo ili kuyalinda na kuyaainisha hayo ambayo yapo ndani ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yaliyotolewa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka ni ya msingi sana kuhusu suala la Liwale. Tupende kueleza tu kwamba palitokea changamoto katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa Mahakama katika Mkoa wa Mtwara na Lindi. Mkoa wa Lindi haukuwa na Mahakama hata moja ya wilaya, tumeshajenga mahakama tatu Mchauka na Liwale ipo katika hatua hiyo. Kwa hiyo Liwale hajasahaulika ila ni kwa sababu ya changamoto kubwa ya mahitaji ya mahakama katika wilaya hiyo na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika muda mfupi tutaona ni jinsi gani pia Liwale tuiweke katika msimamo huo unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niliweka kiporo kidogo suala liliiloletwa na Mheshimiwa Restituta Taska Mbogo. Ni kweli kabisa kabla ya uhuru sheria za kimila zilikuwa

hazitambuliwi kabisa, wakoloni waliziona sheria za kimila ni sheria za kishenzi na ndoa za kimila ni ndoa za kishenzi, lakini pia Waafrika walikuwa hawapelekwi mahakamani walikuwa wanahukumiwa na Machifu au Watemi na rufaa zao zilikuwa zinakwenda kwa Mkuu wa Wilaya. Zikitoka kwa Mkuu wa Wilaya, kwa Mkuu wa Jimbo, zikitoka kwa Mkuu wa Jimbo zinakwenda kwa Gavana. Mahakama ilikuwa ni kwa ajili ya Wazungu na Wahindi tu, ndio maana tunapata Uhuru mwaka 1961 waliopigania uhuru wa nchi hii na mmoja Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye yeye mwenyewe katika essay yake ya *Socialism and Rural Development* anaeleza ubovu wa baadhi ya mila zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere bado aliona ni muhimu kwanza kuzitambua sheria za kimila kuwa ni sheria za watu wastaarabu na sio sheria za watu washenzi, ndio maana mwaka 1963 tunafanya *codification* ya *Customary Law* lakini *codification* hiyo ya *Customary Law* ya mwaka 1963 ilifanya pia mabadiliko ndani ya hizo sheria za kimila na ilitungwa chini ya Sheria za Serikali za Mitaa, kwa mfano kuhusu suala la wanawake kurithiwa wanapokuwa wamefiwa na wanaume zao, sheria ile iliongeza kipengele iwe kwa hiyari yake kama hataki asirithiwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hiyo ilikuwa imepiga hatua kubwa kuliko sheria ya maandishi kwa sababu ndio sheria ambayo ilisema kitanda hakizai haramu, maana yake nini, haikutaka ubaguzi wa watoto ndani ya ndoa. Kwa hiyo sio kila sheria ya mila ichukuliwe jinsi ilivyo, ilifanyiwa marekebisho ili iendane na hali inayotakiwa. Sasa sheria hii imetungwa chini ya Sheria za Serikali za Mitaa, ndio maana ni muhimu tena Mabaraza ya Madiwani wa Halmashauri za Mitaa wazipitie tena sheria za mila na kuzuhisha kwa mazingira yaliyopo, lakini kuzituhumu na kusema sheria zinazotungwa na Bunge tu ndio sheria nzuri, tunarudi kuwatukana wahenga wetu kama walivyotukanwa na wakoloni kwamba sheria zao ni za kishenzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siamini sheria za mila ni za kishenzi, yapo maeneo ni muhimu yarekebishwe, lakini

kuzitupa moja kwa moja tukumbuke msemo wa Kiswahili *Mkataa asili ni mtumwa*. Hii isieleweke natetea sheria za kimila hivi hivi, lakini leo tuna mwanya mwingine, Katiba yetu ina sura nzima za haki za binadamu, bado mtu anaweza kwenda mahakamani kusema sheria hii ya kimila kwenye eneo hili inakwenda kinyume na haki za binadamu na mahakama ikafanya marekebisho ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mambo yaliyorekebisha na mahakama ni kuhusu kwa makabila yale ya ubabani, maana yake hapa Tanzania kuna makundi mawili ya makabila, makabila ya ubabani na makabila ya umamani, hakuna mjomba ni umamani. Kuanza kusema hawa ni wa upande wa wajomba ni kuwadhalilisha akinamama, ni makabila ya ubabani (*Patrilineal*) na makabila ya umamani (*matrilineal*).

Mheshimiwa Naibu Spika, huku kwenye makabila ya ubabani ukiisoma kesi ya Benardo Ephrahim dhidi ya Horaria Pastory na Gervas Kaizelege, Mahakama ilisema wazi kabisa sheria ya kumzuia mwanamke kurithi ardhi ni kinyume cha Katiba, ndio sheria ya Tanzania sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hivyo tu, ukisoma shauri lilihofanywa na Jaji Kisanga kwenye kesi ya Haji Athuman Issa dhidi ya Routama Mituta imesema hivyo hivyo kwamba, sheria ye yote inayomnyima binti kurithi mali ikiwa ni ardhi ni kinyume cha Katiba. Kwa hiyo tuzisome sheria hizo na maamuzi ya mahakama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona hatari, Watanzania tumeanza kusahau kwamba sisi mfumo wetu wa sheria ni wa *common law* na kwenye *common law* huisomi sheria tu, unaisoma sheria pamoja na maamuzi ya mahakama ili kupata *jurisprudence* ya eneo hilo. Ningelewa msimamo huu kama ingekuwa tupo *continental Europe* na nina bahati ya kusoma katika mifumo yote miwili; nimesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, common law nimesoma Freie Universität Berlin ambayo ni *civil law*. Kwenye *civil law* hoja hiyo ina msingi, lakini sisi ni lazima daima turejee katika

mashauri ya mahakama ili kujua sasa tafsiri ya sheria ni nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi ni watu wa *common law*, tuache na sisi wanataaluma sasa tuanze kutoa *commentary* ili watu wanaposoma kifungu cha Katiba ajue na maamuzi ya Mahakama ambayo yametoa tafsiri hiyo. Hata kabla ya hapo kuna Jaji mmoja Mkuu wa Tanzania tunamsahau mara nydingi sana na ndio alikuwa Jaji Mkuu wa kwanza Mtanzania Jaji Augustino Said; katika shauri la Ndewauyosia *Daughter of Mbehanso* dhidi ya Emmanuel Son of Malasi ya mwaka 1968 alisema Sheria ya Wachaga ya kuwazuia wasichana kurithi kihamba ni kinyume. Kwa hiyo ukiyachukua maamuzi yote haya, tayari yamekwishakupa mwelekeo wa nini msimamo wa sheria za Tanzania kuhusu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu, kuna mradi ambaao uliana katika Tume ya Kurekebisha Sheria kwa sababu mwaka 1963 *codification* ya *Customary Law* ifanyiwa tu kwa makabila ya ubabani, makabila ya umamani hawakuwafanya *codification* ya *matrilineal* na hayo yameleta matatizo makubwa na hasa katika mahakama zetu. Baadhi ya Mahakimu wanaofanya hivyo ni mahakimu ya jinsia ya kike kwa sababu hawajui mfumo wa sheria wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa mmojawapo ni wa Morogoro ambapo baadhi ya watoa haki hawaelewi kwamba kule wasimamizi wa ardhi ya ukoo ni wanawake; ni mama na dada. Kwa hiyo mama na dada wanapokwenda kusema kaka hakuwa na haki ya kufanya hivi kimila hawaelewi na mara nydingi hawaelewi kwa nini wasimamizi wa mirathi ni madada na sio makaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo asilimia 20 ni muhimu Serikali sasa itafanya juhudii ili sheria za kimila za watu wa umamani ambazo mimi naamini zitawasaidia wale wa sheria za mila za ubabani na wao kubadilika wakati ndio huu. Tukizipitia zile sheria hatuna haja ya kwenda kwa wataalam

wa *gender* wa Marekani, wataalamu wa *gender* wa Ulaya, twende kwa wataalam wa *gender* wa Kimwera, Kimakua, Kiya, Kimakonde, Kikwera, Kizaramo, Kikaguru, Kikutu, Kinguu na Kiluguru, tutapata majibu ya jinsi gani ya kumfanya mwanamke achukue nafasi yake ambayo anaichukua katika jamii hizo za sheria za umamani. Tofauti na sisi wengi ambao tunaishi katika sheria za ubabani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nilieleze hili kwa muda kidogo ili niliweke wazi kwamba tunao utajiri ambao utatusaidia ndani ya Tanzania kubadilisha sheria zetu kwa sababu shida kubwa ya *gender studies* tumeanza kusoma *European gender studies*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda katika mukano mmoja, wao matatizo yao makubwa sasa ni kwa nini bei ya sidiria ni kubwa kuliko bei ya shati. Sasa leo mjadala wa bei ya sidiria kuwa na bei kubwa kuliko shati Tanzania haina maana, sisi maana ni wanawake waweze kumiliki mali, wanawake waweze kufanya hivyo, lakini kwa wao mambo ya kumiliki mali na kufungua akaunti yalikwisha, sasa wanahangaikia bei ya sidiria na bei ya shati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo ambalo linahitaji umakini na nilliona niliweke mwisho ili nilitolee ufanuzi na tulifanyie kazi. Mengine yale yote tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha naomba tena Bunge lako likubali na kuidhinisha kiasi cha shilingi 78,464,886,000 kwa ajili ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake na shilingi 153,228,859,000 kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa wabunge hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu. Katibu!

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MATUMIZI YA KAWAIDA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge Fungu hili ndiyo lina mshahara wa Waziri ambapo nimeletewa majina hapa ya Wabunge ambao wanahitaji ufanuzi na kulingana na utaratibu tulionao vyama vimeshaleta majina hapa tutaanza na Mheshimiwa...

FUNGU 41 - WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management* ... Sh. 7,466,974,000

MWENYEKITI: Ahsante sana nimeshaletewa majina hapa Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ni kweli natarajia kushika shilingi ya Waziri kama majibu ya nitakachomuuliza hayata nirdhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita tulifanya uzinduzi wa mahakama zinazotembea na kwa uelewa wetu mahakama hizi ziliwalenga sana watu wengi ambao wako mbali na sehemu za kupatia haki na ukizingatia sisi tunakotoka watu wanafuata huduma ya haki mahakamani zaidi ya kilomita 100 mpaka na 120 na magari haya baada ya kuzinduliwa yanazunguka tu mjini ambako kuna mahakama karibu kila mtaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi wa kutosha nisiporidhia nitaendelea kumshikia shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ufanuzi .

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru ndugu Mheshimiwa Musukuma kwa kulileta suala hili la mahakama zinazotembea. Ni kweli tumeanzisha mahakama hizi zinazotembea na mpaka sasa tumezianzisha kwa majaribio katika Mkoa wa Mwanza na katika Mkoa wa Dar es Salaam. Na sasa Mhimili wa Mahakama unafanya tathmini ya utekelezaji wa matumizi ya hizi Mahakama zinazotembea katika Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Mwanza kwa lengo sasa la moja kuisambaza huduma hiyo katika Mikoa mingi zaidi, lakini pia kwa lengo la kuboresha zaidi utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kweli magari haya hasa kwa Dar es Salaam yamekuwa ni mji kwasababu ya ukubwa wa mji wa Dar es Salaam na hivyo hivyo katika mji wa Mwanza. Lakini ni lengo la Serikali sasa tutakapokamilisha tathmini ya hizo Mahakama zinazotembea na wote tunavyokumbuka hapa Bungeni halikuwa suala rahisi kueleweka tutaanza Mahakama hizo kwenda vijijini na siyo vijijini tu tunataka sasa kuwa na *mobile court* maalum kwa ajili ya kesi za mirathi, ndoa na Watoto na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunafikiria uwezekano wa kuwa na mashua au boti ambazo pia zitakuwa ni mahakama zinazotembea katika maziwa ukichukua kwamba Ziwa Victoria Ukerewe peke yake ina zaidi ya vijiji 40. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Musukuma aniachie hiyo shilingi ili sasa tukamilishe tathmini ya *mobile court* na baada ya hapo sasa tuzipanue zaidi ikiwa ni Pamoja na kwenda vijijini lakini kwenye visiwa mbalimbali vyat Ziwa Victoria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ninakubali kumrudishia shilingi yake lakini nimuombe tathmini hiyo iongeze spidi maana yake tathmini

ya miaka minne na sipendi kumwambia Prof. maneno mabaya kwasababu ni mwalimu wangu naridhia. (*Makof/ Kicheko*)

MWENYEKITI: Kweli safari hii tumepata mwalimu wa Mheshimiwa Musukuma! Humu ndani. Mheshimwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwenye mchango wangu nilielezea kuhusiana na Waziri kuleta mabadiliko ya sheria ya ndoa kifungu cha 13 na 17 kama ambavyo inaelekezwa na mahakama ili tuweze kuwanusuru mabinti zetu kuhusiana na mambo ya ndoa na mimba za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu na nisiporidhishwa na majibu ya Waziri nakusudia kushika shillingi. Waziri anasema mwezi wa kwanza mwaka huu alileta Muswada wa kujadili sheria ya ndoa kuhusiana na mambo ya ndoa na mirathi, mwezi wa kwanza Muswada ulioletwa ulikuwa unaongelea habari ya kubadilisha lugha ya mahakama iwe ya Kiswahili. Hiyo Habari anayoisema Mheshimiwa Waziri mimi sina Habari nayo na hatukuiona na Miswada yote inakuwa-*tabled* ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaturudisha nyuma hoja zote alizozisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikata rufaa akiwa na hoja tano mojawapo ni hiyo ya ubaguzi, akakata rufaa kuhusiana zilikuwa hoja tano na hoja zote zilikuwa na mjadala mkubwa ndani ya Mahakama ya Rufani na mwisho wa siku Mahakama ya Rufani ikatoa *judgement* yenye page 52 ikiielekeza Wizara na Mwanasheria Mkuu wa Serikali walete mabadiliko ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hadithi anayotusimulia Mheshimiwa Waziri kwamba amepeleka kwa wadau ndiyo *procedure* inavyotaka hivyo? Kwamba ukitoka Mahakama ya Rufani unatakiwa upeleke jambo kwa wadau wakati Mahakama ya Rufani imeshaelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atupe ufanuzi na nisipokubaliana naye nitaomba Wabunge wenzangu mniunge mkono tuwatetee wasichana wa Kitanzania wanaolewa katika umri mdogo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kabla hujasimama kwasababu kuna hoja hapo ya kwamba Serikali ilishaleta Muswada na ikashauriwa kwa hiyo hilo sasa nalazimika kulitolea maelezo.

Mheshimiwa Salome Makamba utaratibu wetu hapa wa Kibunge unapoingia Muswada humu ndani ni kwamba kuna vikao vinakuwa vimeshakaa huko na ukafika hapa ndiyo utaratibu ulivyo. Kwa hiyo siyo kwamba anatoka huko atokako Waziri anauleta hapa halafu labda viongozi wa Bunge tunapatia taarifa hapa kwamba kumbe ndiyo Muswada huu, hapana. Kwa hiyo taarifa aliyoitao Waziri yuko sahihi Muswada ulikuja ukiwa na marekebisho ya sheria nydingi tu siyo hiyo ya ndoa peke yake, na hiyo ya Kiswahili ilikuwa ni mojawapo.

Sasa nimelazimika kutoa maelezo kwasababu maelezo aliyyoatoa Waziri kwamba Muswada ulikuja ni kweli ulikuja kama alivyosema. Kwa hiyo, Mheshimiwa Salome ni kweli wewe hufahamu lakini nafahamu kwamba Muswada ulikuja na viongozi wa Bunge kwa maana ya wale wanaomshauri Mheshimiwa Spika ndiyo waliompa huo ushauri na uzuri viongozi wake hawatoki nje ya Bunge wanatoka humu Bungeni. Ndiyo waliompa ushauri kwamba hilo jambo lipite kwanza huko kabla ya humu ndani kwasababu humu ndani vikao vingi vikifanyika hata ngazi ya kamati zetu tunavutana. (*Makofii*)

Kwa hiyo akashauriwa liende kwanza huko likamalize linapokuja hapa iwe rahisi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Salome kwa maelezo hayo wala usiwe na wasiwasi hata na mimi, mimi ni mmoja wa watu ambaa naamini hata miaka 18 haitoshi kwa ndoa kwa kweli kwa mtoto wa kike. Miaka 18 hana uwezo japokuwa sisi tunafikiri 18 ndiyo anao uwezo miaka 18 hana uwezo wa kuzaa na hana uwezo wa kuhimili

ndoa. Kwa hiyo, sheria itakapokuja hapa tutaelewana vizuri wakati huo lakini kwa sasa nadhani haya maelezo yanatosheleza.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Salome hoja yako maelezo ni hayo niliyoyatoa mimi ili tusiliweke kwa namna ambayo pengine haistahili. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeletewa hapa majina yaliyokuwa yanaomba ufanuzi yalikuwa ni mawili na ndiyo hayo ambayo moja nimeshatoa ufanuzi kwasababu alichokisema Waziri kilikuwa sahihi.

(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit* Sh. 412,999,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Division* Sh. 917,343,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit* Sh. 195,321,000
Kifungu 1005 - *Government Communication Unit*.....Sh. 63,408,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*Sh. 211,972,000
Kifungu 1007 - *Information and Communication Technology Unit* Sh. 323,556,000
Kifungu 2001 - *Human Right Division* Sh. 625,692,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 2004 - *Public Legal Services Division* ... Sh. 836,847,000

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyezekiti, Vote 21114 ikiambatana na Vote 21121 kwenye miaka hii miwili ya nyuma hiki kifungu naona ilikuwa haitengewi fedha lakini sasa naona mwaka huu kuna imetengewa fedha kuna mabadiliko ya aina gani? Nikijaribu kufuatilia hata vifungu vingine vilivyopita sasa hivi kwenye huku *allowance allowance* naona tumechangulzia nataka njue sasa ndiyo tumeanza kufungulzia ma-*allowance* au vipi.

MWENYEKITI: 2000 na ngapi?

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: 2004 Vote 21121

MWENYEKITI: *Sub Vote 2004 lakini kifungu kipi? 21114 Personnel allowances.*

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Na 121.

MWENYEKITI: *Okeyna 121 Mheshimiwa Waziri vifungu hivi havikuwa na fedha kabla na sasa vimewekewa fedha? Ni nini kilichobadilika?*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Imeongezeka kutokana na kuongezeka kwa baadhi ya viwango vya posho.

(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2005 – *Natural Wealth and Resource Observatory* Sh. 443,820,000
Kifungu 4001 – *Constitutional and Justice Monitoring Division* Sh. 456,818,000

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 12 - TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management* ... Sh. 1,343,731,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* Sh. 61,780,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Division* Sh. 48,310,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit* Sh. 17,745,000

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge hasa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi sauti huwa zinaangia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge sasa mtu atakapokuja kujiuliza kama hivi vifungu vilipita ama havikupita atasikia sauti za watu ambao wanaitikia. Kifungu kinaafikiwa

Kifungu 1005 – *Recruitment Appointment and Confirm* Sh. 462,160,000
Kifungu 1006 – *Ethics and Discipline Section* ...Sh. 1,006,840,000
Kifungu 1007 – *Planning Monitoring and Evaluation* Sh. 65,240,000
Kifungu 1008 - *Information and Communication Technology Unit* Sh. 94,750,000
Kifungu 1009 – *Legal Services Unit* Sh. 19,635,000

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 16 - OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management* Sh. 2,112,129,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts* Sh. 357,232,000
Kifungu 1003 – *Planning Division* Sh. 466,488,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit* Sh. 200,030,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit* Sh. 139,370,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit* Sh. 170,208,000
Kifungu 1008 – *Research and Library Service Unit* Sh. 79,060,000
Kifungu 1009 – *Information and Communication Technology Unit* Sh. 205,976,000
Kifungu 2001 – *Coordination and Advisory Services* Sh. 949,632,000
Kifungu 2003 – *Legislative Drafting* Sh. 1,465,227,000
Kifungu 3002 – *Treaties and Contracts Division* Sh. 948,424,000
Kifungu 5001 – *Regional Attorney General's Office DSM* Sh. 133,015,000
Kifungu 5002 - *Regional Attorney General's Office Arusha* Sh. 59,064,000
Kifungu 5003 - *Regional Attorney General's Office Mbeya* Sh. 53,900,000
Kifungu 5004 - *Regional Attorney General's Office Kilimanjaro*... Sh. 54,584,000

Kifungu 5005 - *Regional Attorney*
 General's Office Mtwara Sh. 57,900,000
Kifungu 5006 - *Regional Attorney*
 General's Office Mwanza Sh. 57,584,000
Kifungu 5007 - *Regional Attorney*
 General's Office Kagera Sh. 48,568,000
Kifungu 5008 - *Regional Attorney*
 General's Office Tabora Sh. 55,900,000
Kifungu 5009 - *Regional Attorney*
 General's Office Tanga Sh. 58,900,000

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 19 - OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Kifungu	<i>1001 – Administration and Human Resource Management.</i>	... Sh. 7,243,703,800
Kifungu	<i>1002 – Finance and Accounts Unit</i>	... Sh. 142,528,200
Kifungu	<i>1003 – Planning Division</i>	... Sh. 156,905,500
Kifungu	<i>1004 – Internal Audit Unit</i>	... Sh. 89,252,700
Kifungu	<i>1005 – Procurement Management</i>	... Sh. 131,003,600
Kifungu	<i>1006 – Information and Communication Technology Unit</i>	... Sh. 329,535,500
Kifungu	<i>1007 – Government Communication Unit</i>	... Sh. 136,754,500
Kifungu	<i>1008 – Library Services and Research Unit</i>	... Sh. 89,252,700
Kifungu	<i>1009 – Legal Registry Unit</i>	... Sh. 198,679,100

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna kitu kimeandikwa hapa ukurasa wa 74 juu kabisa ndiyo tunakita futia maelezo. Mheshimiwa Waziri uko na kitabu hapo? Ukurasa wa 74 juu kabisa hapo, kuna hiyo bilioni 8, kwa sababu hiyo haijahojiwa ndiyo naitafuta hiyo imejumlisha ipi na ipi, maana yenyewe haijatajwa, washa kipaza sauti *Chief Whip.*

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI - KAIMU MNADHIMU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naiona hii ni *total* ya hizi *subvote* zinazoanza na 1001 mpaka hii 1009 ndiyo *total* yake inakuja Sh. 8,517,616,600/=.

MWENYEKITI: Sawa. Haya, Katibu tuendelee.

Kifungu 2001 – *Case Management and Quality Assurance*Sh. 578,805,500

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Aha, ni kwenye hiki kifungu cha 2001.

MBUNGE FULANI: Ndiyo.

MWENYEKITI: Pole sikukuona na tumeshahoji kwa sababu tukishahoji hatuwezi kufungua tena, utuwie radhi. Katibu.

Kifungu 2002 – *Arbitration Division*.....Sh. 1,641,856,500

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2003 – *Litigation Division*.....Sh. 1,393,069,400

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata uafanuzi kidogo maana hii *trend* tunayokwenda nayo naona kama hivi vifungu *vya personal allowance* vimerejea kwa nguvu sana, kila *Vote* ina vifungu *vya personal allowance* na miaka miwili mfululizo vilikuwa havitengewi fedha, lakini sasa imeanza kutengewa fedha nataka kupata maelezo.

MWENYEKITI: Huwezi kuyapata ya jumla tukishafika hapa, tutajie kifungu.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu cha 21114.

MWENYEKITI: Kifungu cha 21114 - *personal allowances*, shilingi 30,000,000, Waziri umeiona hiyo, maelezo?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, akisoma ataona hiyo ni fedha iliyowekwa na imeelezwa wazi ni *discretionary optional*/maana yake hawa Mawakili wa Serikali wakati mwingine wanalazimika kufanya kazi nje ya muda wao au katika mazingira maalumu. Kwa hiyo, ni posho ambayo imewekwa ili iwe na kasma ili ikitakiwa kulipwa inaweza kulipwa kwa mahitaji maalumu.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Hapa huwezi kusimama mara mbili Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri pale mwanzo ilikuwa inahusiana na hiyo hiyo, hizi *allowances* zilikuwa hazitajiki hiyo miaka miwili ya nyuma?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema katika kutambua uzito wa kazi wanayoifanya Mawakili wa Serikali na hasa hii *Vote 19*, sote tunafahamu kwamba ofisi ni mpya na wakati inaanza vitu vingi vilikuwa havijaangaliwa na ilikuwa inabebwa kwa kiasi kikubwa pia na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mashtaka ya Taifa. Sasa kila muda unapokwenda baadhi ya majukumu yamekuwa yanarudi katika ofisi yenye we ya Wakili Mkuu wa Serikali na kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nadhani sasa tumeelewa vizuri.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 35 – OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA

Kifungu 3001 – <i>Fraud, Money Laundering and Corruption Offence</i>	Sh. 784,149,000
Kifungu 3002 – <i>Assets Forfeiture Transnational & Specialized Crimes</i>	Sh. 793,395,000
Kifungu 3003 – <i>Case Management, Coordination of Criminal Cases</i>	Sh. 782,498,000
Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resource Management</i>	Sh. 5,001,403,000
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> ...	Sh. 409,098,000
Kifungu 1003 – <i>Planning Division</i>	Sh. 352,298,000
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 198,532,000
Kifungu 1005 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 152,923,000
Kifungu 1006 – <i>ICT and information Unit</i>	Sh. 149,454,000
Kifungu 1007 – <i>Government Communication Unit</i>	Sh. 157,688,000
Kifungu 1008 – <i>Research and Library Services Unit</i>	Sh. 142,394,000
Kifungu 1009 – <i>Legal Registry Unit</i>	Sh. 195,201,000
Kifungu 2002 – <i>Civilianization and Prosecutions</i>	Sh. 806,577,000
Kifungu 2004 – <i>Regional Office Arusha</i>	Sh. 816,008,000
Kifungu 2005 – <i>Regional Office Dodoma</i>	Sh. 420,189,000
Kifungu 2006 – <i>Regional Office Dar es Salaam</i>	Sh. 1,679,156,000
Kifungu 2007 – <i>Regional Office Iringa</i>	Sh. 422,159,000
Kifungu 2008 – <i>Regional Office Moshi</i>	Sh. 408,593,000
Kifungu 2009 – <i>Regional Office Kagera</i>	Sh. 381,453,000
Kifungu 2010 – <i>Regional Office Mbeya</i>	Sh. 481,598,000
Kifungu 2011 – <i>Regional Office Mtwara</i>	Sh. 378,115,000
Kifungu 2012 – <i>Regional Office Mwanza</i>	Sh. 880,009,000
Kifungu 2013 – <i>Regional Office Ruvuma</i>	Sh. 289,507,000
Kifungu 2014 – <i>Regional Office Sumbawanga</i>	Sh. 386,528,000
Kifungu 2015 – <i>Regional Office Tabora</i>	Sh. 499,621,000
Kifungu 2016 – <i>Regional Office Tanga</i>	Sh. 507,590,000
Kifungu 2017 – <i>Regional Office Shinyanga</i>	Sh. 448,603,000
Kifungu 2018 – <i>Regional Office Singida</i>	Sh. 333,992,000

Kifungu 2019 – *Regional Office Lindi* Sh. 280,928,000
Kifungu 2020 – *Regional Office Mara*..... Sh. 363,789,000
Kifungu 2021 – *Regional Office Manyara* Sh. 192,275,000
Kifungu 2022 – *Regional Office Kigoma* Sh. 262,136,000
Kifungu 2023 – *Regional Office Pwani* Sh. 318,344,000
Kifungu 2024 – *Regional Office Njombe*..... Sh. 290,114,000
Kifungu 2025 – *Regional Office Morogoro* Sh. 359,004,000
Kifungu 2026 – *Regional Office Geita*..... Sh. 317,226,000
Kifungu 2027 – *Regional Office Simiyu* Sh. 216,752,000
Kifungu 2028 – *Regional Office Katavi*..... Sh. 223,992,000
Kifungu 2029 – *Regional Office Songwe* Sh. 185,521,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 40 - MFUKO WA MAHAKAMA

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resource Management*.... Sh. 72,685,298,744
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.... Sh. 395,254,000
Kifungu 1003 – *Planning and Monitoring Division*.... Sh. 702,836,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*.... Sh. 209,048,700
Kifungu 1005 – *Information, Communication & Technology Unit*.... Sh. 336,640,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*.....Sh. 353,615,000
Kifungu 1008 – *Estates Management Unit*.... Sh. 356,674,900
Kifungu 1009 – *Records Management Unit* Sh. 273,485,000
Kifungu 1010 – *Library Services Unit*.... Sh. 173,559,900
Kifungu 1011 – *Legal Services Unit*.... Sh. 50,943,500
Kifungu 2001 – *High Court Main Registry*.... Sh. 1,629,036,900
Kifungu 2002 – *Court of Appeal Dar es Salaam*.... Sh. 1,865,300,099
Kifungu 2003 – *High Court Zones*.... Sh. 9,372,600,960
Kifungu 2004 – *High Court Divisions* Sh. 3,341,184,300
Kifungu 2005 – *Resident Magistrate Courts* ...Sh. 5,382,638,000
Kifungu 2006 – *District Courts*.... Sh. 7,901,689,072
Kifungu 2007 – *Primary Courts*.... Sh. 7,050,157,168

Kifungu	2008 – <i>Case Management</i>	
	<i>Division.....</i>	Sh. 491,002,805
Kifungu	2009 – <i>Judicial Service Inspection,</i>	
	<i>Supervision & Ethics</i>	Sh. 147,953,952
Kifungu	2010 – <i>Judiciary Delivery Unit</i>	Sh. 319,940,000
Kifungu	2065 – <i>Primary Court Magistrate Dodoma.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2185 - <i>Primary Court Magistrate Kigoma.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2202 - <i>Primary Court Magistrate Bariadi.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2226 - <i>Primary Court Magistrate Handeni.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2244 - <i>Primary Court Magistrate Ngara.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2252 - <i>Primary Court Magistrate Mbanga</i>	Sh. 0
Kifungu	2254 - <i>Primary Court Magistrate Tunduru</i>	Sh. 0
Kifungu	2259 - <i>Primary Court Magistrate Moshi</i>	Sh. 0
Kifungu	2261- <i>Primary Court Magistrate Same</i>	Sh. 0
Kifungu	2263 - <i>Primary Court Magistrate Rombo.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2265 - <i>Primary Court Magistrate Siha</i>	Sh. 0
Kifungu	2267 - <i>Primary Court Magistrate Mwanga.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2269 - <i>Primary Court Magistrate Hai</i>	Sh. 0
Kifungu	2273 - <i>Primary Court Magistrate Iringa</i>	Sh. 0
Kifungu	2275 - <i>Primary Court Magistrate Kilolo.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2277 - <i>Primary Court Magistrate Mufindi.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2296 - <i>Primary Court Magistrate Mpanda</i>	Sh. 0
Kifungu	2302 - <i>Case Management Division.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2303 - <i>Complaints Management</i>	
	<i>and Inspectorate.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2304 - <i>Primary Court Magistrate Kinondoni.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2308 - <i>Shinyanga High Court.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2310 - <i>Mediation Centre.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2311 - <i>District Magistrate Meru</i>	Sh. 0
Kifungu	2312 - <i>Primary Court Magistrate Meru.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2320 - <i>District Magistrate Kigamboni.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2321 - <i>Primary Court Magistrate Kigamboni.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2324 - <i>District Magistrate Tanganyika.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2325 - <i>Primary Magistrate Tanganyika.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2326 - <i>Corruption and Economic</i>	
	<i>Crimes Court.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2327 - <i>Judiciary Delivery Unit.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2328 - <i>Mbeya Juvenile Court.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2329 - <i>Primary Court Magistrate Illemela.....</i>	Sh. 0
Kifungu	2330 - <i>Primary Courts Magistarate Kalambo</i>	Sh. 0

Kifungu 2331 - *Resident Magistrate Songwe*.....Sh. 0
Kifungu 2332 - *District Magistrate Songwe*Sh. 0
Kifungu 2333 - *Primary Court Magistrate Songwe*.....Sh. 0
Kifungu 2334 - *Primary Court Magistrate Momba*.....Sh. 0
Kifungu 2335 - *Primary Court Magistrate Nyasa*.....Sh. 0
Kifungu 2336 - *District Magistrate Malinyi*Sh. 0
Kifungu 2337 - *Primary Court Magistrate Malinyi*.....Sh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 55 – TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*Sh. 2,661,892,295
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.... Sh. 217,886,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*.... Sh. 118,910,000
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit*.... Sh. 385,668,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*.... Sh. 136,914,000
Kifungu 1006 – *Management Information System Unit*... Sh. 195,285,295
Kifungu 1007 – *Planning Monitoring and Evaluation Unit*... Sh. 149,739,200
Kifungu 2001 – *Complaints and Investigation Division*.... Sh. 1,011,548,500
Kifungu 2003 – *Public Education, Comm, Research & Documentation*.... Sh. 464,261,800
Kifungu 3001 – *Zanzibar Office*.... Sh. 291,308,600
Kifungu 3002 – *Mwanza office* Sh. 220,715,300
Kifungu 3003 – *Lindi Office* Sh. 85,465,310
Kifungu 3004 – *Pemba Branch* Sh. 62,753,000
Kifungu 3005 – *Dar es Salaam Office* Sh. 343,488,700

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 59 – TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource Management</i>	Sh. 1,674,142,000
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh.233,865,000
Kifungu 1003 - <i>Planning and Coordination Unit</i>	Sh. 133,690,000
Kifungu 1003 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.146,240,000
Kifungu 1005 - <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 100,739,000
Kifungu 1006 - <i>Public Legal Awareness Unit</i>	Sh. 224,769,000
Kifungu 1007 - <i>Law Review Unit</i>	Sh. 367,950,000
Kifungu 1008 - <i>Law Research Unit</i>	Sh. 363,534,000

(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 16 – OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Kifungu 1001- <i>Administration and Human Resource Management</i>	Sh. 1,000,000,000
<i>(Kifungu Kiliviyotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)</i>	

FUNGU 35 - OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource Management</i>	Sh. 3,000,000,000
Kifungu 2002 - <i>Civilianization and Prosecutions</i>	Sh. 393,616,000
Kifungu 3001 - <i>Fraud, Money Laundering and Corruption Offence</i>	Sh. 600,000,000

Vifungu Viliviyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 40 – MFUKO WA MAHAKAMA

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource Management</i>	Sh. 0
Kifungu 1003 - <i>Planning and Monitoring Division</i>	Sh. 40,190,000,000
Kifungu 1005 - <i>Information, Comm. and Technology Unit</i>	Sh. 0
Kifungu 1008 - <i>Estates Management Unit</i>	Sh. 0
Kifungu 2001 - <i>High Court Main Registry</i>	Sh. 0
Kifungu 2010 - <i>Judiciary Delivery Unit</i>	Sh. 0
Kifungu 2302 - <i>Case Management Division</i>	Sh. 0
Kifungu 2303 - <i>Complaints Mgmt. and Inspectorate</i>	Sh. 0
Kifungu 2327 - <i>Judiciary Delivery Unit</i>	Sh. 0

(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 41 – WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Division</i> ...Sh.	7,358,598,000
---	---------------

(Kifungu Kiliviyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 55 – TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Kifungu 1007 - <i>Planning, Monitoring and Evaluation Unit</i>	Sh. 373,616,000
--	-----------------

(Kifungu Kiliviyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI: Mheshimwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123, 3 (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Nakuomba kwamba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Sasa kwa taratibu zetu nitawahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria ya mwaka wa fedha 2021/2022.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa
Mwaka 2021/2022 – Wizara ya Katiba na Sheria
yalipitishwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nyote nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu wake wa Katiba na Sheria na Watendaji wao Wakuu ambao wako hapa pia kwa maandalizi ya bajeti hii ambayo Bunge limepitisha kwa kadri mlivyoomba, haijapungua hata Shilingi. Tunawapongeza sana. (*Makofii*)

Pia tunaamini kwamba mawazo ambayo yametolewa na Kamati yetu ya Bunge ya Katiba na Sheria

na maoni pia yaliyotolewa na Wabunge humu ndani, naamini yote mmeyachukuwa; na kama mlivyosema kwamba mnaenda kuyafanya kazi; na baadhi ya hoja za Wabunge ambazo zinahitaji ufanuzi, basi mtazileta huo ufanuzi kwa maandishi kama mlivyoahidi. Nasi tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa yale yote miliyahidi kwenye bajeti hii kwamba mnaenda kuyatekeleza katika mwaka wa fedha unaofuata kwa maana ya 2021/2022. Tunawatakia kila la heri.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka jana Mheshimiwa Spika alitangaza kuhusu *iftar* inayotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tutakapomaliza hapa, wote mnakaribishwa katika lile eneo mlilokuwa mmekaribishwa na Mheshimiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, ni pale pale, ndipo ambapo *iftar* ya Waziri Mkuu itakuwa. Kwa hiyo, tukitoka hapa tutaelekea hapo, halafu kwa wale ambao watakuwa wanaelekea kwenye kuswali kabla ya kwenda hapo, basi nao watapata fursa.

Kabla sijaahirisha shughuli zetu, yupo mgeni ambaye ameingia mchana huu; na huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido kutoka Mkoani Arusha. Huyu ni Wakili Dkt. Jumaa Mhina. Karibu sana. (*Makofisi*)

Waheshimiwa Wabunge, leo tulikuwa tunazungumza hapa habari za Wizara hii ya Katiba na Sheria na kama Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anavyosisitiza kwamba Serikali ni moja, nasi kama Wabunge, Wawakilishi wa Wananchi tunatamani Serikali iwe inazungumza, kwa maana ya kwamba Watanzania wote wana haki zinazofanana. Mambo yanayotofautiana ni nani anakaa wapi?

Sasa mchana huu nikawa sijalewa vizuri. Sheria zile tulizotunga humu ndani, Mabaraza ya Madiwani yanaporuhusiwa kutunga Sheria Ndogo, ndiyo maana umewekwa utaratibu, Sheria Ndogo ikitungwa haiwezi kufanya kazi kabla haijaja kwa aliyekasimu hayo madaraka

kwa yule mtunga Sheria Ndogo. Ndiyo maana inakuja kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amalize na yeze, naamini na watu wa TAMISEMI wahusike huko, Serikali izungumze.

Nimepata taarifa mchana huu kwamba kuna mahali watu wanachajiwani kwa kupaki vibaya shilingi 200,000 mpaka shilingi milioni moja. Sasa hilo jambo halikubaliki, kwa sababu nimeuliza Dar es Salaam ni shilingi 50,000; nimeuliza hapa Dodoma, nikaambiwa shilingi 50,000; kwingine shilingi 200,000.

Kama chombo ni hicho hicho, kwa nini kwingine nchi hii hii, kuwe bei ndogo na kwingine bei kubwa, wakati Halmashauri zote zinasimamiwa na TAMISEMI? Kwa hiyo, Serikali izungumze, watu wasiwe wanaonewa bila ya sababu. Sheria zinazotumika ni hizi hizi. Zinazowapa mamlaka Dar es Salaam kutengeneza Sheria Ndogo ni hizo hizo zinategenezwa Dodoma na hizo hizo zinatengeneza pengine. (*Makofii*)

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itusaidie, wanapopelekewa hizi, wawe wanaangalia mambo haya yasitofautiane sana kama hakuna sababu. Naamini hilo litakuwa limeeleweka; Serikali ni moja na Mwenye nchi ameshasema, ndio hiyo tunayofuata wote, kauli mbiu ni moja.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.36 Jioni Bunge lilihahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 29 Aprili, 2021Saa Tatu Asubuhi)*